

## **Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)**

**BUNGE LA TANZANIA**

**MAJADILIANO YA BUNGE**

**MKUTANO WA NNE**

**Kikao cha Pili – Tarehe 8 Juni, 2011**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatuh Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa mezani na:-

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU):**

Mpango wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano, 2011/2012 - 2015/2016  
(*The National Five Year Development Plan, 2011/2012 - 2015/2016*).

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. GREGORY G. TEU): -**

Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2010 na Mwelekeo wa Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2011/2012.

Taarifa ya Sera za Fedha kwa Kipindi cha Mwaka 2010/2011 na Mwelekeo wa Sera za Fedha kwa Mwaka 2011/2012.

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 11

**Maslahi ya Madiwani na Vyombo vyatya Usafiri**

**MHE. PROF. PETER M. MSOLLA (K.n.y. MHE. DEO FILIKUNJOMBE)**  
aliuliza:-

Madiwani ni wawakilishi wa karibu sana na wananchi lakini mazingira ya kazi zao ni magumu kutohana na maslahi madogo na kutokuwa na vyombo vyatya usafiri:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha maslahi ya Madiwani wote hapa nchini?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuwakopesha madiwani wa Ludewa vyombo vya usafiri kama vile pikipiki ili waweze kuwahudumia wananchi kwa ufanisi zaidi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Deo Filikunjombe, Mbunge wa Ludewa, swalii lake lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua kuwa Waheshimiwa Madiwani ni Viongozi walio karibu sana na wananchi na ndio wasimamizi wakuu wa shughuli za maendeleo katika Kata zao. Kwa kuzingatia hilo Serikali imekuwa ikiboresha maslahi yao ikiwemo posho na stahili mbalimbali kwa lengo la kuboresha usimamizi katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo ngazi ya Kata.

Mheshimiwa Spika, suala la maslahi ya Waheshimiwa Madiwani limekuwa likijadiliwa mara kwa mara na Serikali imekuwa ikiboresha maslahi hayo kadri hali ya uchumi wa nchi inavyoimarika. Katika mwaka wa fedha 2007/2008, Serikali ilitekeleza ahadi yake ya kuongeza posho za madiwani kama ifuatavyo: -

(i) Posho ya mwezi shilingi 120,000/- ambapo shilingi 60,000/- ni ruzuku ya Serikali Kuu;

(ii) Posho ya kikao shilingi 40,000/-; na

(iii)Posho ya madaraka kwa Wenyeviti/Mameya viwango ni kati ya shilingi 100,000 na 350,000/-.

Mheshimiwa Spika, ikumbukwe kwamba idadi ya madiwani imeongezeka kutoka madiwani 3,425 kati ya mwaka 2005 - 2010 hadi 4,451 mwaka 2011. Ongezeko hili la madiwani haliendani na kasi ya kuimarika kwa uchumi wa nchi na hivyo kuwa vigumu kwa Serikali kutimiza azma ya kuboresha maslahi ya madiwani kwa kipindi hicho. Aidha, azma ya Serikali ni kuendelea kuboresha maslahi ya madiwani ipo pale pale kwa kadri hali ya uchumi inavyoruhusu.

(b)Mheshimiwa Spika, pamoja na nia njema ya kuwarahisishia utendaji madiwani kwa kuwapa vyombo vya usafiri; Sheria za Serikali za Mitaa, Sheria ya Fedha za Umma, Mwongozo wa Bajeti, Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa hazitoi mwanya kwa Halmashauri kuwakopesha, kuwadhamini, kuwanunulia wala kuwachangia

madiwani gharama za kununua vyombo vya usafiri. Bado Serikali inaendelea kuzingatia upya Sheria za Serikali za Mitaa ili kuhakikisha kwamba zinaendana na wakati tulio nao.

**MHE. PROF. PETER M. MSOLLA:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kumshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake fasaha na mazuri.

Je, katika kuwawezesha kufanyakazi vizuri Serikali iko tayari kuwafikiria hawa Waheshimiwa Madiwani ambao ni nguzo moja katika zile tatu, mafiga matatu ili waweze kukopeshwa na vyombo vya fedha wapate usafiri wa kuaminika ili kuweza kuwafikia wananchi jirani zaidi kama inavyofanywa kwa Wabunge? (Makofi)

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Prof. Peter M. Msolla, Mbunge wa Kilolo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ninaomba nikuhakikishie tu kwamba nimepita mimi mikoa karibu yote ya Tanzania sasa hivi, hakuna kitu kinachozungumziwa sasa hivi kama suala la maslahi ya Madiwani, na baada ya ku- *introduce* kitu kinachoitwa *D by D* kwa maana ya kutoa madaraka zaidi kwa wananchi na wakati huo huo kupeleka nyenzo raslimali.

Majukumu ya Waheshimiwa Madiwani yameongezeka maradufu. Nina hakika na ninasema hayo ili kuzuia maswali mengine yasije yakaulizwa hapa kwamba ni kweli hakuna mtu ye yote asiyona umuhimu wa Madiwani; tumezungumza habari ya shule za sekondari wale ndiyo ambao wamefanyakazi ya kuzijenga hizo shule za sekondari, tumezungumza habari ya Zahanati wale ndiyo wanafanyakazi hiyo, sasa hivi tunazungumza kila Tarafa iwe na *A-Level* Madiwani ndiyo wanafanyakazi hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo Wabunge wasije wakachukua muda mrefu hapa kutaka kuuliza maswali kama vile hatuelewi jambo hili. Mheshimiwa Waziri Mkuu analijua jambo hili, Mheshimiwa Rais wa nchi anafahamu jambo hili, Waziri wa nchi na Serikali wote tunajua kwamba madiwani wana-play role muhimu na ninaomba nichukue nafasi hii kwa niaba ya Serikali kuwapongeza Madiwani kwa kazi nzuri wanayoifanya katika nchi hii. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, hili linalozungumzwa hapa ukisoma kwenye Ripoti ya Lubeleje wa Mpwapwa anazungumza mle ndani, mimi Serikali ikitamka hapa ikasema kutoka sasa Madiwani wanaruhusiwa wapewe vyombo vya usafiri kwa kukopeshwa kwa kiherehere changu nitakimbia haraka hapa kuja kusema kwamba jamani imekubalika.

Kwa hiyo ninachosema hapa na mimi ninashiriki kuiomba Serikali ione umuhimu wa jambo hili. (Makofi/Kicheko)

**SPIKA:** Tunaendelea, amesema msiulize swali. Kwa hiyo tunaendelea swali linalofuata.

Na. 12

**Uhitaji wa Jokofu na Chumba cha Kuhifadhi Maiti Hospitali ya Wilaya,  
Kisarawe**

**MHE. SELEMANI S. JAFO** aliuliza:-

- (a) Lini chumba cha kuhifadhia maiti kitawekwa jokofu katika Hospitali ya Kisarawe?
- (b) Lini atapatikana mtaalam wa kutoa dawa za usingizi katika Hospitali ya Kisarawe?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOZA NA  
SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Selemmani S. Jafo, Mbunge wa Kisarawe, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Spika, Hospitali ya Wilaya ya Kisarawe inacho chumba cha kuhifadhia maiti chenye uwezo wa kuhifadhi maiti kwa siku moja tu. Mpango wa Serikali ni kufanya upanuzi na ukarabati mkubwa wa chumba cha kuhifadhia maiti na uweki jokofu ifikapo mwaka 2012/2013. Chumba hicho kitakapokamilika kitakuwa na uwezo wa kuhifadhi maiti sita (6).

Huduma ya kuhifadhi miili ya marehemu kwa sasa inafanyika katika hospitali ya Amana na Temeke ambazo zipo karibu umbali kwa kilometra 9 kutoka Kisarawe. Kutohana na ukomo wa Bajeti ya Halmashauri kwa mwaka 2011/2012 imeweka kipaumbele cha ujenzi wa nyumba za waganga katika kituo cha afya cha Chole na katika zahanati mbili (2) zilizokamilika.

(b) Mheshimiwa Spika, Halmashauri katika mwaka 2011/2012 imepanga kuwapeleka masomoni madaktari wawili (2) wa kutoa dawa za uzingiti katika Chuo cha Udaktari *KCMC* ili kukidhi upungufu wa madaktari katika hospitali ya wilaya. Aidha, halmashauri imeomba madaktari watano (5) wa fani mbalimbali za udaktari pamoja na waugazi kutoka Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii katika Bajeti ya 2011/2012.

**MHE. SELEMANI S. JAFO:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri naomba kuuliza maswali ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali ina mipango ya kufanya ukarabati wa ujenzi wa hicho kitengo maalum cha kuhifadhia maiti, tena kwa mwaka wa fedha ujao:-

(a)Je, Serikali ina mipango gani kuhakikisha kwamba kufanyike juhudi ya haraka ili mradi wakazi wa Kisarawe waweze kupata fursa ya kutumia mafungu yake mbalimbali kuhakikisha kwamba watu wa Kisarawe wasiweze kupata adha ya kupeleka maiti katika Jiji la Dar es Salaam.

(b)Kwa kuwa tumeona kwamba wataalam wa usingizi wilaya ya Kisarawe hawapo na hivi sasa wananchi wa wilaya ya Kisarawe wanapata shida kubwa sana.

Je, Serikali haioni sababu ifanye juhudi za makusudi kabla ya hao kupelekwa *KCMC* lakini apatikane mtu mwingine wa haraka ili mradi huduma za oparation ziweze kuendelea katika hospitali ya Wilaya ya Kisarawe?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Selemani S. Jafo, Mbunge wa Kisarawe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mimi naelewa Mheshimiwa Jafo anachozungumza hapa. Anachozungumza hapa ni kwamba maiti ikipelekwa pale huwezi kulaza pale kwa siku mbili kwa sababu hakuna jokofu, hakuna kitu chochote na kama alivyoeleza hapa wanachukuliwa hao wanapelekwa Amana, Amana ni kule mjini Dar es Salaam ambapo *traffic jam* na matatizo mengine mengi yanazungumzwa hapa.

Mimi sitaki nibishane hapa na Mheshimiwa Mbunge, nataka nimwambie nimezungumza mimi na Mkurugenzi nikamwuliza kwenye Bajeti hii tunayokwenda nayo mmeliweka hili jambo humo? Ananiambia sisi tumepanga kuweka nyumba za waganga.

Suala la hela za kupeleka katika *mortuary* ni suala la *priority* na maoni yangu mimi suala hili linalozungumzwa hapa ni jambo kubwa. Kwa hiyo, ninamwomba Mheshimiwa Mbunge tushirikiane nae twende tuzungumze jambo hili vizuri tuone umuhimu wa kuanzisha hiyo *mortuary* pale ili wananchi waweze kusaidiwa katika jambo hili, wala sioni problem katika jambo hilo ni suala la kupanga tu vipaumbele vile.

Mheshimiwa Spika, la pili hili analozungumza madaktari ambao watasaidia kuhusu suala hili la kaputi, pale ni kweli kabisa huwezi kuweka mtu ni mtu pale unawenza ukamweka mtu akamlaza mtu usingizi akalala moja kwa moja asiamke tena. Sasa nikimbishia hapa nikamwambia, naomba Mheshimiwa Mbunge tutakapomaliza hapa tutawasiliana na wenzetu wa Wizara ya Afya tuzungumzie jambo hili kwa sababu anazungumzia hata kama mtapeleka *KCMC* tufanye ili tuone uwezekano wa kumpata walau mtu mmoja ambaye atapelekwa pale asaidie wakati tunapeleka watu *KCMC*. (*Makofii*)

**MHE. SULEIMAN M. NCHAMBI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Kwa niaba ya wananchi wa wilaya na jimbo la Kishapu kwa kuwa sisi hatuna kabisa chumba

cha kuhifadhia maiti, hatuna hospitali ya wilaya. Je, Serikali haioni umuhimu wa kuwasogezea wananchi wa jimbo la Kishapu hospitali kwa taabu wanazozipata hasa akina mama Mheshimiwa Spika kama wewe wanapata taabu kwa kusafiri kilomita zaidi ya 150 kwenda kujifungua Shinyanga Mjini?

Naomba Mheshimiwa Waziri anihakikishie hapa. Je, haoni umuhimu wa afya za wanawake na wananchi wa jimbo la Kishapu kupata huduma ya hospitali ya Wilaya?

**SPIKA:** Hapo umeni-*black mail* sasa. (*Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Suleiman M. Nchambi, Mbunge wa Kishapu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa bahati nzuri Kishapu yenyewe nimefika sijui kama wakati ule mheshimiwa alikuwa ni Mbunge, nafikiri yeye ni mpya. Analosema hapa ni kweli jana nilikuwa najibu swali hapa kuhusu hospitali za wilaya, wilaya hizi mpya zinazoanza sasa hivi ukisema kwamba zote kwa mpigo utazipa hospitali za wilaya *it is impossible*, haitawezekana.

Nilichosema jana maoni ya serikali ni kwamba hebu kila wilaya mpya itafute mahali ambapo tutaanza katika kipindi cha mpito. Useme hapa kwenye kituo cha afya ndipo tutakopatumia kama hospitali ya wilaya mpaka hapa tutakapokuwa tumefika mahali ambapo tunajenga hospitali ya wilaya, hivyo ndivyo ninavyoamini kwamba inaweza ikasaidia na ndivyo Serikali inavyoamini. Kwa hiyo, ninachomwomba Mheshimiwa Mbunge wa Kishapu wao wa-*identify* ili waweze kupewa ile heshima inayolingana na hospitali ya wilaya wakati tunaendelea kusaidia jambo hilo.

Mheshimiwa Spika, isisahaulike hapa kujenga hospitali ya wilaya unazungumza habari ya bilioni tisa (9). Kwa hiyo, ninachosema hapa amezungumza habari ya akina mama; akina mama ndio wanaotuleta hapa duniani, mimi siwezi kusimama hapa nikasema kwamba tusiwasaidie akina mama, akina mama wasaidiwe na tuwasaidie kwa utaratibu na sisi wote tunaona umuhimu huo. (*Kicheko*)

**SPIKA:** Hasa Spika akiwa mwanamke ndiyo lazima? (*Kicheko*)

**MHE. MUNDE TAMBWE ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kumwuliza Mheshimiwa Waziri swali la nyongeza.

Mheshimiwa Waziri, kwa kuwa Tabora manispaa ni wilaya ya muda mrefu na kwa kuwa wananchi hao mpaka leo hii hawana hospitali ya wilaya jambo linalosababisha hospitali ya mkoa wa Tabora ambayo inahudumia wilaya sita ( 6 ) za mkoa mzima wa Tabora kuwashudumia wananchi wa Tabora manispaa hivyo

inawasababishia kukosa huduma muhimu kiasi kwamba hata kama mtu amejikata na jembe ni lazima aende hospitali ya mkoa;

Je, Serikali inatwambiaje kuhusu kutujengea hospitali ya wilaya ndani ya Tabora manispaa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Munde A. Tambwe, sijui kama nililipata vizuri jina lake anisamehe kama nitakuwa nimekosea.

Mheshimiwa Spika, kuhusu hili suala la manispaa. Manispaa pale tatizo lililopo nimefika ni kwamba kuna *congestion* kwa sababu zile hospitali zote, Uyuyi wote wanakwenda pale ndiyo tatizo lililopo pale. Wangeweza wakawa na *advantage* wakatumia huduma ile lakini sasa panajazana pale kwa sababu watu wote wanategemea hapo.

Mheshimiwa Spika, jibu ni lile lile ninachosema hapa manispaa ya Tabora ikae chini iseme hivi sisi tunajua tuna hospitali ya mkoa hapa kuna *congestion* pale lakini petu tunapofikiri kwamba hii tuitambue kama hospitali ya wilaya ni hapa, halafu wakati huo sasa tuanze kuzungumza habari ya kuwa na hospitali ya Manispaa. Kuna *issue* ya *designated hospitals* unaweza ukaenda ukamwona Baba Askofu, ukaenda BAKWATA kama wana hospitali pale ikakubalika kuwa hii itumike *in the mean time* kwa ajili ya kazi ile tunafanya hivyo.

Kwa hiyo, mimi nashauri kwamba tuyaaangalie haya yote lakini sisi kama Wizara tuko tayari kushirikiana na Mheshimiwa Mbunge ili tuone ni jinsi tutakavyosaidia katika tatizo hili la msongamano ulioko pale manispaa ya Tabora.

**SPIKA:** Ahsante, kwa hiyo ni ushauri kwa wote.

Na. 13

**Barabara ya Kinyanambo – Mlimba**

**MHE. MAHMOUD H. MGIMWA** aliuliza:-

Barabara itokayo Kinyanambo – Itimbo- Usokami – Kibengu – Mapanda, Ukame, Kisusa mpaka Mlimba Wilayani Kilombero ni muhimu sana kwa maendeleo ya Taifa letu, kwani ndiko kwenye Bwawa la Kihansi na pia kuna vyura ambao hawapatikani sehemu yeote Duniani:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kujenga barabara hiyo yeny urefu wa kilomita 116?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mahmoud H. Mgimwa, Mbunge wa Mufindi Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara itokayo Kinyanambo – Itimbo – Usokami – Kibengu, Ukama, Kisusa mpaka Mlimba Wilayani Kilombero yeny urefu wa kilomita 112 ni barabara ya Wilaya inayohudumiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi.

Mheshimiwa Spika, barabara hii inaunganisha Wilaya za Mufindi kwa mkoa wa Iringa na Kilombero kwa mkoa wa Morogoro na inapitia katika maeneo muhimu yeny rutuba kwa uzalishaji wa mazao ya misitu ya mbao na matunda na pia hupita kwenye kituo cha uzalishaji umeme cha Kihansi. Aidha, barabara hii imekuwa ikifanyiwa matengenezo ya kuimarisha sehemu korofi mwaka hadi mwaka na kuifanya barabara hiyo iweze kupitika.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua umuhimu wa barabara hii, Halmashauri katika Bajeti yake ya mwaka 2010/2011 ilitenga shilingi milioni 80 kutoka Mfuko wa barabara kwa ajili ya matengenezo ya sehemu korofi za barabara hiyo yaani *spot improvement*. Aidha, Halmashauri inaendelea kufuatilia upatikanaji wa fedha hizo ili kuifanya matengenezo barabara hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua umuhimu wa barabara hii Mkoa wa Iringa kupitia kikao chake cha Bodi ya Barabara kilichofanyika tarehe 1 Machi, 2011 ambacho Mheshimiwa Mahmoud H. Mgimwa ni mjumbe, kiliazimia kupeleka maombi Wizara ya Ujenzi kwa ajili ya kuipandisha hadhi. Maombi hayo yamewasilishwa Wizara ya Ujenzi na yanafanyiwa kazi kwa mujibu wa Sheria ya Barabara Na. 13 ya mwaka 2007 na Kanuni zake za mwaka 2009. (*Makofi*)

**MHE. MAHMOUD H. MGIMWA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya kisiasa ya Naibu Waziri napenda kutoa masikitiko yangu. Kwanza amekiri kwamba Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi haina uwezo wa kutengeneza hiyo barabara kwa sababu inaunganisha baadhi ya maeneo na maeneo mengine. Sasa hivi wananchi katika eneo hilo wanatembea zaidi ya kilomita 50 kwenda mjini kwa ajili ya kupata huduma muhimu. Sasa nasema ni lini Serikali itatambua tatizo hilo na kusaidia kuchukua barabara hiyo ili iwe na hadhi ya Kimkoo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, kwanza labda nimweke vizuri hapa kinachozungumzwa ni siasa. Hapa tunazungumza ni namna ya ku-allocate resources za nchi kwa ajili ya maendeleo yetu ni *politics* hizo. *Politics* ni *reflection* ya *economics* na *economics* ni *reflection* ya *economics*. (*Makofii*)

Nataka nimhakikishie ndugu yangu na nimepanga kwamba nitakwenda Mkoo wa Iringa kwa ajili ya kufuatilia hii barabara. Hakuna majibu ya kisiasa yanayotolewa hapa swali limeulizwa hivi kuna mkakati gani wa kusaidia barabara hii. Mkakati tukasema kwamba tui-*promote* hii barabara, tumwombe Waziri wa Ujenzi haipokee barabara hii kwa sababu Halmalshauri ya Wilaya ya Mufindi uwezo wake ni mdogo. Amekwenda Mkuu wa Wilaya kukagua hii barabara, amekwenda Mkurugenzi Mtendaji kwenda kukagua hii barabara na wanansikiliza huko waliko, wamekwenda kuangalia yote hayo na haya anayosema Mheshimiwa Mbunge ni kweli.

Mheshimiwa Spika, majibu haya ni ya kisiasa naomba unihurumie sauti yangu hii huwa inapanda kwa sababu ya kuamini katika jambo hili sio sauti. Nataka tu nimhakikishie hii barabara tunamwomba Mheshimiwa Pombe Magufuli ambaye ndiye mwenye dhamana na tumezungumza nao wamesema wata-*consider* kesi ya ku-*promote* hii barabara ili mzigo wa kubeba hii barabara uhamie Wizara ya Ujenzi ambayo ina unafuu katika suala hilo. Nashukuru sana. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante tunasubiri Wizara ya Ujenzi tunaendelea na Ofisi ya Makamu wa Rais. Atakayeuliza swali ni Mheshimiwa Mwanamrisho Taratibu Abama.

Na. 14

### **Mgao wa Mapato ya Muungano**

#### **MHE. MWANAMRISHO TARATIBU ABAMA aliuliza:-**

Kwa muda mrefu kumekuwepo mchakato wa kuangalia utaratibu wa kutumia katika ugawaji wa mapato ya Muungano na mapato sasa hakuna taarifa iliyotolewa kuhusu kukamilika kwa utaratibu huo:-

(a) Je, Serikali inatoa tamko gani ili wananchi wawe na taarifa sahihi kuhusu mgao wa mapato ya Muungano?

(b) Je, ni lini mgao huo wa mapato utaanza ili kila upande uweze kufaidika?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO)** aliibuu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mwanamrisho Taratibu Abama, Mbunge wa Viti Maalum, lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a)Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inaelewa umuhimu wa kuwepo kwa utaratibu si katika ugawaji wa mapato tu bali hata uchangiaji wa gharama za Muungano. Kwa kutambua jambo hilo Serikali imeunda Tume ya Pamoja ya Fedha kwa mujibu wa Ibara ya 133 na 134 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977. Tume hii imeshatoa mapendekezo ya vigezo vya kuchangia gharama za Muungano na mapendekezo ya kugawana mapato ya Muungano kwa Serikali zetu mbili. Mapendekezo hayo bado yanafanyiwa kazi kwa ajili ya kutoa maamuzi.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo Serikali zetu mbili ziliweka utaratibu wa muda wa kugawana misaada ya kibajeti itokanayo na faida ya Benki Kuu ya Tanzania ambapo Zanzibar inapata asilimia 4.5. Aidha, eneo jingine ni mapato yatokanayo na uvuvi wa bahari kuu ambapo Serikali zote mbili zimekubaliana kuwa Mamlaka ya Uvuvi katika bahari kuu itapata jumla ya asilimia 50 ya mapato yote kwa ajili ya kugharamia uendeshaji wa Mamlaka na majukumu yake na asilimia 50 iliyobaki itagawanywa kwa asilimia 60 kwa Tanzania Bara na asilimia 40 kwa Zanzibar.

(b)Mheshimiwa Spika, kama nilivyokwishaeleza kwa sasa Serikali zetu zipo katika mchakato wa kupitia kwa makini mapendekezo yaliyotolewa na Tume ya Pamoja ya Fedha ili kufanya maamuzi sahihi kwa faida ya Watanzania wote au kwa faida ya pande zote mbili za Muungano. Uamuzi ukishatolewa viwango vipyta vitakavyotumiwa na Serikali zetu ndivyo vitakavyotumika katika kugawa mapato ya Muungano na kuchangia gharama za Muungano. Nawaomba Waheshimiwa tuvute subira kidogo mpaka hapo muafaka utakapatikana.

**MHE. MWANAMRISHO TARATIBU ABAMA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri naomba nimwulize suala moja la nyongeza.

Kwa kuwa utaratibu wa mgao mpya wa mapato ndio kwanza unataka kuanza au unashiriki maamuzi ya Serikali zote mbili. Je, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inatoa kauli gani kuhusu kufidia siku ambazo Serikali ya Zanzibar imekosa mgao huo? (*Makofî*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO):** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema awali kwamba Serikali zetu mbili ziko katika kujadiliana kuhusu mgao wa fedha hizo. Katika majadiliano hayo kama suala la fidia litakuja basi nalo litajadiliwa na wataafikiana ipasavyo. Ahsante sana.

**MHE. NIMROD E. MKONO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniona. Kwa kuwa suala hili la Muungano na mzozo kati ya Serikali ya Zanzibar na ya Bara ni suala ambalo mmeli-*prevail* kwenye Katiba kama kuna manung'uniko wa mgao wa fedha kwa nini basi hilo Baraza la Usuluhishi kati ya Serikali hizi mbili halijaanza kutumika maana matatizo yote yanalenga pale pale. Kwa nini basi hiyo Sheria ya Katiba isitumike mapema iwezekanavyo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO):**  
Mheshimiwa Spika, kama alivyosema kwamba kuna mgogoro na hivyo Baraza la Usuluhishi lifanye kazi hiyo. Nataka kutoa taarifa kwamba kwanza hakujaundwa Baraza la Usuluhishi na hii ni kwa sababu hakuna mgogoro ila kuna changamoto zitokanazo na Muungano na kuna Kamati inayoshughulikia hayo. Lakini pia inapotokea haja Tume kama *GFC* itaundwa ili kutoa mapendekezo. Kwa hiyo, hamna mgogoro na kwa hiyo Baraza la Usuluhishi halijaundwa. Ahsante sana. (*Makofit*)

Na. 15

### **Idadi ya Wizara Zinazohusiana na Mambo ya Muungano**

**MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO** aliuliza:-

- (a) Je, kuna Wizara ngapi katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania?
- (b) Je, ni Wizara ngapi zinahusiana na Mambo ya Muungano baina ya Tanzania Bara na Tanzania Visiwani?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Kombo Khamis Kombo, Mbunge wa Mgogoni, lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Idadi ya Wizara za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imekuwa ikibadilika mara kwa mara kutokana na Rais anayekuwepo madarakani anavyoona inafaa kutekeleza kazi zake kulingana na mamlaka aliyopewa na Katiba. Kwa mujibu wa Tangazo la Serikali Namba 494 la tarehe 17 Desemba, 2010 kwa sasa kuna Wizara 26 zinazoongwa na Mawaziri 29.

(b) Mheshimiwa Spika, jibu ni kwamba zipo jumla za Wizara 6 ambazo ni za Muungano, Wizara hizo ni Ofisi ya Makamu wa Rais inayoshughulika na Mambo ya Muungano, Wizara ya Fedha kupitia GFC, BOT na Sera za Kifedha, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa. Aidha, zipo Wizara ambazo si za Muungano lakini zinasimamia masuala ya Muungano kama yalivyoordheshwa katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977. Mfano Wizara hizo ni Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma ambao hushughulika na suala la Utumishi katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano.

Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu na Bunge ambayo husimamia masuala ya Bunge, Wizara ya Nishati na Madini ambayo husimamia suala la mafuta na gesi asilia, Wizara ya Katiba na Sheria ambayo husimamia suala la Katiba ya Jamhuri ya Muungano

wa Tanzania, Wizara ya Viwanda na Biashara ambao husimamia masuala ya Biashara za Nje, Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia inayosimamia Masuala ya Mawasiliano, Wizara ya Uchukuzi ambayo husimamia suala la usafiri wa anga na majini na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundu ambayo husimamia suala la Elimu ya Juu na Baraza la Mitihani la Taifa.

**MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa Wizara zinazohusiana na mambo ya Muungano ni 6. Na kwa kuwa tuna nia ya dhati ya kulinda na kuuenzi Muungano wetu. Na kwa kuwa kuna kero mbalimbali ambazo zinalalamikiwa na pande mbili zinazohusiana na Muungano.

Je, Serikali haioni kwamba kuna haja sasa ya kuleta mabadiliko ya uwepo wa muundo wa Serikali tatu ambazo zitaondosha kero za Muungano? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pili, kabla ya kuletwa Muswada huo, je, Serikali hii kero ya mgao wa asilimia 4.5 inayopewa Zanzibar kutoka katika Muungano itapatiwa ufumbuzi lini na limekuwa ni suala la kila siku?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO):** Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la Serikali tatu. Naomba wananchi wafanye wajibu wao wa kuchangia vizuri katika marekebisho ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tunayotegemea kuyafanya hivi karibuni. Na kwa maana hiyo kama wapo wanaohisi Muungano utanawiri vizuri katika muundo wa Serikali tatu, basi wakaeleze huko pamoja na sababu zao.

Suala la mgao wa asilimia 4.5 kama nilivyojibu katika swali namba 14 kwamba suala hili linafanyiwa kazi na pale Serikali mbili zitakapoafikiana basi jibu muafaka litatoka. Ahsante sana.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

Tokea Tume ya Pamoja ya Fedha iundwe kwa mujibu wa Sheria Namba 15 ya mwaka 1994 ilipeleka mapendekezo yake Serikalini...

**SPIKA:** Mheshimiwa hili swali la pili hili?

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Ndilo hilo hilo inahusiana na Tume.

**SPIKA:** *Okay endelea.*

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Ikiwa ni pamoja na Wizara zote za Muungano, mapato yake na mgawano wake tokea mwaka 2006 wamepeleka mapendekezo yake.

Lakini Serikali mbili zimeshindwa kuamua matokeo yake Tume ilikuwa haina kazi tena inakaa inasubiri matokeo ya Serikali ambayo yamepelekwa toka mwaka 2006.

Je, haioni Serikali kwa kitendo hicho inaendelea kuvunja Katiba ya Nchi kifungu hicho ambacho Waziri amekisema cha 130 ambayo inatakiwa Serikali hizi mbili zichangie Mfuko wa Muungano na mapato yake yaweze kujulikana. Huoni Serikali inaendelea kuvunja Katiba?

**SPIKA:** Mheshimiwa kwa kweli swalilile la 14, lakini hili ni la 15 na Mheshimiwa naomba ujibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI WA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO):**  
Mheshimiwa Spika, majibu ni yale yale kama nilivyosema suala linakera 4.5 pengine Tume imependekeza kiwango kikubwa zaidi ya hiki, lakini kama nilivyosema Serikali zetu mbili zinalifanyia kazi kwa manufaa ya pande zote mbili. Kwa hiyo, litakapomalizwa kufanyiwa kazi majibu muafaka yatatoka. Ahsante sana. (*Makofî*)

Na. 16

**TRA Kuanzisha Utaratibu wa Kupitia Nyaraka za  
Mizigo Bandarini Kwa Saa 24**

**MHE. MUSSA ZUNGU AZZAN** aliuliza:-

Wafanyabiashara wengi hapa nchini wamekuwa wakilalamikia utaratibu wa utoaji wa mizigo bandarini unaotumika kwa sasa ambao hupelekeea ucheleweshaji na wafanyabiashara kutozwa gharama kubwa; utaratibu huo wa ucheleweshaji wa kutoa mizigo bandarini hasa kwa Mamlaka ya Mapato (TRA) ambayo shughuli za ukaguzi wa nyaraka za mizigo hufungwa saa 11 jioni, umesababisha wafanyabiashara wengi kukimbia Bandari yetu na kutumia Bandari za nchi jirani.

Je, Serikali itakuwa tayari kuielekeza TRA kuanzisha utaratibu wa kupitia nyaraka za mizigo kwa masaa 24 kama ilivyo kwenye viwanja vya ndege ili kuwavutia wafanyabiashara waendelee kutumia bandari hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. GREGORY G. TEU)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, napenda kujibu swalilala Mheshimiwa Mussa Zungu Azzan, Mbunge wa Ilala, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania imekuwa ikichukua hatua zinazolenga katika kuharakisha ushughulikiwaji wa kadhia na nyaraka

zinazotumika katika kuingiza bidhaa nchini. Moja kati ya hatua zilizochukuliwa ni kuongeza muda wa kufanya kazi ili kuharakisha utoaji wa shehena katika vituo vyatipaka yetu.

Kwa sasa muda wa kufanya kazi katika kituo kinachoshughulikia kadha na nyaraka za uingizaji wa bidhaa (*Central Data Processing Office*) umeongezwa hadi kufikia saa mbili usiku kwa siku za kawaida na siku za Jumamosi kuanzia saa mbili asubuhi mpaka saa saba mchana. Kwa sasa kituo hiki kinaweza kupitisha kadha zinazowasilishwa zikiwa zimekamilika na bila makosa ndani ya siku mbili.

Mheshimiwa Spika, Serikali tayari imeshaelekeza Mamlaka ya Mapato kuongeza muda wa kufanya kazi ili kuondoa msongamano na ucheleweshaji wa kuondoa mizigo.

Napenda nitoe taarifa kwa Bunge lako Tukufu kwamba usimamizi wa utoaji wa mizigo bandarini Dar es Salaam hususan makontena kupitia lango namba 5 hufanyika kwa saa 24 na kupitia lango namba 3 hufanyika kwa saa 18 siku za kazi. Utaratibu huu wa kuongeza muda wa kushughulikia bidhaa unalenga katika kufanya kazi kwa masaa 24 kulingana na mahitaji ya maeneo husika.

**MHE. MUSSA ZUNGU AZZAN:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu ya Mheshimiwa Waziri, lakini kwa utaratibu huu bado bandari yetu inakimbiwa. Gharama za kupitisha mizigo bandari yetu ni kubwa mno na hii inatokana kwa TRA hawafanyi kazi masaa 24 kama bandari zingine duniani.

Mimi namwomba ili ku-*champion revenue* vizuri katika bandari hii na maeneo ya tipaka yetu Serikali na TRA sasa ianzishe utaratibu wa TRA ku-clear mizigo na kuwa na *shift* za masaa 24 ili tuweze kurudisha imani ya uagizaji mizigo kutoka Malawi, Rwanda, Zambia ambayo wameikimbia bandari yetu. (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. GREGORY G. TEU):** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa namshukuru kwa kuona umuhimu wa kuweza kuboresha kero ambazo zinatokea ili kuweza kuharakisha kutoa mizigo bandarini.

Lakini suala la kuongeza masaa kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi ni kwamba kuongeza masaa kuna ukomo. Kama nilivyosema jibu la msingi kwamba tumeshaongeza tipaka masaa 24 kwa siku yaani siku nzima mchana na usiku na siku za kawaida tumeongeza masaa 18 kwa hiyo suala la masaa lina ukomo.

Mheshimiwa Spika, ninavyoona hapa suala la msingi ni kwamba jitihada ambazo zinafanywa na TRA ni kwamba ni lazima tuongeze teknolojia mpya, teknolojia mpya ndiyo itakayosaidia kazi hii ya kutoa kero ya bandarini na sasa hivi ninavyoongea ni kwamba kuna mazungumzo ambayo yanaendelea ili kuboresha teknolojia ya kisasa ili kuweza kuharakisha mizigo bandarini na mazungumzo yanaendelea wenzetu Wakorea wamejitokeza kwamba watatusaidia katika upande wa teknolojia na mazungumzo yanaendelea kuboresha zaidi teknolojia na kuongeza masaa ya kufanya kazi. Kwa hiyo,

tatizo baada ya kuongeza masaa na teknolojia kwa sambamba yatasaidia zaidi katika kuboresha utoaji wa mizigo bandarini.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniona na mimi pia napenda nimwulize Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba ucheleweshaji wa mizigo bandarini unatokana na msongamano wa mizigo.

Je, Serikali haioni kwamba kuna umuhimu wa kuanzisha bandari kavu hasa katika mkoa wa Singida ili kupunguza msongamano wa mizigo ya nchi za jirani na nchi jirani waweze kuchukulia mizigi bandari kavu katika Mkoa wa Singida?

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

**SPIKA:** Aisee! Kutoka bandarini mpaka Singida? Mheshimiwa Naibu Waziri labda una utaalam huo. (*Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. GREGORY G. TEU):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa Martha Mlata, kama ifuatavyo.

Bandari kavu mpaka Singida nafikiri ni ushauri amba ni mzuri kwa sababu Singida nako vilevile kama mizigo itakuwa inapokelewa pale baada ya kutoka bandarini Dar es Salaam ni vizuri zaidi. Ushauri wake unachukuliwa, unapokelewa na tutaangalia jinsi ya kuboresha hata tupate bandari kavu ambapo tutaweza kupokea mizigo yetu. Lakini kwa nyongeza zaidi ni kwamba bandari za Tanga na Mtwara zinapanuliwa na hizo za nchi kavu nazo ikibidi tutafanya hivyo.

**SPIKA:** Kwa nini usiseme tu litafanyiwa kazi? Naomba usema litafanyiwa kazi maana yake vitu vingine naona haiwezekani. Tunaendelea na Mheshimiwa Halima Mdee, swalii la nyongeza.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Hivi karibuni tarehe 1 Juni, 2011 TRA imeanzisha mtindo mpya wa kukadiria kodi za mizigo na hususani mizigo ya magari ambapo badala ya kuangalia gharama halisi ya manunuzi ya mizigo husika wamekuwa wakijiwekea vigezo vyao wenyewe matokeo yake mteja anajikuta analipa kodi kuliko hata thamani ya gari alilonunu.

Sasa nilitaka Mheshimiwa Waziri anisaidie kwa kuwa iko chini yake ni vigezo gani mlivyotumia kuanzisha huu utaratibu kandamizi?

**SPIKA:** Itategemea kujibu kwa sababu hili swalii liki kidogo nje lakini kama Mheshimiwa Waziri unaliweza jibu lakini kama huliwezi utajibu siku nyingine.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. GREGORY G. TEU):** Mheshimiwa Spika, naomba nijibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo;

Swala hili ni jipya kwa hiyo ninaomba aliletu rasmi halafu nitaliingiza kwenye mchakato na litajibiwa kikamilifu. (*Makofit*)

**SPIKA:** Inaruhusiwa hiyo, tunaendelea kwani hatuwezi kuuliza maswali ya nyongeza matano katika swali moja. Kwa hiyo, tunaendelea na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, Mheshimiwa Dkt. Festus B. Limbu.

Na. 17

### **Mpango wa Bima ya Afya ya Jamii**

**MHE. KEBWE S. KEBWE (K.n.y. MHE. DKT. FESTUS B. LIMBU)** aliuliza:-

Serikali imeanzisha Mfuko wa Afya ya Jamii ambapo kila familia inatakiwa kuchangia shilingi elfu kumi ili ipate matibabu na dawa bure kwa mwaka mzima kwenye zahanati, vituo vya afya na hospitali za Wilaya.

(a) Je, Serikali ina taarifa kuwa mpango huu bado haujalewaka vizuri na wananchi walio wengi?

(b) Je, Serikali inafanya mikakati gani ya kuhamasisha na kuelimisha wananchi kuhusiana na mpango huu?

(c) Kwa kuwa, Zahanati na vituo vingi vya Afya huwa havina madawa. Je, Serikali haioni kuwa, wananchi wanaumia kwa kuchangia Mfuko wa Afya ya Jamii na kisha wanaandikiwa wanunue dawa kwenye maduka binafsi?

**SPIKA:** Inategemea kama mabadiliko hayataharibu swali, Mheshimiwa Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, majibu tafadhalii.

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Festus B. Limbu, Mbunge wa Magu, lenye sehemu a,b na c kwa pamoja kama ifuatavyo.

(a) Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba mpango wa Mfuko wa Afya ya Jamii (*CHF*) bado haueleweki vizuri kwa wananchi walio wengi. Hadi kufikia Septemba, 2010 mpango huu ulikuwa unatekelezwa katika Halmashauri 99 kati ya Halmashauri 136 za Tanzania Bara, ambapo jumla ya kaya 424,700 zenye wanufaika milioni 2.7 zilikuwa zimejiunga na kupata huduma kuititia utaratibu huu.

(b) Serikali inaendelea kuzihamasisha Halmashauri kutenga fedha za uhamasishaji kuititia Mipango Kabambe ya Afya ya Halmashauri. Kuwatumia

Wawakilishi wa Wananchi wakiwemo Waheshimiwa Madiwani na Wabunge ambao ndiyo hupitia na kupidisha Mpango ya Halmashauri zao, kuwashirikisha Viongozi mbalimbali katika Jamii wakiwemo Viongozi wa Dini na watu maarufu katika Halmashauri husika, kutoa elimu ya mpango huu na kuwaelimisha wananchi kupidisha Mpango wa Elimu wa Kata kwa Kata unaendeshwa na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya.

(c) Ili kuondoa tatizo la ukosefu wa dawa au kuwaandikia wananchi dawa kununua katika maduka binafsi hususani wanachama wa mfuko wa Bima ya Afya au wanufaika wa Mfuko wa Bima ya Afya, Serikali imechukua hatua zifuatazo:-

(i) Kwamba fedha za dawa zimekuwa zikilipwa moja kwa moja katika Bohari Kuu ya dawa yaani *MSD. (Makofit)*

(ii) Kuendelea kuwasilitiza Waganga Wakuu wa Mikoa, Wilaya na katika vituo vya afya kuwasilisha mahitaji ya dawa mapema katika Bohari Kuu ya dawa ili waweze kupatiwa dawa kulingana na mahitaji yao.

(iii) Bohari kuu ya dawa imeanza mpango wa kusambaza dawa moja kwa moja hadi kwenye vituo vya afya.

(iv) Kuzihusisha Halmashauri kununua dawa kutoka kwenye maduka ya dawa binafsi kwa kutumia vyanzo vingine vya makusanyo vilivyoainsihwa kwa ajili ya matumizi hayo kama vile fedha za Mpango wa Afya ya Jamii (*CHF*), fedha za mfuko wa uchangiaji yaani *Cost Shairing*, fedha za mfuko wa wahisani yaani *Basket Fund* na fedha za huduma ya Vima ya Afya ili kuhakikisha kuwa wananchi wanaendelea kupata huduma ya dawa kama ilivyostahili.

**MHE. KEBWE S. KEBWE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Sehemu a, kutokakana na takwimu za majibu ya msingi inaonekana wanufaika ni wachache sana takribani milioni 2.7, lakini ili Mfuko wa Afya ya Jamii ufanye kazi vizuri, wanufaika angalau wawe 67%, kiwango hiki kiko chini sana.

Je, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya TAMISEMI wana mpango gani?

Sehemu ya b, tunaelewa wazi kwamba kwa bahati nzuri mwaka jana Wizara ya Afya iliweza kuajiri watumishi wapatao 6,700 wapya. Lakini pia Wabunge takribani 65% ni wageni kwa ujumla wake, Chama tawala 70% wageni, wako Madiwani wageni, viongozi wengine katika ngazi ya jamii ni wageni kutokana na Uchaguzi Mkuu wa mwaka juzi 2009 Serikali za Mitaa wakiwemo viongozi wa jamii katika Wilaya na Serikali kwa ujumla.

Je, Wizara ina mpango gani kupandisha uelewa ili kusudi Mfuko wa Afya ya Jamii uweze kupanda?

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Kebwe S. Kebwe, kwa niaba ya mWuliza swali la msingi kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, ni kweli hii tumeona ni mojawapo ya changamoto kubwa ndani ya Wizara yangu namna gani tunaweza tukainua huu Mfuko wa Afya ya Jamii ambao tunaamini ni njia mojawapo ya kuweza kuongeza ufanisi. Kwa hali hii tunaweza tukajazia huduma za afya kwenye upande wa gharama maana Serikali peke yake haiwezi kubeba jukumu hili. Kwa hiyo, vilevile tunawahusisha wananchi kuchangia kwenye huduma hizo za Afya.

Kwa hiyo, huu Mfuko wa Afya ya Jamii kama wananchi wote au kaya zote wangeweza kuchangia kwa ukamilifu, maana yake kama *coverage* ilikuwa 100% kungekuwa na ufanisi mkubwa sana katika upatikanaji wa dawa na vifaa vingine.

Hivyo basi, tuna mpango wa makusudi kwa kushirikiana na TAMISEMI, lakini la kwanza ni kuhakikisha kwamba tujitahidi kwenye vituo vyetu vya afya dawa zipatikane kwa sababu ndiyo kero mojawapo kwamba wananchi hawachangii huu mfuko wa Afya ya Jamii. Wanajiiliza unachangia shilingi 5,000/= au 10,000/= kwa mwaka kwa kaya lakini siku ya pili tu ukienda kwenye zahanati au kituo cha Afya unaambiwa hata *Panadol* ukununue kwenye duka la dawa, hiyo inawakatisha tamaa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo bado tuna kampeni, tutaendesha kampeni na tunaomba Waheshimiwa Wabunge mtusaidie kuwahamasisha zaidi wananchi waelewe umuhimu wao kujunga na huu Mfuko wa Afya ya Jamii.

Lingine ni kutoa sauti ya wananchi kwamba kila Kituo cha Afya, Zahanati, Hospitali ya Wilaya kuna zile *Board* au Kamati za Afya. *Board* au Kamati nyingi siyo hai, lakini hizi zikiwa hai zitatusaidia sana kuweza kusukuma au kusimamia upatikanaji wa dawa na huduma nyingine kwenye Zanahati au Vituo vya Afya ambazo kwao vinaweza vikaongeza uwezo wa wananchi au kuwafanya wananchi waweze kuwa na imani zaidi na wakachangia zaidi ili huo mfuko uweze kutumika.

Ameuliza swali B kuhusu kupandisha uelewa kama alivyosema katika swali la msingi kwamba mojawapo ya vitu ambavyo tunapanga kupandisha uelewa wa wananchi pamoja na ninyi Wabunge tunatumia redio, televisheni na ile kampeni yetu ambayo huu Mfuko wa Afya ya jamii kuitia Bima ya Afya wanaendesha kampeni ya Kata kwa Kata ambao wanahusisha Madiwani na Wabunge ili wawe na uelewa mpana zaidi, faida na namna gani huduma hizi za Mfuko wa Afya ya Jamii unatolewa.

**SPIKA:** Jamani mkishamwita daktari hapa mjue mnapewa Semina ya bure. Kwa hiyo, naomba niendelee na Wizara ya Viwanda na Biashara.

Mheshimiwa Munde Tambwe Abdallah, aulize swali linalofuata.

### **Kuanzisha Kiwanda cha Kukaushia Tumbaku Tabora**

**MHE. MUNDE TAMBWE ABDALLAH** aliuliza:-

Je, Serikali haioni umuhimu wa kuanzisha kiwanda cha kukaushia Tumbaku Tabora hasa ikitiliwa maanani kuwa Tabora ni Mkoa pekee unaolima Tumbaku kwa wingi nchini na kwamba kwa kuanzisha kiwanda hicho kungesaidia kutoa ajira kwa wakazi wa Mkoa huo na kuondokana na umaskini uliokithiri?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Munde Tambwe, Abdallah, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tunanakubaliana na Mheshimiwa Munde Tambwe kuwa kuna umuhimu wa kuanzisha Kiwanda cha Tumbaku Tabora kwa sababu Tumbaku inalimwa kwa wingi katika mkoaa huo. Kiwanda hicho kitakuwa kinaongeza thamani ya Tumbaku inayozalishwa na hivyo kuleta manufaa mbalimbali nchini na hasa kwa Mkoa wa Tabora, kama vile kutoa ajira na kuongeza mapato nchini na hasa kwa Mkoa wa Tabora, kama kwa kuza Tumbaku kwa bei kubwa kutoana na kuongezwa thamani. Hali hii itainua siyo tu Mkoa wa Tabora bali pia kuchangia ukuaji wa Pato la Taifa. Kwa kutamua hilo Wizara itaendelea kuhamasisha sekta binafsi kuwekeza katika sekta mbalimbali za uchumi ikiwa ni pamoja na eneo hili la Tumbaku. Jukumu la Serikali kwa sasa ni kuendelea kuandaa mazingira wezesi ili Sekta binafsi iwekeze katika viwanda vikiwemo vya kuongeza thamani malighafi zinazopatikana hapa nchini. (*Makofii*)

**MHE. MUNDE TAMBWE ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, napenda niulize swalii dogo la nyongeza.

Kwa kuwa, kwenye Mkoa wa Tabora kumekuwa na kero ya muda mrefu ya upatikanaji wa viwanda, sisi kama wakazi wa Mkoa wa Tabora, tumejitahidi sana kutafuta wawekezaji lakini kitu kinacholeta tatizo ni miundombinu.

Je, Mheshimiwa Waziri atatuambiaje kuhusu maji, barabara na umeme ili wawekezaji hao waweze kukubali kuja kuwekeza ndani ya Mkoa wa Tabora?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, nirudie tena kumpongeza sana Mheshimiwa Munde Tambwe Abdallah, kwa jitihada zake za kuwaendeleza wananchi wa Mkoa wa Tabora.

Naomba nirudie tena azma ya Serikali ya kuhakikisha kwamba Sekta Binafsi inawezeshwa na inawekewa mazingira wezesi ili kuwekeza katika viwanda nchi

nzima na Serikali inafanya kila jitihada kuhakikisha kwamba miundombinu hasa ya barabara, umeme na vinginevyo inaendelea kuwezeshwa. Kuna mfano mdogo tu na nimwambie kwamba Serikali imeanza kuhakikisha kwamba barabara inayotoka Manyoni kuelekea Tabora inajengwa kwa kiwango cha lami.

Hali kadhalika Serikali ya Chama cha Mapinduzi (CCM) imekamilisha kabisa barabara inayotoka Dodoma kwenda Singida kupitia Mkoa wa Tabora mpaka Mwanza na tuna mpango wa kuimarisha Reli ili kuhakikisha kwamba tunawezesha usafirishaji wa malighafi inayotoka Tabora kwenda Dar es Salaam.

Suala la umeme Mheshimiwa Rais alilizungumzia kwa kirefu sana ni azma ya Serikali kuhakikisha kwamba tunalitatu.

**SPIKA:** Tunaendelea na Mheshimiwa Vita Kawawa Mwenyekiti wa Bodi ya Tumbaku.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa, pia mji wa Songea una kiwanda cha kusindika Tumbaku kilichokuwa chini ya umoja wa Vyama vyta Ushirika na ambacho kilikuwa kinaajiri watu zaidi ya 3,000. Lakini kiliingia ubia ambao uliathirika baada ya mwekezaji aliyeingia ubia wa 40% kushindwa kukiendeleza kiwanda hicho.

Je, Serikali inaweza kukiweka kiwanda hicho katika mpango wa kukisaidia kufufua ili kuleta ajira na kuongeza thamani ya zao?

**SPIKA:** Sasa ni la kwako hilo au? Mheshimiwa Maghembe siyo la kwenu hilo? Naibu Waziri anasema analiweza hata hilo.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, naomba tena nimhakikishie Mheshimiwa Vita Kawawa kwamba ni azma ya Serikali na ni sera ya viwanda kuhakikisha kwamba tunapitia mikataba yote ya awali na kama tulivyozungumza hapo nyuma kwa viwanda vyote vilivyobinafsishwa hapa nchini na kuhakikisha kwamba kwa mujibu wa Sheria zilizotumika na kwa mujibu wa mikataba viwanda hivyo vinafanya kazi kama ilivyokusudiwa. Zoezi hili bado linaendelea na zoezi hili litakapokamiliika Serikali itatoa tamko hapa Bungeni kwa maana ya utekelezaji wake.

**SPIKA:** Tunaendelea na swali linalofuata Mheshimiwa Anne K. Malecela, lakini kwa niaba yake Mheshimiwa Betty Machangu.

**MHE. BETTY ELIEZER MACHANGU (K.n.y. MHE. ANNE K. MALECELA)** aliuliza:-

Bei za vyakula na bidhaa muhimu zimepanda sana kuliko uwezo wa wananchi kiuchumi, hali inayohatarisha ustawi wa Taifa.

(a) Je, serikali imeliona hilo?

(b) Je, Serikali ina mpango gani madhubuti wa kurekebisha hali hiyo ili wananchi waweze kumudu maisha yao?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Anne K. Malecela, Mbunge wa Jimbo la Same Mashariki, lenye sehemu a na b kama ifuatavyo.

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali inaomba kumhakikishia Mheshimiwa Anne Kilango Malecela kwamba inatambua kuwepo kwa ongezeko kubwa la bei za vyakula na bidhaa nyingine na huduma muhimu nchini hasa katika kipindi cha kuanzia mwishoni mwa mwaka 2010 hadi sasa. Bidhaa za vyakula zilizoguswa zaidi na ongezeko hili ni pamoja na Mahindi, Maherage, Viazi Mviringo, ikiwa ni pamoja na bidhaa muhimu za viwandani hususani Sukari, mafuta ya kupikia na vifaa vya ujenzi.

Mheshimiwa Spika, sababu za ndani za ongezeko la bei ya vyakula nchini na bidhaa muhimu ni pamoja na upatikanaji duni wa nishati, gharama kubwa za usafirishaji, miundombinu na teknolojia duni. Sababu za nje ni ongezeko la bei ya mafuta ya *Petrol* duniani, uharamia wa meli katika Ghuba ya Somalia na machafuko ya kisiasa katika baadhi ya nchi zinazozalisha mafuta kwa wingi. Aidha, ongezeko la mahitaji ya mazao ya kilimo duniani kutokana na kushuka kwa uzalishaji kulikosababishwa na janga la ukame, mafuriko sehemu mbalimbali duniani na tetemeko la ardhi hivi karibuni nchini Japan. Hivi vyote vimechangia kuwepo kwa uhaba wa chakula na hivyo kusababisha kuongezeka kwa bei ya chakula.

(b) Mheshimiwa Spika, ili kudhibiti ongezeko la bei za vyakula na bidhaa muhimu, hatua zifuatazo zimechukuliwa.

(i) Kwa bidhaa ya Sukari, Serikali imefanya majadiliano na wadau wa kuzalisha na kusambaza Sukari nchini na kukubaliana kutangaza bei elekezi kwa kuzingatia gharama za uzalishaji na usambazaji. Tangazo hilo la bei elekezi limesaidia kupunguza bei ya Sukari hapa nchini.

(ii) Serikali imetua maelekezo kwa Wakala wa Hifadhi ya Chakula (*NFRA*) kuuza kwa bei nafuu kwa wasambazaji sehemu ya Mahindi yaliyohifadhiwa katika maghala ili kuziba pengo la upungufu katika soko kwa nia ya kumpunguzia mlaji makali

ya bei. Hili limefanyika na bei imeanza kushuka katika Mikoa ya Kigoma, Lindi, Morogoro, Mtwara, shinyanga, Songea na Tabora.

(iii) Serikali inaendelea na kuongeza jitihada mbalimbali za upatikanaji wa nishati mbadala ikiwa ni pamoja na kuzalisha umeme kwa kutumia makaa ya mawe, upepo, gesi asilia, *biogas* na kuwezesha uzalishaji katika sekta ya viwanda kuwa wa bei nafuu zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudi hizo nilizozielekeza, Serikali itaendelea kuimarisha Sekta binafsi ili ishiriki kununua kwa wingi mazao, kuyasindika na kuyasambaza kwenye maeneo yenye upungufu kwa bei nafuu.

**MHE. BETTY E. MACHANGU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri. Naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Kilimanjaro ni Mkoa ulioko mpakani. Pamoja na Serikali kupunguza chakula kilichoko kwenye hifadhi ili wananchi wa Tanzania waweze kununua chakula kwa bei nafuu, lakini wafanyabiashara wanaotoka nchi za nje wamekuwa wanununa mazao haya kwa bei ya juu na hivyo kuleta mtafaruku katika bei hizo.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza bei ya mazao haya kutoka kwa wakulima ili wakulima hawa wasiwe na tamaa ya kuuza chakula nje ya nchi?

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Serikali ina mkakati gani na inasadidhidi zile Serikali za Vijiji zilizoko kwenye Mikoa iliyoko mipakani kwa ajili ya kuweza ku-*charge* ushuru kwa wafanyabiashara hawa ambao wanaenda kununua mazao kule na hasa baada ya ufunguzi wa Soko la Afrika Mashariki?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu! Hata Waziri wa Kilimo anawenza kujibu, tusitumie muda mara mbili kwa sababu kama linalekeea kwake, inakuwa vizuri.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa fursa niweze kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Betty Machangu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri sana. Mheshimiwa Spika, suala la chakula kununuliwa kwa wingi na wageni wa nchi zinazotuzunguka, kwa kweli ni fursa ya kibiashara.

Mheshimiwa Spika, jambo ambalo tunaendelea kulifanya ni kujipanga ili tuweze kufaidika zaidi na fursa hizi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunaendelea kutoa mahindi katika Hifadhi ya Taifa kujaribu tunavyoweza kuteremsha bei za chakula hasa mahindi katika miji ambayo bei za unga zimepanda sana. Kuanzia jana, tumeanza kuuza mahindi katika Hifadhi ya Taifa kwa shilingi 300/- kwa kilo moja.

Kwa hiyo, tunawahimiza wasagaji wadogo wa mahindi waendelee kununua mahindi katika Hifadhi zetu za Taifa ili kusaidia kuteremsha bei ya unga katika miji mikubwa. (*Makofi*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Tuko nje ya muda. Tunaingia Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo. Mheshimiwa Yusuf Haji Khamis, atauliza swali hilo!

Na. 20

### **Ukuzaji wa Mchezo wa Mpira wa Miguu**

#### **MHE. YUSSUF HAJI KHAMIS** aliuliza:-

Katika kukuza mchezo wa mpira wa miguu, Mheshimiwa Rais aliruhusu Chama cha Mpira wa Miguu kutafuta Kocha ambaye analipwa na Serikali:-

- (a) Je, ni nini tathmini ya jumla ya maendeleo ya soka nchini katika kipindi cha miaka mitano iliyopita?
- (b) Je, Taifa *Stars* imecheza michezo mingapi ya kirafiki ya Kimataifa na imeshinda na kufungwa mingapi?
- (c) Je, Taifa *Stars* imecheza michezo mingapi ya kutafuta ubingwa na imeshinda vikombe vingapi?

#### **NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Yussuf Haji Khamis, Mbunge wa Nungwi, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

- (a) Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha miaka mitano iliyopita, mchezo wa mpira wa miguu umeonekana kupiga hatua na kuanza kuleta matumaini mapya katika maendeleo ya mchezo huo hapa nchini. Maendeleo hayo yamekuja kutokana na sababu za msingi zifuatazo:-

· Mabadiliko na kuimarika kwa uongozi na utendaji wa vyombo vinavyosimamia mchezo huo katika ngazi ya Taifa.

· Ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya michezo hususan viwanja vya mpira wa miguu.

· Ujio wa walimu wa kigeni wa mpira wa miguu kwa Timu za Taifa (wanaume na wanawake) na vijana (wanaume) ambapo Timu ya Taifa (*Taifa Stars*) ilipanda kiwango cha *FIFA* kutoka nafasi ya 165 mwaka 2005 hadi nafasi ya 89 mwaka 2008.

· Kushiriki kwa timu hizo katika mashindano mbalimbali na michezo ya kirafiki ya Kimataifa. Mfano ni michezo ya mashindano ya Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ligi za Ndani (*CHAN*), Fainali za Kombe la Afrika kwa Timu ya Wanawake na michezo ya kirafiki ya Kimataifa.

· Mapenzi makubwa ya wananchi kwa Timu ya Taifa pamoja na motisha kwa wachezaji, jambo ambalo limechangia kuwapa hamasa na hivyo kufanya vizuri katika michezo mbalimbali.

· Kupata ufadhili wa uhakika na michango kutoka kwa wadau mbalimbali kwa ajili ya maandalizi ya Timu ya Taifa.

(b) Mheshimiwa Spika, Timu ya Taifa (*Taifa Stars*) imecheza michezo 79 ya kirafiki na Kimataifa. Kati ya hiyo, imeshinda 32, kushindwa 25 na kutoka sare michezo 22.

(c) Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha miaka mitano iliyopita, Timu ya Taifa (*Taifa Stars*) imeshiriki katika mashindano mbalimbali kama ifuatavyo:-

· Mwaka 2006 hadi 2010 imeshiriki katika mashindano ya Kombe la *Challenge* ambapo mwaka 2010 ilitwaa ubingwa wa Kombe hilo.

· Mwaka 2008 na 2010 imeshikiri mashindano ya awali ya Kombe la Mataifa ya Afrika.

· Mwaka 2008 hadi 2010 ilishiriki mashindano ya Kombe la *CHAN*, ambapo mwaka 2008 ilifanikiwa kushiriki kwenye fainali za mashindano hayo yaliyofanyika nchini *Ivory Coast*.

· Mwaka 2010 ilishiriki mashindano ya Kombe Jipyala Bonde la Mto Nile yaliyofanyika huko *Egypt*. (*Makofî*)

**MHE. YUSSUF HAJI KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Timu yetu ya Taifa ya Vijana Chini ya Umri wa Miaka 23 imekuwa ikifanya vizuri katika mashindano yake ya Kimataifa na kwa kumbukumbu nilizonazo mimi, hivi karibuni imeishinda Timu ya Vijana wa Cameroon kwa mikwaju ya penati.

Kama hiyo haitoshi, siku ya tarehe 5 Juni, 2011, siku ya Jumapili, Mwezi huu wa Juni, timu yetu imeifunga timu ngumu ya vijana ya Nigeria kwa bao moja kwa bila. Kutokana na maendeleo mazuri ya timu hii.

Je, Serikali ina mikakati gani ya kuiendeleza na kuitunza timu hii ya vijana ili baadaye washirikiane na Timu ya Taifa katika michezo ya Kimataifa? Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, kwanza, nataka nichukue nafasi hii na mimi pia niwapongeze hiyo timu ya Vijana Chini ya Miaka 23. Ni kwamba Serikali imejipanga vizuri katika kuhakikisha tunawatafutia wafadhili mbalimbali, kuhakikisha kwamba wanapata nafasi ya kwenda kufanya mazoezi nchi za nje ili kusudi waweze kupata *practice* ya kuweza kushinda watakapoendelea kushindana tena. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini pia tumejipanga kuhakikisha kwamba wana Kocha mpya wa kuweza kuhakikisha anawasaidia kuweza kucheza mchezo wao vizuri. Kwa kifupi ni kwamba Serikali itawabeba kila wakati tutakapopata nafasi ya kuweza kufanya hivyo.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, samahani muda umekwisha kabisa kabisa. Kwa hiyo, *next time*.

Waheshimiwa Wabunge, wengine wanaandika *vi-note* kutoka upande huu, wanasema: “Mheshimiwa Spika una kengeza hutuoni” Na mwingine anaandika: “Mheshimiwa Spika una kengeza hutuoni”. Mimi nawaona wote. Kwa hiyo, mridhike kwamba nawaona wote ndiyo maana huyu akilalamika na huyu analalamika. Kwa hiyo, mnaonwa wote, isipokuwa tuko wengi, muda hautoshi.

Waheshimiwa Wabunge, mimi nina wageni leo amba ni Wajumbe wa Baraza la vyama vya Siasa wakiongozwa na Dkt. Emmanuel Makaidi – Mwenyekiti. Mwenyekiti yupo? Asimame kama yupo! Ndiye Mwenyekiti ambaye anatoka chama cha *NLD* na ameongozana na Rashid Abdallah. Wako wawili wawili. Wajumbe kutoka *TLP*, Hamad Mkadamu Rajab na Richard Lyimo. Kutoka chama cha *UPDP* yuko Felix Makua na Abdallah Mohamed. Chama cha *AFP* yuko Said Soud Said na Rashid Rai. Chama cha *UMD* yuko Salim Alli na Mohamed Omar. Chama cha *DP* yupo Haji Alli Nihu na G. C. Mtikila. Nyie mnajua Mtikila mmoja, yupo na mama pia. Chama cha *APPT-Maendeleo* yuko Khamis S. Khamis na Peter Mziray (Huyu alishagombea Urais). Chama cha Jahazi Asilia yupo Said Komba Said na Amour Rajab. Chama cha *CUF* yuko Julius Mtatiro (kijana machachari) na Ismael Jusa. Chama cha *NCCR-Magezi* yuko Faustine Sungura na

Haji Ambari. Chama cha CHAUSTA yupo Absalom Mashoto na Amir Haji Makame. Chama cha TADEA yupo John Lipha Chipaka (Maarufu) na Juma Alli Khatib. Halafu, chama cha *UDP* yupo John Nkolo na Juma Khamis Faki. Chama cha *NRA* yuko Rashid Mtuta na Simai Abdallah. Chama cha CCM yupo Pius Msekwa na Salehe Ramadhan Feroudh.

Chama cha *SAU* yuko Paul Henry na Alli Bakari Kaniki. Chama cha Demokrasia Makini yuko Aziz Mohamed Kaniki na Dominique Lyamtai na Chama cha CHADEMA yupo V. P. Kimesera.

Waheshimiwa Wabunge, ahsante sana. Hawa ni wageni wangu, nimewaalika kwa ajili ya kusikiliza Hotuba ya Hali ya Uchumi na jioni watakuwepo kwenye Hotuba ya Bajeti. Hawa ni kutoka vyama ambavyo vimeandikishwa kihalali kwa mujibu wa Katiba yetu. Tunapenda kuwashirikisha katika mambo ya uongozi wetu wa nchi. Karibuni sana. Nadhani mtapewa huduma mnazostahili. Tutaonana na Mwenyekiti. Katibu, tunaendelea! (*Makofi*)

## **HOJA ZA SERIKALI**

### **Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2011 na Mwelekeo wa Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka 2011/2012**

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu sasa likae kama Kamati ili liweze kupokea na kujadili Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa katika kipindi cha mwaka 2010 na malengo katika kipindi cha Muda wa Kati (2011/2012 – 2015/2016). Pamoja na hotuba hii, nawasilisha Kitabu cha Hali ya Uchumi wa Taifa katika mwaka 2010 na Kitabu cha Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Spika, kikao hiki cha Bunge la Bajeti ni cha kwanza baada ya Uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani uliofanyika tarehe 31 Oktoba, 2010. Katika uchaguzi huo, Chama cha Mapinduzi (CCM) kilishinda na kupata ridhaa ya wananchi ya kuongoza nchi kwa kipindi kingine cha miaka mitano. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuchaguliwa tena kuongoza kwa muhula wa pili wa Serikali ya Awamu ya Nne. Aidha, ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa imani kubwa aliyonayo kwangu kwa kunichagua kwa mara nyingine tena kuongoza Wizara kubwa na nyeti. Ninamwahidi kuwa sitamwangusha. Ninampongeza Mheshimiwa Dkt. Mohammed Gharib Billal kwa kuchaguliwa kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Vile vile, nampongeza Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge na kuteuliwa tena na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuitishwa na Waheshimiwa Wabunge kwa kishindo kuwa Waziri Mkuu kwa muhula wa pili wa Serikali ya Awamu ya Nne. (*Makofi*)

Napenda kukupongeza wewe binafsi kwa kuchaguliwa na hivyo kuwa mwanamke wa kwanza Tanzania kuwa Spika wa Bunge letu tukufu. Aidha, nampongeza Naibu wako Mheshimiwa Job Ndugai, kwa kuchaguliwa kushika wadhifa huo wa juu katika Bunge kwa kipindi cha Muhula wa Pili wa Serikali ya Awamu ya Nne. Nawapongeza pia Mawaziri wenzangu wote pamoja na Naibu Mawaziri wote kwa kuteuliwa kwao na Mheshimiwa Rais. Aidha, napenda niwapongeze Wabunge wote kwa kuchaguliwa na kuteuliwa kwao kuingia katika Bunge hili Tukufu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Abdallah Omari Kigoda, Mbunge wa Handeni, kwa kuchaguliwa tena kuiongoza Kamati ya Fedha na Uchumi katika Bunge lako Tukufu. Aidha, napenda kutoa shukurani za dhati kwa Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi, kwa kutupatia ushauri wa kina wakati wa kuandaa taarifa hii. Mchango wa Kamati hii siku zote umekuwa na umuhimu wa pekee katika kuboresha taarifa ya Hali ya Uchumi na mapendekezo ya Mpango wa Muda wa Kati. Napenda kuchukua nafasi hii pia kumshukuru Katibu Mtendaji wa Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango, Dkt. Philip Mpango, kwa ushirikiano wake katika kufanikisha maandalizi ya taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, kabla sijatoa maelezo ya mapitio ya Hali ya Uchumi kwa mwaka 2010, kwanza nibainishe vipaumbele vya mwaka 2011/2012 ambavyo Serikali itavipa umuhimu katika bajeti ijayo. Vipaumbele hivi vinatokana na changamoto zinazowakabili wananchi katika kukabiliana na hali ngumu ya maisha kwa hivi sasa na umuhimu wa kujenga uchumi imara na wenye ushindani.

Mheshimiwa Spika, niseme kwamba Mheshimiwa Rais jana alinisaidia katika mambo mengi ambayo nitayazungumza, lakini kwa sababu ni lazima nizungumze ni lazima niyazungumze yote niliyoyaandika. Vipaumbele hivyo ni kama ifuatavyo:-

(i) Nishati ya umeme; Kuongeza uzalishaji na upatikanaji wa uhakika wa umeme ili kuziwezesha shughuli za kiuchumi na maendeleo ya jamii kufanyika kwa wakati wote;

(ii) Usalama wa chakula; Kuongeza upatikanaji wa chakula kwa kuhimiza kilimo, hasa cha umwagiliaji na kuimarisha hifadhi ya chakula ili kujikinga na tatizo la uhaba wa chakula nchini;

(iii) Miundombinu; Kuimarisha miundombinu ya maji, reli, bandari na barabara pamoja na kupunguza msongamano wa magari katika jiji la Dar es Salaam;

(iv) Ukosefu wa ajira; Kuongeza fursa za ajira na kuwanufaisha wananchi walio wengi hasa vijana ambao ndio kundi kubwa katika soko la ajira la Tanzania hivi sasa. Aidha, Wizara, Idara na Taasisi za Serikali zinaelekezwa kuzingatia suala la kuongeza ajira katika maeneo yao; na

(v) Mfumuko wa bei; Mfumuko wa bei umesababishwa na kuongezeka kwa wastani wa bei za chakula, bei za mafuta, umeme na gharama za uzalishaji na

usafirishaji. Hatua zitachukuliwa kudhibiti ongezeko la bei za mafuta, bei za chakula na kuongeza uzalishaji wa umeme.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, sasa naomba nianze kutoa muhtasari wa mapitio ya Hali ya Uchumi na Maendeleo ya Jamii kwa mwaka 2010 ikiwa ni mapitio ya kwanza baada ya Uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani wa Oktoba 2010. Aidha, ikumbukwe kuwa taarifa hii ni ya kipindi cha kuanzia Januari hadi Desemba 2010 na sehemu chache zimegusia robo ya kwanza ya mwaka 2011.

Mheshimiwa Spika, taarifa hii inatokana na uchambuzi wa mwenendo wa viashiria muhimu katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii, na unyambuaji wa masuala muhimu yaliyojitekeza nchini, kikanda na duniani katika mwaka 2009/10 hususan, suala la ukame uliojitekeza nchini mwishoni mwa mwaka 2010 na athari zake kwa sekta mbalimbali za kiuchumi kama vile kilimo, nishati, uzalishaji viwandani pamoja na kupanda kwa kasi bei za mafuta katika soko la dunia.

Mheshimiwa Spika, Mapitio ya mwenendo wa uchumi duniani katika kipindi cha mwaka 2010; mwaka 2010, uchumi wa dunia na wa Tanzania kwa ujumla ulianza kuimariika baada ya kupita katika kipindi cha m dororo wa uchumi duniani. Kuimariika kwa uchumi wa dunia kulichochea kuongezeka kwa mahitaji ya mauzo nje, uwekezaji wa moja kwa moja na kuongezeka kwa mapato yatokanayo na utalii.

Mheshimiwa Spika, Hali ya Uchumi Duniani; mwaka 2010 biashara duniani ilimariika ikilinganishwa na miaka iliyotangulia kutokana na kuongezeka kwa mahitaji ya bidhaa katika Nchi Zilizoendelea na Zinazoendelea. Aidha, Pato la dunia liliimariika baada ya kuathiriwa na matokeo ya kuyumba kwa uchumi wa dunia. Mwaka 2010, kasi ya ukuaji wa uchumi duniani iliongezeka hadi wastani wa asilimia 5.0 ikilinganishwa na ukuaji hasi wa asilimia 0.5 mwaka 2009. Kuimariika huko kwa uchumi ni matokeo ya jitihada zilizochukuliwa na Nchi Zilizoendelea za kunusuru uchumi zikiwemo zile za kibajeti na kifedha.

Mheshimiwa Spika, Pato la Nchi Zilizoendelea lilikua kwa asilimia 3.0 mwaka 2010 ikilinganishwa na ukuaji hasi wa asilimia 3.4 mwaka 2009. Kwa upande wa Nchi Zinazoendelea na Nchi za Asia zinazoinukia kiviwanda (China na India), viwango vyaa ukuaji wa Pato viliongezeka hadi wastani wa asilimia 7.3 na 9.5 mwaka 2010 ikilinganishwa na asilimia 2.7 na 7.2 mwaka 2009 kwa mtiririko huo. Hii ilichangiwa na kuongezeka kwa uwekezaji na uuzaaji bidhaa nje, kupanda kwa bei za bidhaa na uvutiaji wa mitaji toka nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, Hali ya Uchumi wa Bara la Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara; kiwango cha ukuaji wa Pato la Bara la Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara kiliongezeka kwa wastani wa asilimia 5.0 mwaka 2010 ikilinganishwa na asilimia 2.8 mwaka 2009. Ongezeko hilo lilitokana na kuimariika kwa bei na mahitaji ya bidhaa za kilimo katika nchi zilizoendelea. Aidha, ukuaji huu wa uchumi kwa nchi za Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara ultokana na ukuaji mkubwa kwa nchi zinazouza mafuta

nje ambapo kiwango cha ukuaji kilikuwa wastani wa asilimia 6.5 mwaka 2010 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 4.8 mwaka 2009.

Mheshimiwa Spika, mwenendo wa viashiria vya uchumi jumla nchini katika kipindi cha mwaka 2010, Pato la Taifa, ukuaji halisi wa Pato la Taifa ulikuwa asilimia 7.0 mwaka 2010, sawa na ilivyokadiriwa ikilinganishwa na asilimia 6.0 mwaka 2009. Shughuli za kiuchumi zilizochangia ukuaji huu ni pamoja na kilimo na ufugaji; uzalishaji viwandani; biashara na matengenezo ya zana na mitambo; na usafirishaji na mawasiliano. Ukuaji wa viwango vya juu ulijionesha katika shughuli ndogo za kiuchumi za: mawasiliano (asilimia 22.1); ujenzi (asilimia 10.2); umeme na gesi (asilimia 10.2); fedha (asilimia 10.1); na uzalishaji viwandani (asilimia 7.9).

Mheshimiwa Spika, mwaka 2010, Pato la Taifa lilikuwa shilingi 32,293,479 milioni kwa bei za soko au shilingi 16,828,563 milioni kwa bei za mwaka 2001. Hali kadhalika, kwa mujibu wa kiwango cha ukuaji wa watu cha asilimia 2.9, idadi ya watu Tanzania Bara ilikadiriwa kuwa watu milioni 41.9. Hivyo, pato la wastani la kila mtu lilikuwa shilingi 770,464.3 mwaka 2010 ikilinganishwa na shilingi 693,185 mwaka 2009, sawa na ongezeko la asilimia 11.1.

Mheshimiwa Spika, Kasi ya Upandaji Bei; Ofisi ya Taifa ya Takwimu ilibadilisha mwaka wa kizio wa Fahirisi za Bei za Taifa kutoka mwaka 2001 kuwa mwaka 2007 kwa kutumia matokeo ya Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya Binafsi wa mwaka 2007. Mabadiliko haya yalifanywa kwa kutumia makundi yaliyokubalika Kimataifa ya Mchanganuo wa Matumizi Binafsi “*Classification of Individual Consumption by Purpose (COICOP)*” na maeneo ambayo mara nyingi jamii hununua bidhaa au hupata huduma mbalimbali (*Outlets*). Mfumo huu mpya wa ukokotoaji wa fahirisi za bei unatumia wastani wa kijiometria (*geometric mean*) badala ya wastani wa kawaida (*arithmetic mean*) katika kutengeneza fahirisi za bei katika ngazi za mwanzo kama inavyokubalika kimataifa kwa ulinganisho. Mizania mpya zinajumuisha matumizi ya kaya zote binafsi kutoka mijini na vijijini wakati mizania iliyokuwa inatumika zamani ilijumuisha kaya binafsi za maeneo ya mijini tu.

Mheshimiwa Spika, Mfumo huu wa kutumia wastani wa kijiometria ulianza kutumika Oktoba 2009, kwa kipindi cha miezi 12 ulitoa mfumuko wa bei wa asilimia 4.2 kwa mwezi Oktoba 2010. Hii ilikuwa ni badiliko la asilimia 0.3 ikilinganishwa na mfumuko wa bei uliotumia wastani wa kawaida wa mwezi Septemba 2010 ambao ulikuwa asilimia 4.5.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mfumuko wa bei kuendelea kuwa tarakimu moja, umekuwa na mwelekeo wa kupanda, hususan, katika robo ya kwanza ya mwaka 2011. Mfumuko wa bei uliongezeka kutoka asilimia 5.6 kwa kipindi kilichoishia Desemba 2010 hadi asilimia 6.4 Januari 2011 na kuendelea kupanda hadi asilimia 8.6 mwezi Aprili 2011. Kasi hiyo ya ongezeko la bei ilitokana hasa na kupanda kwa fahirisi za bei za nishati, maji na makazi; fahirisi za bei za usafirishaji; na fahirisi za bei za chakula na vinywaji visivyokuwa na kilevi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Ukuzaaji rasilimali; ukuzaaji rasilimali kwa bei za miaka husika uliongezeka hadi kufikia shilingi 10,342,536 milioni mwaka 2010 kutoka shilingi 8,173,221 milioni mwaka 2009, sawa na ongezeko la asilimia 26.5. Hii ilitokana na kuongezeka kwa uwekezaji katika ujenzi wa majengo na shughuli nyingine za ukuzaaji rasilimali katika ujenzi ikijumuisha uendelezaji ardhi, barabara na madaraja. Uwiano wa ukuzaaji rasilimali kwa Pato la Taifa kwa bei za miaka husika ulikuwa asilimia 32.0 mwaka 2010 ikilinganishwa na asilimia 29.0 mwaka 2009. Hivyo, kadiri uchumi unavyokua, ndivyo na ukuzaaji rasilimali unavyoongezeka.

Mheshimiwa Spika, Ujazi wa Fedha na Karadha; katika kipindi cha mwaka 2010/2011, sera ya fedha ililenga kuwa na kiwango cha ongezeko la ukuzaaji wa fedha kinachoenda sambamba na mahitaji halisi ya uchumi, kasi ya upandaji bei, ongezeko la mikopo ya ndani lisiloathiri uzalishaji mali na ambalo linalingana na malengo ya ujazi wa fedha, na kuwa na akiba ya fedha za kigeni itakayoweza kukidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa kipindi kisichopungua miezi mitano.

Mheshimiwa Spika, hadi Desemba 2010, ujazi wa fedha kwa tafsiri pana (M2) ulikua kwa asilimia 21.8 kiwango ambacho kilikuwa chini ya kiwango cha ukuaji cha asilimia 26.3 kwa mwaka ulioishia Juni, 2010. Hata hivyo, kiwango hicho kilikuwa juu kidogo ikilinganishwa na makadirio ya kiwango cha asilimia 20.8 hadi Desemba 2010. (*Makofi*)

Katika kipindi hicho, ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) ulikua kwa asilimia 25.4 ikilinganishwa na asilimia 25.1 kwa mwaka ulioishia Juni, 2010, na hali kadhalika ikilinganishwa na makadirio ya ukuaji wa asilimia 23.5 Desemba 2010. Kasi ya ongezeko la ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi ilitokana na kasi ya ongezeko la amana katika fedha za kigeni, ambapo ziliongezeka kwa asilimia 23.3 kutoka dola za kimarekani milioni 1,657.3 mwezi Desemba 2009 hadi dola milioni 2,043.6 mwezi Desemba 2010, pamoja na kuimarika kwa dola ya Kimarekani dhidi ya sarafu nyingine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kiwango cha ukuaji wa mikopo inayotolewa kwa sekta isiyo ya Serikali kiliendelea kuongezeka na kufikia asilimia 20.0 Desemba 2010 kutoka asilimia 16.3 Juni 2010. Hii inatokana na kuanza kujengeka kwa imani ya mabenki dhidi ya sekta binafsi kufuatia kuanza kuimarika kwa hali ya uchumi wa dunia baada ya kupitia katika kipindi cha msukosuko wa Masoko ya Fedha na Mitaji. Sehemu kubwa ya mikopo hii ilielekezwa katika sekta za: biashara asilimia 17.6; uzalishaji bidhaa viwandani asilimia 13.6; uchukuzi na mawasiliano asilimia 9.0; kilimo asilimia 12.3; na mikopo kwa shughuli binafsi asilimia 23.1.

Mheshimiwa Spika, Mwenendo wa Viwango vya Riba; wastani wa jumla wa viwango vya riba za mikopo katika benki za biashara ulipungua hadi asilimia 13.45 Desemba 2010 kutoka asilimia 14.38 Desemba 2009. Wastani wa riba za kukopa kwa muda mfupi (hadi mwaka mmoja) ulipungua kutoka asilimia 13.96 Desemba 2009 hadi asilimia 12.40 Desemba 2010.

Aidha, wastani wa jumla wa riba za amana za akiba za muda maalum ulipungua kutoka asilimia 6.36 Desemba 2009 hadi asilimia 5.11 Desemba 2010. Vile vile, wastani wa riba za amana za akiba za muda maalum (miezi 12) ulipungua na kufikia asilimia 7.09 Desemba 2010 kutoka asilimia 8.99 Desemba 2009. Aidha, wastani wa riba za amana za akiba ulipungua na kufikia asilimia 2.41 Desemba 2010 kutoka asilimia 2.83 Desemba 2009. Kutokana na mwelekeo huo wa riba, tofauti baina ya viwango vya riba za amana na mikopo (mwaka mmoja) iliongezeka kutoka asilimia 4.97 Desemba 2009 hadi asilimia 5.31 Desemba 2010.

Mheshimiwa Spika, tofauti kati ya viwango vya riba vinavyotozwa kwenye mikopo na vile vinavyotolewa kwenye amana kama faida imeendelea kuwa juu, licha ya kuongezeka kwa ushindani katika sekta ya kibenki. Hii imechangiwa kwa kiasi kikubwa na kukosekana kwa taarifa sahihi za wakopaji (*credit reference data bank*) na kutokuwepo kwa taasisi ya utoaji wa taarifa sahihi za waombaji mikopo (*Credit Reference Bureau*) nchini. Aidha, ukosefu wa vitambulisho vya kitaifa na gharama kubwa za kufanya biashara kutokana na miundombinu hafifu, umechangia kuongeza viwango vya riba vinavyotozwa kwenye mikopo.

Mheshimiwa Spika, Thamani ya Shilingi ya Tanzania; thamani ya Shilingi ya Tanzania kwa mwaka 2010 ilishuka kwa asilimia 8.5 hadi wastani wa shilingi 1,432.3 kwa dola moja ya Kimarekani kutoka wastani wa shilingi 1,320.0 mwaka 2009. Hata hivyo, thamani ya shilingi ilishuka kwa kiwango kidogo mwaka 2010 ikilinganishwa na asilimia 10.4 mwaka 2009.

Kushuka kwa thamani ya shilingi kulitokana na kuongezeka kwa mahitaji ya dola nchini pamoja na kuimarika kwa dola ya Kimarekani dhidi ya sarafu za mataifa mengine. Aidha, bei ya dola moja ya Kimarekani mwishoni mwa Desemba 2010 ilikuwa na thamani ya shilingi 1,453.5 ikilinganishwa na shilingi 1,313.3 mwishoni mwa Desemba 2009. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Nje; mwenendo wa biashara ya bidhaa na huduma nje kwa mwaka 2010 uliendelea vizuri na ulikuwa wa kuridhisha ikilinganishwa na mwaka 2009. Thamani ya mauzo ya bidhaa na huduma nje iliongezeka kwa asilimia 24.1 hadi Dola za Kimarekani milioni 6,388.2 kutoka dola milioni 5,149.5 mwaka 2009. Ongezeko hilo lilitokana na kuongezeka kwa thamani ya bidhaa zisizo asilia hususan, madini ya dhahabu na kuongezeka kwa mapato yatokanayo na huduma za usafirishaji na utalii.

Vile vile, thamani ya bidhaa na huduma zilizoagizwa toka nje (*f.o.b*) iliongezeka hadi dola za Kimarekani milioni 8,974.7 kutoka dola milioni 7,543.2 mwaka 2009, sawa na ongezeko la asilimia 19.0. Hii ilitokana na kupanda kwa bei za bidhaa katika soko la dunia na kupanda kwa gharama za malipo ya huduma za usafirishaji.

Mheshimiwa Spika, Akiba ya Fedha za Kigeni; akiba ya fedha za kigeni imeendelea kuongezeka hadi kufikia Dola za Kimarekani milioni 3,948.0 Desemba 2010,

kutoka Dola milioni 3,552.5 Desemba 2009, sawa na ongezeko la asilimia 11.1. Kiasi hiki cha akiba ya fedha za kigeni kwa mwaka 2010 kinakidhi uagizaji wa bidhaa na huduma nje kwa muda wa miezi 6.3.

Mheshimiwa Spika, Maboresho ya Sekta ya Fedha; Serikali ilianza kutekeleza Awamu ya Pili ya Mageuzi katika Sekta ya fedha mwaka 2006/2007. Mageuzi haya ni pamoja na kuimarisha sekta ya mabenki kwa lengo la kuimarisha mazingira na ushindani katika utoaji wa huduma, kuimarisha masoko ya fedha, mageuzi katika usimamizi wa uwekezaji rasilimali kwa Mifuko ya Hifadhi za Jamii, kuboresha utoaji wa mikopo ya muda mrefu ikiwa ni pamoja na mikopo kwa ajili ya kilimo, mikopo ya makazi na Mikopo ya karadha na kuboresha taarifa za wakopaji kwa kuanzisha chombo cha kutoa taarifa hizo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, hadi sasa mafanikio yamekwisha patikana ikiwa ni pamoja na sekta ya fedha nchini kuendelea kukua kwa kasi ya kuridhisha. Kulingana na vigezo na viashiria vya uimara wa sekta ya fedha, mabenki yote nchini yanakidhi viwango vya mtaji unaoweza kuhimili madai (*capital adequacy ratio*); yana ukwasi wa kutosha kukidhi malipo kwa wateja (*liquidity ratio*); na ukuaji wa kuridhisha wa mikopo kwa sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, taasisi za kifedha zinaendelea kufungua matawi kwenye maeneo nje ya miji mikubwa ili kuweza kupata wateja na pia kwa sababu ya ushindani mkubwa uliopo sasa maeneo ya mjini. Taasisi nyingine kama vyama vya kuweka na kukopa (*SACCOS*) na vingine na Benki za wananchi zimeweza kujipenyeza hata kwenye miji midogo na vijijini. Huduma asilia za kibenki kwa ujumla zimeongezeka sambamba na ongezeko kubwa kwenye huduma zinazotolewa kwa njia za teknolojia ya mawasiliano ya simu na mashine za kuweka na kutoa fedha - ATMs. Changamoto kubwa kwa sasa ni juu ya suala la usimamizi kwani makampuni ya simu yanayotoa huduma hizi yanasisi na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania -TCRA, ambayo haihusiki na masuala ya kifedha bali ya masuala ya mawasiliano. Hata hivyo, Benki Kuu inakamilisha mazungumzo na TCRA kuiwezesha kushiriki katika kusimamia masuala ya huduma za kifedha zinazofanywa na makampuni ya simu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, takwimu zinaonesha kuwa hadi mwishoni mwa mwaka 2010 huduma na taasisi za fedha zilikuwa kama ifuatavyo: Idadi ya benki na taasisi za fedha - 43; Akaanti za benki - 4,241,610; Matawi ya benki na taasisi za fedha - 475; Mashine za kutolea fedha - ATMs, - 969; Mtandao wa malipo (*Switches*) - 2; Vituo vya mauzo (POS) - 1,427. Aidha, baadhi ya taasisi za fedha hutoa huduma za kibenki bila matawi. Idadi ya benki zinazotoa huduma za kibenki kuititia simu za mkononi - 5; Idadi ya benki zinazotoa huduma za kibenki kuititia intaneti - 5; Watumiaji wa huduma za kibenki za malipo kwa njia ya simu za mkononi - 10,372,331. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, elimu ya masuala ya kifedha ni muhimu katika kusaidia kupanua wigo wa huduma za kibenki na Serikali imefanya juhudzi za kuweka mazingira bora ya kuongeza elimu hii ambapo mwongozo wa kitaifa umeshaandaliwa. Aidha, maandalizi ya utafiti wa msingi juu ya uelewa wa umma kuhusu maana ya uwezo kifedha

yanaendelea. Matokeo ya utafiti huu yatarahisisha utoaji wa elimu ya kifedha kwa umma. Vilevile, mchakato wa kuandaa mfumo wa kumlinda mtumiaji wa huduma za kifedha umeshaanza. Mfumo huo utaongeza upatikanaji wa huduma za kifedha kwa kuwawezesa wananchi kuwa na taarifa sahihi na za uwazi kuhusu huduma hizo.

Mheshimiwa Spika, Mkakati wa Huduma za Kifedha Vijijini, umeandaliwa. Lengo la Mkakati huo ni kuboresha upatikanaji wa huduma za kifedha kwa mtu mmoja mmoja, kaya na wajasiriamali wadogo wadogo na wa kati ili kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi na kupunguza umasikini kwa maeneo ya vijijini. Mkakati huo upo katika mchakato wa kuridhiwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeanzisha kampuni itakayohusika kutoa mikopo ya nyumba kwa kupitia katika benki za biashara, na hivyo wananchi kuweza kukopa kupitia katika benki hizo. Kampuni hizo inajulikana kwa jina la “*Tanzania Mortgage Refinance Company*” (*TMRC*) na iko chini ya usimamizi wa Benki Kuu. Aidha, mchakato kwa ajili ya kuanzisha mfuko wa kutoa mikopo midogo na ya muda mrefu kwa ajili ya ujenzi wa nyumba kwa wananchi wa kipato cha chini umeanza.

Mheshimiwa Spika, mchakato wa kuanzisha Benki ya Maendeleo ya Kilimo uko kwenye hatua za mwisho. Lengo la uanzishwaji wa benki hii ni kuwasaidia wananchi kupata mikopo kwa riba nafuu na ya muda mrefu ili waweze kujikwamua kiuchumi. Aidha, wakati mchakato wa uanzishwaji wa Benki hiyo unaendelea, Serikali kwa muda mfupi, imefungua dirisha la kutoa mikopo ya kilimo katika Benki ya Rasilimali Tanzania. Serikali pia imeibadili Benki ya Rasilimali na kuwa taasisi ya kutoa mikopo ya maendeleo ya muda mrefu. Aidha, Serikali inaandaa mfumo wa kisera, sheria, kanuni na taratibu za upatikanaji na utoaji wa mikopo ya muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, mfumo wa malipo nchini umeboreshwa na kuleta ufanisi katika kutekeleza sera za kiuchumi na fedha. Mfumo wa malipo baina ya mabenki nchini ulioanza kutumika rasmi mwaka 2004 umeendelea kuboreshwa kwa kuhakikisha kwamba unatumika kurahisisha ukusanyaji wa mapato ya Serikali na baadhi ya malipo yanayofanywa na Serikali. Hali kadhalika, mfumo wa malipo ya hundi umeendelea kuboreshwa kwa kupunguza malipo kwa njia ya hundi.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2010, Kanuni zitakazotumika katika masuala ya taarifa za mikopo zilichapishwa kupitia Tangazo la Serikali namba 177 na 178 la mwaka 2010 na kuanza kutumika rasmi mwezi Oktoba 2010. Hali kadhalika, Serikali ilihitimisha mchakato wa uanzishwaji wa Mamlaka ya Kusimamia Mifuko ya Hifadhi ya Jamii (*Social Security Regulatory Authority - SSRA*) ambayo jukumu lake ni kukuza ufanisi na kuongeza ushindani katika mifuko ya pensheni na hivyo kuchangia zaidi kwenye ustawi wa uchumi. Aidha, Serikali inaendelea na mchakato wa kuboresha taratibu za mafao ya mifuko yote ya hifadhi ya jamii ili ilingane na iwe endelevu.

Mheshimiwa Spika, licha ya mafanikio yaliyopatikana chini ya programu ya uboreshaji wa sekta ya fedha, zipo changamoto ambazo Serikali itaendelea kutafuta ufumbuzi wake. Changamoto kubwa ni viwango vikubwa vya riba kwenye mikopo

ambavyo vimeendelea kutozwa na benki za biashara ikilinganishwa na riba ndogo inayolipwa kwa amana. Serikali inaendelea na mkakati wa kuimarisha soko la dhamana za Serikali ili kufikia viwango halisi vya riba vinavyotokana na nguvu za soko na visivyobadilika mara kwa mara. Hali kadhalika, Serikali inaendelea na mikakati yenye lengo la kuimarisha miundombinu katika sekta ya fedha pamoja na kuimarisha mazingira ya ushindani katika sekta hiyo.

Bajeti ya Serikali, mapato ya ndani yaliongezeka kwa asilimia 8.2 mwaka 2009/2010 kufikia shilingi bilioni 4,661.5 kutoka shilingi bilioni 4,293.1 mwaka 2008/2009. Hata hivyo, kiasi hicho kilichokusanywa ni pungufu ya makadirio kwa asilimia 8.8 kwa mwaka 2009/2010. Wastani wa makusanyo kwa mwezi uliongezeka kutoka wastani wa shilingi bilioni 357.8 kwa mwezi mwaka 2008/09 hadi shilingi bilioni 388.5 kwa mwezi mwaka 2009/2010 na shilingi bilioni 473 kwa mwezi kwa miezi tisa ya mwaka 2010/2011.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai 2010 hadi Machi 2011, mapato ya ndani yakijumuisha mapato ya Halmashauri yalifikia shilingi bilioni 4,256.3, ikiwa ni asilimia 31 chini ya lengo la bajeti ya mwaka 2010/11 ambalo ni shilingi bilioni 6,176.2. Mapato yaliyopatikana katika kipindi hicho cha Julai 2010 hadi Machi 2011 yalikuwa asilimia 21 zaidi ya mapato yaliyokusanywa katika kipindi kama hicho mwaka 2009/2010. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, misaada na mikopo, misaada ya nje katika mwaka 2009/2010 ilikuwa shilingi bilioni 1,405.3 ikilinganishwa na matarajio ya shilingi bilioni 2,090.9 katika kipindi hicho. Aidha, mikopo ya nje katika mwaka 2009/2010 ilikuwa shilingi bilioni 1,379.6 na mikopo ya ndani ilikuwa shilingi bilioni 568.5 ikilinganishwa na matarajio ya shilingi bilioni 1,037.1 na shilingi bilioni 500.2 kwa mtiririko huo. Katika kipindi cha Julai 2010 hadi Machi 2011, jumla ya misaada na mikopo ya kibajeti ilikuwa shilingi bilioni 845.7, sawa na asilimia 3 zaidi ya makadirio ya bajeti. Misaada na mikopo kwa ajili ya miradi ya maendeleo ilifikia shilingi bilioni 1,427.6, sawa na asilimia 58 ya Bajeti.

Mheshimiwa Spika, Matumizi, matumizi ya Serikali yalifikia shilingi bilioni 8,173.7 mwaka 2009/2010, sawa na asilimia 92.0 ya makadirio. Kati ya hizo, matumizi ya kawaida yalikuwa shilingi bilioni 5,562.4 na ya maendeleo yalikuwa shilingi bilioni 2,611.3. Matumizi ya maendeleo yalikuwa asilimia 8.0 chini ya lengo hasa kutozwa na kuchelewa kwa utekelezaji wa miradi kulikosababishwa na baadhi ya Wizara, Idara, Mikoa na Halmashauri kuchelewa kukamilisha taratibu za ununuzi na kutoa taarifa za matumizi ya fedha za miradi. Matumizi ya kawaida pia yalikuwa asilimia 8.0 chini ya malengo.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai 2010 hadi Machi 2011, matumizi ya Serikali yalifikia shilingi bilioni 7,169.3, ikiwa ni asilimia 67 ya makisio ya matumizi kwa mwaka mzima wa 2010/2011. Katika kipindi hicho cha robo tatu mwaka, matumizi ya maendeleo yalikuwa shilingi bilioni 1,942.4 na ya kawaida yalikuwa shilingi bilioni 5,226.9 ikilinganishwa na bajeti ya shilingi bilioni 3,819.0 na shilingi bilioni 7,790.5 kwa

mwaka 2010/2011 kwa mtiririko huo. Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka 2011/2012 nitakayowasilisha leo jioni itabainisha kwa kina na kwa undani zaidi, mwenendo wa mapato na matumizi ya Serikali kwa mwaka 2010/2011 na makadirio ya mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Spika, Deni la Taifa, hadi kufikia mwezi Desemba 2010, deni la Taifa lilikuwa limefikia Dola za Kimarekani bilioni 11,380.2 ikiwa ni ongezeko la Dola milioni 654.28 ikilinganishwa na deni la kipindi kama hicho mwaka 2009. Ongezeko hili lilitokana na mikopo mipya ya ndani na nje yenye masharti nafuu kwa ajili ya kugharamia miradi mbalimbali ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, malipo ya deni la Taifa katika kipindi cha robo tatu ya mwaka ulioishia Machi 2011 yalikuwa shilingi bilioni 803.64. Malipo ya deni la nje kwa kipindi hicho yalikuwa shilingi bilioni 73.66. Kati ya hizo, shilingi bilioni 29.06 zilikuwa ni malipo ya mtaji na shilingi bilioni 44.6 zilikuwa ni malipo ya riba. Malipo ya deni la ndani kwa robo tatu mwaka ulioishia Machi 2011 yalikuwa shilingi bilioni 730.3. Kati ya hizo, shilingi bilioni 556.7 zilitumika kulipia dhamana za Serikali zilizoiva kwa utaratibu wa kukopa na kulipia gharama zilizoiva na shilingi bilioni 173.6 zilikuwa ni malipo ya riba.

Mheshimiwa Spika, Ushirikiano wa Kiuchumi wa Kikanda na Kimataifa, mwaka 2010 Ushirikiano wa Tanzania Kimataifa na Kikanda uliendelea kuimarika na hivyo kuendelea kulijengea taifa mazingira mazuri ya shughuli za kiuchumi na kijamii.

Kanda hizo ni pamoja na za Jumuiya ya Afrika Mashariki; Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika; Umoja wa Afrika na Tume ya Uchumi ya Bara la Afrika; Umoja wa Nchi za Mashariki na Kusini mwa Afrika wa Udhibiti wa Biashara ya Fedha Haramu na Ufadhilli wa Ugaidi; na Tume za Pamoja za Kudumu za Ushirikiano.

Mheshimiwa Spika, Jumuiya ya Afrika Mashariki, katika mwaka 2010, Wakuu wa Nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki walikutana mjini Arusha na kuichagua Burundi kuwa Mwenyekiti kwa kipindi cha mwaka mmoja. Wakuu hao walielekeza Baraza la Mawaziri la Jumuiya kuchagua kwa makini vipaumbele vinavyotekelzeza katika kuandaa Mkakati wa Maendeleo ya Afrika Mashariki kulingana na uwezo wa kibajeti. Aidha, walielekeza Baraza la Mawaziri la Jumuiya likamilishe majadiliano ya kuanzishwa kwa Soko la Pamoja la Jumuiya ili kuweka mpangilio wa taasisi zitakazosaidia utekelezaji wake kuanzia mwaka 2011. Vilevile, walielekeza kuongeza kasi ya kufikia malengo ya pamoja ya uchumi jumla kwa nchi za Jumuiya ambayo ni kigezo muhimu kwa ajili ya kuanzisha matumizi ya sarafu moja.

Mheshimiwa Spika, katika hatua zilizochukuliwa za kuimarisha biashara mionganoni mwa nchi wanachama, biashara kati ya Tanzania na nchi hizi za Jumuiya ya Afrika Mashariki iliendelea kukua ambapo mauzo ya bidhaa za Tanzania katika nchi hizi yaliongezeka kwa asilimia 70.6 kufikia Dola za Kimarekani milioni 450 mwaka 2010 kutoka Dola milioni 263.8 mwaka 2009, wakati ambapo uagizaji wa bidhaa ulipungua kwa asilimia 8.2.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na matukio ya meli kutekwa kwenye eneo la Bahari ya Hindi hadi kufikia pwani za baadhi ya nchi za Jumuiya. Hali hii inahatarisha usalama na wala kuhujumu uchumi wa nchi wanachama. Hivyo, Wakuu wa Nchi walielekeza zichukuliwe jitihada za kukabiliana na tishio hilo katika ngazi za kitaifa, kijumuiya na kimataifa ili maharamia hao wasiweze kuhatarisha amani na usalama wala kuhujumu uchumi wa nchi wanachama.

Mheshimiwa Spika, Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika, mwaka 2010, Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika SADC ilishiriki kwenye mkutano wa pamoja wa uwekezaji kwenye miundombinu kwa Jumuiya Tatu za Afrika Mashariki; Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika na Soko la Pamoja la Nchi za Afrika Mashariki na Kusini mwa Afrika ulifanyika Nairobi Kenya. Mkutano huo ulitoa fursa ya pekee kwa SADC kubainisha maeneo ya uwekezaji kwenye miundombinu ya Mashariki na Kusini mwa Afrika kwa washirika wa maendeleo na wawekezaji binafsi kutoka sehemu mbalimbali za dunia. Vipaumbele vilivyoainishwa vipo katika miradi ya ukanda wa usafirishaji, usambazaji wa maji na usafi (*water and sanitation*), nishati na mawasiliano. Vipaumbele hivyo vipo katika Programu ya Uhamasishaji wa Uwekezaji ndani ya SADC ya mwaka 2010.

Mheshimiwa Spika, Umoja wa Afrika na Tume ya Uchumi ya Bara la Afrika, pamoja na ukuaji wa uchumi kwa nchi za Afrika katika kipindi cha muongo mmoja uliopita, imebainika kuwa tatizo la ajira limeendelea kuwa kubwa na linazidi kuongezeka. Hivyo, Umoja wa Afrika - AU, na Tume ya Uchumi ya Bara la Afrika - ECA, katika kikao chake cha tatu cha pamoja kilichofanyika Machi 2010, kilijadili namna ya kusaidia ukuaji wa Uchumi endelevu kwa lengo la kupunguza ukosefu wa ajira ndani ya Afrika. Hii ni kwa sababu ukosefu wa ajira sio kwamba unakwamisha tu jitihada za kupunguza umaskini bali pia ni chanzo cha kudidimiza rasilimali watu, kuongezeka kwa tofauti za vipato na kusababisha vurugu za kijamii katika nchi. Aidha, nchi zilishauriwa kuwa na mwelekeo wa kukuza uchumi unaoendana na ongezeko la ajira kwa wingi ili kufanikisha lengo la kupunguza umaskini.

Mheshimiwa Spika, Tume za Pamoja za Kudumu za Ushirikiano, Tume za pamoja za Ushirikiano kati ya Tanzania na nchi marafiki ziliendeleza mahusiano, ambapo mkutano wa nne wa Tume ya Kudumu ya Ushirikiano kati ya Tanzania na Algeria ulifanyika Dar es Salaam, Juni 2010. Mkutano huo ulikuwa wa manufaa makubwa kwa Tanzania kwa kuwa mkataba wa kufuta deni la dola za kimarekani milioni 144.14 ultiwa saini. Aidha, mazungumzo juu ya makubaliano ya kutotoza kodi mara mbili baina ya nchi hizi mbili bado yanaendelea.(*Makofi*)

Katika kipindi hicho, mkutano wa wataalam kati ya Tanzania na Brazil ulifanyika, ambapo suala la masharti nafuu ya kulipa deni la Tanzania inalodaiwa na Brazil kiasi cha dola za Kimarekani milioni 237.0 lilijadiliwa. Makubaliano ya awali ilikuwa kwamba tulipe sehemu ya deni ambalo lilikuwa ni kiasi cha dola za kimarekani milioni 17.6 na sehemu iliyobaki tungesamehewa. Mpaka sasa tumeshalipa kiasi cha dola za Kimarekani milioni 6.4. Aidha, ushirikiano kati ya Tanzania na Msumbiji

ulifanikisha ujenzi wa daraja la Umoja kati ya nchi mbili hizi, ambapo uzinduzi wake ulifanyika mwezi Mei 2010 na Marais wa Msumbiji na Tanzania.

Umoja wa Nchi za Mashariki na Kusini mwa Afrika wa Udhibiti wa Biashara ya Fedha Haramu na Ufadhilli wa Ugaidi (*ESAAMLG*).

Mheshimiwa Spika, Tanzania inaendelea kushiriki katika mikutano ya Baraza la Mawaziri la Umoja huo ambao makao makuu ya Sekretarieti yapo mjini Dar es Salaam. Aidha, Tanzania inaendelea kuboresha mfumo wa usimamizi wa Sekta ya Kifedha ili kuboresha mifumo hiyo kwa lengo la kudhibiti biashara ya fedha haramu katika shughuli za kiuchumi ambazo zinaweza kudhoofisha uchumi wa nchi.

Mheshimiwa Spika, Maendeleo ya Shughuli Mbalimbali za Kiuchumi na Kijamii, Mawaziri wa Wizara husika wataeleza kwa kina maendeleo katika maeneo yao; hivyo katika hotuba hii, nitatoa tathmini ya kiujumla tu ya maendeleo katika baadhi ya maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, Kilimo, Mifugo, Misitu na Uwindaji, shughuli za kiuchumi za kilimo zinazojumuisha mazao; mifugo; na misitu na uwindaji zilikua kwa kiwango cha asilimia 4.2 mwaka 2010 ikilinganishwa na asilimia 3.2 mwaka 2009.

Ukuaji huu ulitokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa mazao kufuatia kuwepo kwa hali nzuri ya hewa katika msimu wa kilimo wa mwaka 2009/10, kuimarika kwa miundombinu ya umwagiliaji; jitihada za Serikali za kuongeza ruzuku ya pembejeo za kilimo; na utekelezaji wa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo *ASDP*. (*Makofi*)

Aidha, mchango wa shughuli za kiuchumi za kilimo ulikuwa asilimia 24.1 ya Pato la Taifa mwaka 2010 ikilinganishwa na asilimia 24.6 mwaka 2009.

Mheshimiwa Spika, Uvuvi shughuli za kiuchumi katika uvuvi zilikua kwa kiwango cha asilimia 1.5 mwaka 2010 ikilinganishwa na asilimia 2.7 mwaka 2009. Kiwango kidogo cha ukuaji kilitokana na kuongezeka kwa ushindani wa mauzo ya samaki na mazao yake nje ya nchi; kupungua kwa kasi ya uvuvi, hususan katika maji baridi uliotokana na kudhibiti uvuaji holela na uharibifu wa mazingira katika mazalia ya samaki; vitendo vya uvuvi haramu; na matumizi ya zana duni za uvuvi. Aidha, mchango wa shughuli za uvuvi katika Pato la Taifa ulikuwa asilimia 1.4 kama ilivyokuwa mwaka 2009.

Mheshimiwa Spika, Viwanda na Ujenzi. Shughuli za viwanda na ujenzi zinajumuisha: Uzalishaji bidhaa viwandani; umeme na gesi; usambazaji wa maji; madini, uchimbaji wa mawe na ujenzi. Shughuli za kiuchumi katika viwanda na ujenzi zilikua kwa kiwango cha asilimia 8.2 mwaka 2010 ikilinganishwa na asilimia 7.0 mwaka 2009. Aidha, mchango wa shughuli za viwanda na ujenzi katika Pato la Taifa uliongezeka kutoka asilimia 22.0 mwaka 2009 hadi asilimia 22.4 mwaka 2010.

Mheshimiwa Spika, shughuli za uzalishaji bidhaa viwandani zilikua kwa kiwango cha asilimia 7.9 mwaka 2010 ikilinganishwa na asilimia 8.0 mwaka 2009. Kupungua kwa kiwango cha ukuaji kulitokana na kuongezeka kwa garama za uzalishaji. Mchango wa shughuli za uzalishaji bidhaa viwandani katika Pato la Taifa uliongezeka kutoka asilimia 8.6 mwaka 2009 hadi asilimia 9.0 mwaka 2010. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kiwango cha ukuaji wa shughuli za kiuchumi katika umeme na gesi kilikuwa asilimia 10.2 mwaka 2010 ikilinganishwa na asilimia 8.4 mwaka 2009. Hii ilitokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa umeme unaotokana na nguvu za maji; na juhudzi za Serikali za kuweka mitambo ya kuzalisha umeme kwa kutumia gesi. Shughuli za kiuchumi za umeme na gesi zilichangia asilimia 1.8 katika Pato la Taifa mwaka 2010 ikilinganishwa na asilimia 1.7 mwaka 2009. Pamoja na kuwa na mchango kidogo katika Pato la Taifa, umeme na gesi ni sekta muhimu inayotegemewa sana kwa maendeleo ya sekta nyingine kama vile uzalishaji viwandani na huduma.

Mheshimiwa Spika, shughuli za kiuchumi za ujenzi zilikua kwa kiwango cha asilimia 10.2 mwaka 2010 ikilinganishwa na asilimia 7.5 mwaka 2009. Ukuaji huo ulichangiwa na kuongezeka kwa shughuli za ujenzi na ukarabati wa barabara na madaraja; majengo ya kuishi na yasiyo ya kuishi; viwanja vya ndege; na miundombinu ya maji. Mchango wa shughuli za ujenzi katika Pato la Taifa ulikuwa asilimia 8.0 mwaka 2010 ukilinganisha na asilimia 7.9 mwaka 2009.

Mheshimiwa Spika, Huduma. Shughuli za utoaji huduma zinajumuisha biashara na matengenezo; uchukuzi; mawasiliano; hoteli na migahawa; utawala; elimu; afya; huduma za fedha na bima; na upangishaji wa majengo. Kiwango cha ukuaji wa shughuli za kiuchumi katika utoaji huduma kilikuwa asilimia 8.2 mwaka 2010 ikilinganishwa na asilimia 7.2 mwaka 2009. Viwango vya ukuaji katika shughuli zote ndogo za huduma viliongezeka mwaka 2010 kutokana na kuanza kuimarika kwa shughuli zilizoathiriwa na hali ya m dororo wa uchumi duniani kama vile shughuli ndogo za fedha, hoteli na migahawa, biashara na matengenezo na uchukuzi. Mchango wa shughuli za utoaji huduma katika Pato la Taifa ulikuwa asilimia 43.9 mwaka 2010 ikilinganishwa na asilimia 43.6 mwaka 2009.

Mheshimiwa Spika, huduma za mawasiliano katika mwaka 2010 zilikua kwa kiwango kikubwa zaidi kuliko shughuli nyingine za kiuchumi. Kiwango cha ukuaji kwa shughuli hizi kilikuwa asilimia 22.1 mwaka 2010 ikilinganishwa na asilimia 21.9 mwaka 2009. Ukuaji huu ulichangiwa na kuongezeka kwa wateja wa huduma za mawasiliano ya simu za m kononi. Mchango wa shughuli za mawasiliano katika Pato la Taifa uliendelea kuwa asilimia 2.1 mwaka 2010 kama ilivyokuwa mwaka 2009.

Mheshimiwa Spika, shughuli za biashara na matengenezo zilikua kwa asilimia 8.2 mwaka 2010 ikilinganishwa na asilimia 7.5 mwaka 2009. Ukuaji huo ulichangiwa zaidi na kuongezeka kwa mahitaji kufuatia kuanza kuimarika kwa uchumi wa dunia. Shughuli ndogo za biashara na matengenezo ndizo zilizokuwa na mchango mkubwa katika utoaji

wa huduma. Mchango wa shughuli za biashara na matengenezo ulikuwa asilimia 12.1 ya Pato la Taifa mwaka 2010 ikilinganishwa na asilimia 11.8 mwaka 2009. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, masuala mtambuka. Idadi ya Watu idadi ya watu Tanzania kwa mwaka 2010 ilikadiriwa kuwa 43,187,823. Kati ya hao, wanawake walikuwa 21,935,400, sawa na asilimia 50.8 na wanaume walikuwa 21,252,423, sawa na asilimia 49.2. Tanzania Bara ilikadiriwa kuwa na jumla ya watu 41,914,311, sawa na asilimia 97.1 ya watu wote ambapo Tanzania Zanzibar ilikuwa na watu 1,273,512, sawa na asilimia 2.9 ya watu wote wa Tanzania. Mgawanyo wa watu unaonesha kuwa watu 31,809,808, sawa na asilimia 73.7 ya watu wote wanaoishi vijijini, wakati watu 11,378,015, sawa na asilimia 26.3 wanaoishi mijini. Makadirio haya yanatokana na kiwango cha ukuaji wa idadi ya watu cha asilimia 2.9 cha Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2002. Sensa kama hii inatarajiwa kufanyika tena mwakani (2012) na maandalizi yake yanaendelea vizuri.

Mheshimiwa Spika, mchanganuo wa idadi ya watu Tanzania unaonesha kuwa asilimia 44.4 ya watu wote ni wenye umri chini ya miaka 15. Idadi ya watu waliokuwa na umri kati ya miaka 15 - 24 walikadiriwa kuwa 8,580,351, sawa na asilimia 19.9 ya watu wote. Idadi ya watu wenye miaka kati ya 15 - 64, ambao ndio nguvukazi, ilikuwa ni 22,661,280, sawa na asilimia 52.5 ya watu wote. Watu wenye umri wa miaka 65 au zaidi walikuwa ni 1,361,435, sawa na asilimia 3.2 ya watu wote. Kati ya hao, wanawake walikuwa 718,299 na wanaume ni 643,136. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nguvukazi na Ajira.kulingana na matokeo ya Utafiti wa Nguvukazi na Ajira wa mwaka 2006, nguvukazi nchini ilikuwa watu milioni 18.8 ambapo milioni 9.0 walikuwa wanaume na milioni 9.7 walikuwa wanawake. Vilevile, matokeo hayo yanaonesha kuwa watu milioni 16.6 walikuwa wameajiriwa na milioni 2.2 walikuwa hawajaajiriwa, sawa na asilimia 11.7 ya nguvukazi yote nchini. Kati ya walioajiriwa, watu milioni 8.5 walikuwa wanawake na wanaume milioni 8.0. Hata hivyo, kulingana na matokeo ya Sensa ya Idadi ya Watu na Makazi ya mwaka 2002, ilikadiriwa kuwa ifikapo mwaka 2010 kungekuwa na nguvukazi nchini (miaka 15 – 64) ya watu 22,661,280. Sekta ya kilimo iliendelea kuongoza, ambapo zaidi ya asilimia 70 ya walioajiriwa nchini wanajishughulisha na kilimo.

Mheshimiwa Spika, Utawala Bora. Mwaka 2010. Serikali iliendelea kutekeleza azma yake ya utoaji haki kwa wote kwa kutafsiri Sheria kumi na nne kutoka lugha ya Kiingereza kwenda Kiswahili. Vilevile, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora iliendelea na juhudhi zake za kukuzi, kulinda na kuhifadhi haki za binadamu na utawala bora katika jamii.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2010, Tume iliendelea kushughulikia malalamiko ya wananchi ambapo jumla ya malalamiko mapya na ya zamani 7,858 yалишүгүлики. Kati ya hayo, Tume ilihiitimisha malalamiko 1,003 mwaka 2010 ikilinganishwa na malalamiko 657 yалишүгүлики na kuhitimidwa mwaka 2009. Malalamiko 6,855 yалишүгүлики yanaendelea kushughulikia.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010, jumla ya mashauri 2,624 yalipokelewa na Mahakama ya Rufani. Kati ya hayo, mashauri 627 yalikamilishwa na mashauri 1,997 yaliendelea kushughulikiwa. Aidha, katika Mahakama za Hakimu Mkazi na Wilaya, kulikuwa na jumla ya mashauri 62,154. Kati ya hayo, mashauri 46,977 yalisikilizwa na mashauri 15,177 yaliendelea kufanyiwa kazi. Vile vile, katika Mahakama za Mwanzo, jumla ya mashauri 218,767 yalipokelewa ambapo mashauri 167,228 yalisikilizwa na 51,939 yaliendelea kusikilizwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mwaka 2010, Serikali iliendelea na utekelezaji wa Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa (*NACSAP II*). Katika utekelezaji wa Mkakati huo, TAKUKURU ilipokea na kufanyia uchunguzi kesi za rushwa 870. Kati ya kesi hizo, kesi 587 zilifikishwa mahakamani na kesi 64 zilitolewa hukumu.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2010, Serikali iliendelea na utoaji wa mafunzo ya Utawala Bora ambapo kamati za maadili za Wizara 21 na Taasisi za Umma 32 zilipatiwa mafunzo ya utawala bora na usimamiaji wa Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa.

Mheshimiwa Spika, katika kuendelea kupambana na ukatili nchini, Serikali ilitoa mafunzo kuhusu utokomezaji wa ukatili dhidi ya wanawake, watoto na watu wenye ulemavu wa ngozi. Mafunzo haya yaliwahusisha wakuu wa vituo vya polisi 40 na viongozi wa viji 43 kutoka mikoa ya Kigoma, Arusha, Dodoma, Tabora na Manyara. Aidha, mafunzo hayo pia yalitolewa kwa wasimamizi wa sheria katika Wilaya za Rorya, Tarime, Bukombe na Kahama.

Mheshimiwa Spika, Mazingira. Katika mwaka 2010, miongozo mitatu ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira iliandaliwa. Miongozo hiyo ni: Mwongozo wa Kuandaa Mipango ya Usimamizi wa Mazingira ya Wizara na Wakala wa Serikali za Mitaa; Mwongozo wa Ujenzi wa Minara ya Mawasiliano; na Mwongozo wa Kushughulikia Changamoto za Mabadiliko ya Tabianchi.

Mheshimiwa Spika, Serikali iliendelea kutekeleza programu na miradi mbalimbali kwa ajili ya kuhifadhi bioanuwai katika ziwa Tanganyika, mradi wa kuhifadhi mazingira Bonde la Kihansi, na Mradi wa Kuhifadhi Mazingira Pwani katika Bahari ya Hindi. Aidha, Serikali iliendelea kuratibu utekelezaji wa Mkataba wa Kyoto unaolenga kupunguza uzalishaji wa hewa ukaa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vita dhidi ya ukimwi mwaka 2010, upanuzi wa huduma kwa watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI ulifanyika ambapo huduma ziliongezeka kutoka halmashauri 110 mwaka 2009 hadi halmashauri 133.

Idadi ya watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI na ambao wanapata dawa za kupunguza makali ya VVU iliongezeka kwa asilimia 10.3 kutoka watu 284,227 mwaka 2009 hadi watu 313,384 mwaka 2010. Katika idadi hiyo, watoto chini ya miaka 15 walikuwa 28,309 na watu wazima kuanzia miaka 15 walikuwa 285,075.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2010, vituo vinavyotoa huduma ya unasihi na upimaji viliongezeka kwa asilimia 24.5 kutoka vituo 1,743 mwaka 2009 hadi vituo 2,170. Mafunzo mbalimbali yalitolewa kwa washauri 300 na kufanya idadi ya watoa huduma kuwa 5,365 nchini kote. Hadi Desemba 2010, watu wapatao 8,890,207 walikuwa wamepimwa na majibu kutolewa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, Jinsia. Mwaka 2010, Serikali iliendelea kuhakikisha uwepo wa uwiano wa kijinsia kwenye ngazi mbalimbali za uongozi nchini. Katika kipindi cha mwaka 2006 hadi 2010, uwiano wa wanawake kushiriki katika ngazi za maamuzi uliongezeka kutoka asilimia 26 mwaka 2006 hadi asilimia 31 mwaka 2010. Kiwango hiki ni juu ya lengo la MKUKUTA la asilimia 30 kwa mwaka 2010 lakini chini ya lengo la SADC la asilimia 50. Mchanganuo wa baadhi ya nafasi zilizoongezeka zinazoshikiliwa na wanawake tangu mwaka 2006 hadi kabla ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2010 ni kama ifuatavyo:-

Majaji 13 hadi 34; Mawaziri 4 hadi 10; Makatibu Wakuu 7 hadi 9; Makatibu Tawala za Mikoa 4 hadi 10; Wakuu wa Wilaya 20 hadi 25; Wakurugenzi wa Halmashauri 14 hadi 35; na Wakurugenzi kwenye wizara na taasisi, 19 hadi 133. Aidha, kufuatia matokeo ya uchaguzi mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani uliofanyika Oktoba 2010, idadi ya Wabunge wanawake imefikia 126, sawa na asilimia 36 ya wabunge wote 350 waliopo kwa sasa. Aidha, idadi ya Mawaziri wanawake ni asilimia 26.7 ya mawaziri wote 30 waliopo.

Mheshimiwa Spika, Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 ilizinduliwa rasmi mwaka 2000. Mwaka 2010, Serikali ilifanya mapitio ya utekelezaji wa Dira. Malengo makuu ya mapitio hayo yalikuwa ni kuchambua mafanikio yaliyofikiwa katika kutekeleza malengo ya Dira tangu ilipozinduliwa; kubainisha fursa na changamoto ambazo inabidi zifanyiwe kazi katika kipindi kilichobaki toka sasa hadi 2025; na kupendekeza malengo mahsus ya miaka mitano mitano na hatua au sera mbadala ambazo zitaingizwa katika mipango ya maendeleo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, mapitio ya utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 yalibainisha kwamba dhana ya Dira ya Taifa ya Maendeleo bado ni sahihi na inatekelezeka. Aidha, mapitio hayo yalibainisha haja ya kuwa na mfumo linganishi wa utayarishaji na utekelezaji wa mipango ya muda wa kati na mrefu. Vile vile, mapitio yaliweza kubainisha changamoto ambazo Serikali inaendelea kuzifanyia kazi. Changamoto hizo ni kama ifuatavyo:-

- (i) Kwamba ingawa ukuaji wa uchumi ulikuwa unaongezeka, ukuaji huo ulikuwa chini ya kiwango kinachohitajika kufikia shabaha na malengo ya Dira;
- (ii) Vyanzo vya ukuaji wa uchumi havikuwagusa watu wengi hususan, maskini vijijini na katika maeneo ya pembezoni, na havikuweza kuzalisha fursa za ajira za kutosha;

(iii) Umaskini ulipungua lakini kwa kiwango kidogo hususan, vijijini na katika kaya zinazotegemea kilimo;

(iv) Japokuwa kwa kipindi kirefu mfumuko wa bei uliendelea kuwa wa chini na tarakimu moja, athari za majanga yatokanayo na mabadiliko ya hali ya hewa katika uzalishaji wa mazao, sambamba na ongezeko la bei za mafuta katika soko la dunia zimesababisha kuongezeka kwa kasi ya upandaji bei katika siku za karibuni pamoja na gharama za uzalishaji; na

Tanzania imejaliwa kuwa na fursa za rasilimali za asili nyingi, kijiografia imekaa eneo zuri linalopakana na bahari na kushiriki kikamilifu katika mtangamano wa jumuiya za kikanda na kimataifa. Hata hivyo, fursa hizo hatujaweza kuzitumia kikamilifu kuinua uchumi. Tunahitaji kuboresha miundombinu hususan, ya usafirishaji ili tuweze kutumia kikamilifu fursa ya kupakana na bahari kuweza kuwa kitovu cha biashara cha kuhudumia nchi za maziwa makuu na zisizopakana na bahari. (*Makofii*)

Aidha, suala la upatikanaji wa nishati ya umeme ya uhakika ni budi litafutiwe ufumbuzi na mkakati uliopo ni kuboresha miundombinu yake pamoja na kuongeza uzalishaji wa umeme kwa kutumia vyanzo mbalimbali vikiwemo maji, upepo, juu, gesi na makaa ya mawe.

Mheshimiwa Spika, MKUKUTA na Malengo ya Maendeleo ya Milenia (MDGs). Awamu ya kwanza ya Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania (MKUKUTA) ilitekelezwa kwa kipindi cha miaka mitano kuanzia mwaka 2005/2006 hadi 2009/10. Katika utekelezaji wake, mafanikio kadhaa yalipatikana yakiwemo ukuaji wa uchumi, ongezeko katika ukusanyaji wa mapato ya ndani, usimamizi thabiti wa fedha za umma, uimarishaji wa barabara vijijini, pamoja na uboreshaji wa sekta za elimu, afya na maji. Wastani wa kiwango cha ukuaji wa uchumi ulikuwa asilimia 6.9 kati ya mwaka 2005 na 2010 na hivyo kuwa ndani ya lengo la MKUKUTA la asilimia 6 – 8. (*Makofii*)

Hata hivyo, zipo changamoto zilizojitokeza ikiwa ni pamoja na kasi ndogo ya kupungua kwa kiwango cha umaskini, upatikanaji na ubora wa huduma kwa viwango vilivyokusudiwa, ushiriki mdogo wa sekta binafsi, na uhaba wa rasilimali.

Mheshimiwa Spika, changamoto nyingine ziliwuwa nje ya uwezo wa Serikali, zikiwemo kupanda kwa bei za mafuta ya petroli katika soko la dunia, ukame uliotokea katika maeneo mengi nchini katika kipindi cha mwaka 2005/2006 na 2008/09, ukosefu wa umeme wa uhakika na kuyumba kwa uchumi wa dunia kulikoanza mwishoni mwa mwaka 2008.

Pamoja na uhaba wa rasilimali, Serikali ilikuwa ikiongeza mwaka hadi mwaka kiasi cha fedha kinachotengwa kwa ajili ya utekelezaji wa MKUKUTA kutoka asilimia 54.1 ya bajeti yote mwaka 2005/06 wakati utekelezaji wa MKUKUTA ulipoanza hadi asimia 71.2 mwaka 2009/2010.

Mheshimiwa Spika, mafanikio yaliyopatikana, changamoto, na mambo tuliyojifunza katika kipindi chote cha utekekelezaji wa awamu ya kwanza ya MKUKUTA yamechambuliwa kwa kina katika taarifa ya utekelezaji wake kwa mwaka 2009/10. Serikali iliandaa awamu ya pili ya MKUKUTA ambao ulipitishwa mwezi Oktoba 2010. Mchakato wa uandaaji wa awamu hii uliwashirikisha wadau wengi na ulizingatia zaidi mambo tuliyojifunza na mikakati ya kukabiliana na changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji wa awamu ya kwanza ya MKUKUTA.

Mheshimiwa Spika, mapitio ya utekelezaji wa Malengo ya Milenia yanaonesha kuwa, Tanzania imefanya vizuri katika baadhi ya viashiria kama vile uandikishaji katika elimu ya msingi, kupunguza vifo vya watoto wachanga, kupunguza vifo vya watoto chini ya miaka mitano na usawa wa jinsia. Mwaka 2010, kiwango cha kukatisha masomo katika elimu ya msingi kilishuka hadi asilimia 2.6 kutoka asilimia 3.7 mwaka 2009 kutokana na kuboreshwa kwa mazingira ya kufundishia na kujifunzia. Aidha, wastani wa uwiano wa mwalimu kwa wanafunzi uliimariika kutoka uwiano wa mwalimu mmoja kwa wanafunzi 54 mwaka 2009 hadi mwalimu mmoja kwa wanafunzi 51 mwaka 2010 ikilinganishwa na lengo la mwalimu mmoja kwa wanafunzi 45. Aidha, kwa mujibu wa Utafiti wa Afya na Idadi ya Watu wa mwaka 2009/2010, kiwango cha vifo vya watoto wachanga kilipungua mwaka 2010 kufikia vifo 51 kwa kila watoto 1,000 waliozaliwa hai kutoka vifo 68 mwaka 2007, wakati kiwango cha vifo vya watoto walio chini ya umri wa miaka mitano kilipungua mwaka 2010 kufikia 81 kwa kila watoto 1,000 waliozaliwa kutoka vifo 112 mwaka 2007.

Mheshimiwa Spika, changamoto bado zipo katika viashiria vingine, kama vile, afya ya uzazi wa mama na umaskini wa kipato. Hivyo, kipaumbele sasa kimewekwa katika kuongeza ufanisi katika maeneo hayo ya changamoto na kuimarisha zaidi utekelezaji pale ambapo Tanzania imepata mafanikio kiasi.

Mheshimiwa Spika, uwezeshaji wananchi kiuchumi, katika kutekeleza Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi, mafanikio yamepatikana katika utoaji wa mikopo na uanzishwaji wa *SACCOS* na vikundi vidogo vidogo vya kiuchumi vya vijana na wanawake. Mikopo hiyo ilitolewa kuititia mifuko na program mbalimbali ikijumuisha Program ya Taifa ya Kuongeza Kipato; Mpango wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Kuongeza Ajira; Mfuko wa Uwezeshaji Mwananchi; na Mradi wa Kutoa Mikopo kwa Wajasiriamali Wadogo (*SELF*). (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, mwaka 2010, Serikali kuititia Mfuko wa Uwezeshaji wa Wananchi ilitoa mikopo yenyenye masharti nafuu ya thamani ya shilingi bilioni 1.2 na hivyo kufanya jumla ya mikopo iliyotolewa na Mfuko hadi sasa kufikia shilingi bilioni 4.6 kwa wajasiriamali. Mikopo hiyo ilitolewa kwa vyama 30 vya akiba na mikopo (*SACCOS*) katika mikoa ya Mtwara, Lindi, Manyara, Singida na Rukwa. Aidha, mikopo hiyo iliawezesha wajasiriamali kukuza uchumi wao kwa kusaidia ununuzi wa pembejeo za kilimo, kama matrekta ya mikono (power tillers) na hivyo kuwa na uwezo wa kuongeza ukubwa wa mashamba na kipato. Hadi kufikia Desemba 2010, kiasi cha shilingi bilioni 4.34 zilirejeshwa, ikiwa ni sawa na asilimia 94 ya fedha zilizokopeshwa.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2010, utekelezaji wa Mpango wa Uwezeshaji wa Wananchi Kiuchumi na kuongeza Ajira uliendelea kutoa mikopo yenyé masharti nafuu kupidia Benki na asasi nyingine za kifedha. Mikopo yenyé thamani ya shilingi bilioni 47.14 ilitolewa kwa wajasiriamali 72,197. Kati ya wajisiriamali hao, wanaume walikuwa 45,858, sawa na asilimia 64 na wanawake walikuwa 26,339, sawa na asilimia 36. Hadi kufikia Desemba 2010, shilingi bilioni 36.1 ambazo ni sawa na asilimia 76.6 ya mikopo iliyotolewa zilikuwa zimerejeshwa.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2010, Serikali kupidia Mradi wa Kutoa Mikopo kwa Wajasiriamali Wadogo (*SELF*) ilitoa mikopo yenyé thamani ya shilingi bilioni 8.7. Aidha, katika kipindi hicho, Mradi ulikusanya marejesho ya mikopo kiasi cha shilingi bilioni 6.1 sawa na asilimia 70.1 ya mikopo iliyotolewa. Mikopo hiyo iliwa fikia wananchi 8,631, wenye kipato cha chini waliopo mijini na vijijini. Kati ya hao, wanawake walikuwa 5,092 sawa na asilimia 58 na wanaume walikuwa 3,539 sawa na asilimia 41.

Mheshimiwa Spika, uendelezaji wa sekta binafsi, Bunge lako tukufu lilipitisha Sheria ya Ubia Kati ya Sekta ya Umma na Binafsi - *PPPA* Na. 19 ya mwaka 2010 mwezi Agosti 2010. Madhumuni ya Sheria hii ni kuweka mfumo mzuri wa kisheria kwa ajili ya kuratibu ushiriki wa sekta binafsi katika uwekezaji wa miradi na huduma za ubia baina ya sekta ya umma na sekta binafsi. Vitengo vya *PPP* tayari vimeanzishwa katika Wizara ya Fedha na Ofisi ya Waziri Mkuu ili kuratibu masuala yanayohusiana na *PPP*. Kupitia vitengo hivyo, Serikali imekamilisha mkakati na mwongozo wa utekelezaji wa sheria ya *PPP*, hususan katika miradi mikubwa ya miundombinu. Kanuni za utekelezaji wa Sheria ya *PPP* pia zimekamilika. Sambamba na hilo, Serikali kupidia Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Biashara Tanzania (MKUMBITA) inaendelea jitihada za kuondoa urasimu ili kupunguza muda na gharama za kuendesha shughuli za uchumi na biashara nchini.

Mheshimiwa Spika, uwekezaji mitaji ya kigeni ya moja kwa moja, mwaka 2010, thamani ya mitaji ya uwekezaji kutoka nje ya nchi – *FDI*, ilikuwa Dola za Kimarekani milioni 573.3 ikilinganishwa na dola za Kimarekani milioni 558.4 mwaka 2009, sawa na ongezeko la asilimia 2.7. Ongezeko hili linatokana na kuanza kuimarika kwa uchumi wa dunia. Sekta za Viwanda, Utalii, na Majengo ya Biashara ziliongoza katika uwekezaji na kutoa fursa za ajira.

Mheshimiwa Spika, Misingi na Malengo ya Uchumi na Maendeleo ya jamii, malengo ya sera za uchumi jumla katika mwaka 2011/2012 yatakuwa yafuatayo:-

- (i) Pato halisi la Taifa litakua kwa asilimia 6.0 mwaka 2011, na asilimia 7.2 mwaka 2012;
- (ii) Kuendelea kudhibiti kasi ya upandaji bei ili ibaki kwenye viwango vya tarakimu moja;

(iii) Kuongezeka kwa mapato ya ndani yatakayofikia uwiano wa asilimia 17.2 ya Pato la Taifa mwaka 2011/2012 na kuendelea kuongezeka kwa wastani wa asilimia 17.5 kwa mwaka kwa kipindi cha muda wa kati;

(iv) Kudhibiti ongezeko la ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi unaotarajiwa kukua kwa asilimia 19.0 mwaka 2011/2012 na asilimia 18.6 mwaka 2012/2013; Ukuaji huu unalenga kuwiana na malengo ya ukuaji wa uchumi, na kasi ya upandaji bei;

(v) Kuwa na akiba ya fedha za kigeni itakayoweza kukidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma toka nje kwa kipindi kisichopungua miezi 4.6;

(vi) Kupunguza tofauti ya viwango vya riba; na

(vii) Kuwa na kiwango imara cha ubadilishaji wa fedha kitakachotokana na mwenendo wa soko la fedha.

Mheshimiwa Spika, malengo tuliyokusudia ya uchumi jumla katika kipindi cha mwaka 2011/2012 yatafikiwa kwa kuzingatia misingi ifuatayo:-

(i) Kuendelea kuimarika kwa amani, utulivu na utengamano;(ii) Vyanzo vya maji vitaendelea kuhifadhiwa na kukidhi mahitaji;

(iii) Utengamavu wa viashiria vya uchumi jumla na maendeleo ya jamii utaendelea kuimarika;

(iv) Mapato ya ndani yataongezeka na kuboreshwa ikiwa ni pamoja na kubuni vyanya vya kodi, kuimarisha ukusanyaji wa kodi ya majengo, na kupunguza misamaha ya kodi ili kuweza kugharamia vipaumbele vilivyoainishwa;

(v) Ufanisi katika usimamizi wa matumizi ya fedha za umma utaongezeka;

(vi) Rasilimali zitaelekezwa kwenye maeneo yanayochochea ukuaji wa uchumi kwa haraka zaidi;(vii) MKUKUTA II utekelezwa kama ulivyopangwa;

(viii) SAGCOT na nguzo 10 za Kilimo Kwanza zitatekelezwa kama ilivyopangwa;

(ix) Mazingira ya biashara yataboreshwa ili kuendeleza ushirikishwaji wa sekta binafsi; na

(x) Sera ya fedha (*monetary policy*) itaimarika ili iendane na sera za bajeti (*fiscal policies*) zitakazosaidia kupunguza mfumuko wa bei na tofauti ya riba za kukopa na amana, na kuongeza mikopo kwa sekta binafsi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika majumuisho, baada ya kueleza hali ya uchumi wa Taifa, matarajio, misingi na malengo ya mpango na bajeti kwa kipindi cha mwaka 2011/2012 ni wazi kwamba hatua zilizochukuliwa na Serikali katika kuimarisha uchumi kwa kiasi kikubwa zimeweza kuzaa matunda yaliyotarajiwa. Juhudi zitaendelea kuelekezwa katika kuhakikisha ukuaji wa uchumi unaimarika zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda kusisitiza mambo muhimu ambayo tunahitaji kuyapa msukumo zaidi katika utekelezaji na ufuatiliaji wa karibu kwa mwaka 2011/2012 kama ifuatavyo:-

- (i) Kuongeza msukumo katika utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2025;
- (ii) Kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi na kukuza Pato la Taifa;
- (iii) Kuongeza uwekezaji katika maeneo ya kimkakati na yenye mwingiliiano kisekta hususan, umeme, bandari, reli, maji na chakula cha hifadhi na kuhimiza ushiriki wa sekta binafsi katika maeneo hayo;
- (iv) Kutumia fursa za nchi yetu kuwa kiungo muhimu kibiashara na nchi zinazotuzunguka ambazo hazina bandari;
- (v) Kuhimiza na kuhamasisha utekelezaji wa Kilimo Kwanza;
- (vi) Kujizatiti katika kuboresha mazingira ya biashara; na
- (vii) Kuongeza na kusimamia mapato ya ndani ili kupunguza utegemezi na kuimarisha usimamizi katika matumizi ya fedha za umma. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofî*)

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Ahsanteni sana. Kwa hiyo, hoja hii imeungwa mkono. Kama ulivyo utaratibu wetu itaunganika na Hoja ya Bajeti itakayosomwa kuanzia saa 10.00 jioni. Halafu kutokana na mabadiliko tuliyoyafanya siku ya Jumatatu tarehe 13 Juni, 2011 Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, anayehusika na Mambo ya Mipango, Tume ya Mipango, atakuja kusoma Hotuba inayohusiana na kuwasilisha Mpango wa Miaka Mitano. Tutajadili siku mbili, halafu Hoja hii na ile itakayowasilishwa jioni ya leo, itajadiliwa kwa muda wa siku tano baada ya kupitisha ule Mpango kwa utaratibu tuliojipangia. (*Makofî*)

Pia mtaona kutakuwa na mabadiliko kidogo kwenye uwasilishaji wa Wizara. Lakini mtapewa mabadiliko haya kikamilifu baadaye. Sasa hivi sina sababu ya kuwasomeeni kwa sababu haya mabadiliko ni ya mwezi Julai, 2011.

Kwa hiyo, mtapewa nakala nyingine ya mabadiliko ambayo yako sahihi. Wakati natambulisha wageni wangu kwa bahati mbaya katika Orodha niliyosoma Mheshimiwa Profesa Ibrahim Lipumba (CUF) alikuwepo, lakini hakuwepo kwenye orodha niliyosoma mimi. Kwa hiyo, sikumtambua. Naomba nimtambue uwepo wake hapa Waheshimiwa Wabunge. Ahsante sana. (*Makofi*)

Kwa hiyo, wale wanaohusika na wageni wetu wanaweza kupata nakala za vitabu hivi. Ila tu huwa hawaruhusiwi kusoma tukiwa humu ndani. Lakini tukitoka nje wanaruhusiwa kuwa navyo. Makamu Mwenyekiti wa *Bunge Sports Club* amesema niwatangazieni ninyi wachezaji wote wa Timu ya Mpira na Timu ya Netiboli kufika kwenye mazoezi saa 12 asubuhi uwanja wa Jamhuri, Dodoma. Nadhani kila siku sijui. Lakini lengo ni kijiandaa kwa mechi wiki ijayo na Timu ya *Bongo Movies* nyie nadhani mnaijua hii.

Kwa hiyo, mujiandae na sisi tunaomba kupata ushindi kwa niaba yetu halafu sisi tuendelee kufurahi. Kwa hiyo, wanaohusika wote saa 12 asubuhi mazoezi na wengine pia tulikubaliana tufanye mazoezi. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge kwa sababu sina tangazo lingine na kwa sababu mnatakiwa mjiandae kwa sababu ya mkutano wa saa kumi jioni. Kwa hiyo, nataka nisitishe shughuli hizi mpaka saa 10.00 jioni. (*Makofi*)

(*Saa 5.33 asubuhi Bunge lilisitishwa hadi saa 10.00 jioni*)

(*Saa 10.00 jioni, Bunge lilirudia*)

## **HOJA ZA SERIKALI**

### **Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali Kwa Mwaka 2011/2012**

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likubali kujadili na kupitisha makadirio ya mapato na matumizi ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2011/2012. Pamoja na hotuba hii, viro vitabu vinne vinavyoelezea kwa kina takwimu mbalimbali za Bajeti.

Kitabu cha kwanza kinahusu makisio ya mapato. Kitabu cha pili kinaelezea makisio ya matumizi ya kawaida kwa Wizara na Idara zinazojitegemea ambapo cha tatu kinahusu makisio ya matumizi ya kawaida kwa Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa

na cha nne kinalezea makadirio ya matumizi ya maendeleo kwa Wizara, Idara zinazojitegemea, Mikoa pamoja na Mamlaka za serikali za Mitaa. Aidha, upo Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2011, ambao ni sehemu ya Bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dokta Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuchaguliwa tena kuongoza kwa muhula wa pili wa Serikali ya Awamu ya Nne. Aidha ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais, kwa imani kubwa aliyonayo kwangu, kwa kunichagua tena kwa mara nyingine kuongoza Wizara kubwa na nyeti. Namuahidi Mheshimiwa Rais, kwamba nitafanya kazi hii kwa uwezo wangu na ujuzi wangu wote na kwamba sitamwangusha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pia nampongeza Dokta Mohammed Gharib Billal, kwa kuchaguliwa kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Vilevile nampongeza Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge, na kuteuliwa tena na hatimaye kuitishwa na Waheshimiwa Wabunge, kuwa Waziri Mkuu kwa muhula wa pili wa Serikali ya Awamu ya Nne. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda kukupongeza wewe binafsi Mheshimiwa Spika, Anna Makinda, kwa kuchaguliwa kuwa Spika na hivyo kuwa mwanamke wa kwanza kuongoza Bunge katika Afrika Mashariki. Kuchaguliwa kwako kunatokana na imani kubwa waliyonayo Waheshimiwa Wabunge, kwa kuzingatia busara zako, uwezo na uzoefu wako ndani ya Bunge hili.

Napenda pia nimpongeze Mheshimiwa Job Ndugai, kwa kuchaguliwa kuwa Naibu Spika. Nawapongeza pia Mawaziri wenzangu wote pamoja na Naibu Mawaziri wote, kwa kuteuliwa kwao na Mheshimiwa Rais, kushika nyadhifa hizo. Aidha napenda niwapongeze Wabunge wote kwa kuchaguliwa na kuteuliwa kuingia katika Bunge hili Tukufu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba pia nichukue fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa wale wote walioshiriki kwa namna moja au nyingine kufanikisha matayarisho ya Bajeti hii. Maandalizi ya Bajeti ya Serikali, yanahusisha wadau na vyombo mbalimbali. Kipekee, naishukuru Kamati ya Fedha na Uchumi, chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa Dokta Abdallah Omari Kigoda, Mbunge wa Handeni, pamoja na Kamati nyingine za kisekta kwa ushauri mzuri walioutoa wakati wa kuchambua mapendekezo ya Bajeti hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba niishukuru kwa namna ya pekee Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kutayarisha kwa wakati Muswada wa Sheria wa Fedha ya Mwaka 2011 na nyaraka mbalimbali za sheria ambazo ni sehemu ya Bajeti hii. Kwa upande wa Wizara ya Fedha, nawashukuru Naibu Mawaziri Mheshimiwa Gregory Teu na Mheshimiwa Pereira Ame Silima. Namshukuru Katibu Mkuu, ndugu Ramadhani Musa Khijjah na Naibu Makatibu Wakuu, Laston Msongole, Dokta Servacius B. Likwelile na Elizabeth Nyambibo. Napenda kuwashukuru Profesa Benno Ndulu Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania, Harry Kitilya, Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato

Tanzania na Dokta Albina Chuwa, Mkurugenzi Mkuu wa Ofisi ya Takwimu ya Taifa. Aidha napenda kuwashukuru Wakuu wa Idara na wafanyakazi wote Wizara ya Fedha. Vile vile namshukuru Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali, kwa kuchapisha hotuba hii kwa wakati. Mwisho nawshukuru Wataalamu na wale wote waliota mapendekezo kuhusu Sera, mikakati na masuala mbalimbali ya kodi ambayo yamezingatiwa katika kuandaa Bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, huu ni Mkutano wa kwanza wa Bajeti kwa Bunge hili baada ya Uchaguzi Mkuu wa Rais na Wabunge, uliofanyika mwezi Oktoba, 2010 na kukirejesha Chama Cha Mapinduzi pamoja na Serikali yake kwenye kipindi cha pili cha Awamu ya Nne. Wananchi wana matumaini makubwa kwa Bunge hili kwamba litasaidia kuongeza kasi ya kuwapatia maendeleo na kuondokana na umasikini wa kipato unaowakabili wananchi walio wengi. Hili linajidhihirisha kwa uwepo wa Waheshimiwa Wabunge, wenye umri, jinsia, elimu na uzoefu mbalimbali. Ni matumaini ya Serikali kuwa uwepo huo wa Waheshimiwa Wabunge, utakuwa ni chachu katika kuwaletaa maendeleo wananchi kwa ari zaidi, kasi zaidi na nguvu zaidi. Bajeti ya mwaka wa fedha unaoishia 2010/2011, imeendelea kutumika kama chombo muhimu katika kutekeleza Sera na Malengo ya Uchumi na Maendeleo ya Jamii. Katika kipindi hiki, yamekuwepo mafanikio ya kuridhisha katika kutoa huduma bora kwa wananchi na kuimarisha miundombinu ili kuwzesha kukua kwa uchumi na kupunguza umaskini. Bajeti ya mwaka 2011/2012 itazingatia vipaumbele vifuatavyo:-

- (i) Umeme;
- (ii) Maji;
- (iii) Miundombinu ya usafiri na usafirishaji (reli, bandari, barabara, viwanja vya ndege, Mkongo wa Taifa);
- (iv) Kilimo na umwagiliaji; na
- (v) Kupanua ajira kwa sekta binafsi na ya umma.

Mheshimiwa Spika, Bajeti itahakikisha pia kuwa mafanikio yaliyopatikana katika sekta za elimu na afya yanalindwa pamoja na kuimarisha ubora wa huduma zinazotolewa.

Mheshimiwa Spika, Mikakati ya Kupunguza Makali ya Maisha kwa Mwananchi. Serikali inatambua changamoto zinazowakabili wananchi katika kupambana na makali ya maisha. Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2011/2012, pamoja na mambo mengine, inalenga katika kuchukua hatua za kurekebisha hali hiyo. Kumekuwepo na changamoto mbalimbali ambazo zinahitaji hatua za makusudi kuchukuliwa na wadau mbalimbali ikiwemo Serikali, sekta binafsi na mwananchi mmoja mmoja ili kupunguza makali ya maisha kwa mwananchi. Hatua zitachukuliwa maeneo yafuatayo:-

(i) Mheshimiwa Spika, Kasi ya ongezeko la bei za bidhaa na huduma nchini pamoja na mambo mengine inasababishwa na: kuongezeka kwa bei za mafuta katika soko la dunia; kutopatikana kwa umeme wa uhakika na hivyo kuathiri uzalishaji; na upungufu wa chakula nchini na nchi jirani. Serikali itachukua hatua mbalimbali kukabiliana na hali hiyo kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Ongezeko la bei za mafuta ya petroli linatokana na sababu mbalimbali ikiwemo kuongezeka kwa bei katika soko la dunia. Kwa mfano baada ya msukosuko wa uchumi duniani bei ya mafuta ilishuka hadi Dola za Kimarekani 40 kwa pipa. Kwa sasa bei ya mafuta katika soko la dunia imefikia takribani Dola 120 kwa pipa ambayo ni mara tatu ya bei iliyokuwepo awali. Aidha, ongezeko la bei linachangiwa pia na kuongezeka kwa gharama za bima ya mizigo kwa meli zinazoleta mizigo nchini kutokana na tishio la maharamia baharini, uagizaji wa mafuta wa kampuni moja moja na migogoro ya kisiasa katika nchi za Mashariki ya Kati na kaskazini mwa bara la Afrika.

Pamoja na sababu zilizotajwa, bidhaa ya mafuta ya petroli inapoingia hapa nchini hutozwa ushuru wa bidhaa (*excise duty*) na ushuru wa mafuta (*fuel levy*). Zipo pia tozo mbalimbali zinazotozwa na Mamlaka zinazotoa huduma katika mfumo wa uagizaji na upokeaji wa mafuta. Taasisi zinazotoza tozo hizo ni pamoja na *EWURA*, *SUMATRA*, Shirika la Viwango la Taifa (*TBS*), Kiwanda cha *TIPER*, Mamlaka ya Mapato Tanzania, Mamlaka ya Bandari na makampuni yanayoagiza mafuta.

Pamoja na hatua zilizochukuliwa na Serikali za kuondoa Kodi ya Ongezeko la Thamani na kuweka viwango maalum vya ushuru wa bidhaa kwenye mafuta, bado bei ya mafuta imeendelea kuwa kubwa na kuongeza gharama za maisha.

Mheshimiwa Spika, zipo tozo takribani 21 ambazo zinazozwa na haya mashirika niliyoyataja kwenye kila lita ya mafuta. Serikali inakusudia kuzifuta nyingi za tozo hizo na kuzirekebisha zile ambazo zitaonekana kwamba pengine bado zinahitajika.

Hatua na kiasi gani cha tozo na kiasi gani cha pesa itakayofutwa, nitaitoa wakati nitakapowasilisha Muswada wa Fedha tarehe 22 Juni, 2011 mwezi huu. Dalili ni kwamba bei ya mafuta baada ya hatua hizo itapungua na kwa hiyo maisha kwa mwananchi yatakuwa bora zaidi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, ili kupunguza makali ya ongezeko la bei ya mafuta nchini, Serikali imeamua kufanya mapitio ya namna ya kukokotoa tozo zinazotozwa na Mamlaka mbalimbali kwa lengo la kuzipunguza na zoezi hili litakamilika katika mwaka wa fedha 2011/2012. Aidha, Serikali pia inakamilisha taratibu za ununuzi wa mafuta kwa wingi kwa lengo la kuyauzia makampuni ya usambazaji kwa bei ya jumla. Kanuni zitakazotoa mwongozo katika uagizaji mafuta kwa pamoja zimekamilika na utaratibu huu unategemewa kuanza katika mwaka wa fedha 2011/2012 katika miezi mitatu ya mwanzo kwa mwaka wa fedha ujao. Utaratibu huu unatarajiwa kupunguza bei na gharama za usafirishaji wa mafuta hayo. Pamoja na juhudhi hizi za Serikali, sekta binafsi inahimizwa kuwezesha upatikanaji wa huduma ya kutumia gesi kama nishati mbadala wa mafuta ya

petroli hasa mijini. Ni matarajio yangu kwamba hatua hizi zitaleta unafuu wa bei ya mafuta hapa nchini na hivyo kupunguza gharama za maisha kwa wananchi na kuboresha uchumi kwa ujumla.

(b) Mheshimiwa Spika, Upungufu wa Nishati ya umeme: Nchi yetu inakabiliwa na upungufu wa nishati ya umeme kutokana na kiwango kidogo cha uzalishaji usioendana na mahitaji. Kwa kuzingatia kuwa umeme una umuhimu wa kipekee katika kukuza uchumi wa nchi, Serikali itachukua hatua kadhaa za kukabiliana na upungufu huu, ikiwemo kukamilisha mradi wa kuzalisha umeme wa megawati 100 Dar-es-Salaam na ule wa megawati 60 Mwanza; kuiwezesha *TANESCO* kupata mikopo kutoka taasisi za fedha za kimataifa kwa ajili ya kununulia mitambo ya uzalishaji na kuangalia upya namna ya kugawanya shughuli za Uzalishaji, Usafirishaji na Usambazaji; kwa lengo la kuiachia *TANESCO* kujikita kwenye eneo ambalo ina uwezo nalo kiushindani na hivyo kuleta ufanisi katika sekta nzima ya umeme. Aidha, kutokana na kukamilishwa kwa sera, sheria na kanuni za ubia kati ya Serikali na sekta binafsi (*PPP*), Serikali itaandaa utaratibu wa kuhusisha sekta binafsi katika sekta ya umeme na inatarajiwa kwamba baadhi ya miradi ya uzalishaji umeme itatekelezwa kwa njia ya ubia kati ya Serikali na sekta binafsi. Serikali imeshaanza majadiliano na wawekezaji katika uzalishaji wa umeme kwa ubia katika miradi ifuatayo; Mtwara *MW 300*, Mpanga *MW 144*, na miradi ya usafirishaji umeme wa *kV 400* ya Morogoro-Tanga-Kilimanjaro-Arusha km 682 na upanuzi wa Gridi ya Kaskazini Magharibi kwa mikoa ya Kagera, Kigoma na Rukwa, takribani kilometra 1000. Miradi hii ikitekelezwa, inatarajiwa kuongeza si chini ya *MW 1000* katika Gridi ya Taifa. Serikali inawashauri wananchi kuanza kutumia vyanzo mbadala vya umeme wa jua, upopo na nishati inayotokana na biogesi pamoja na kutumia kwa uangalifu nishati ya umeme iliyopo.

(c) Mheshimiwa Spika, Kuimarisha Hifadhi ya Chakula: Kutokana na kuendelea kuwepo kwa upungufu wa chakula kulikosababishwa na ukame katika baadhi ya maeneo ya nchi, Serikali itaendelea kuimarisha hifadhi ya chakula kwa kuongeza ununuzi wa mazao ya chakula katika Wakala wa Hifadhi ya Chakula ya Serikali (*NFRA*).

Aidha, hifadhi hiyo itatumika kupunguza bei ya chakula nchini kwa kusambaza nafaka kwa bei nafuu katika masoko wakati wa uhaba. Kadhalika, wananchi wanashauriwa kuendelea kulima mazao yanayohimili ukame pamoja na kilimo cha umwagiliaji na kuzingatia kuweka akiba ya chakula cha kutosha.

(ii) Mheshimiwa Spika, Kuongeza Ajira: Ukosefu wa ajira, hasa kwa vijana umeendelea kuwa ni changamoto kubwa, hivyo, Serikali inafanya juhudzi za makusudi kupanua ajira katika maeneo mbalimbali kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Mpango wa Ukanda wa Kilimo wa Kusini mwa Tanzania (*Southern Agricultural Growth Corridor of Tanzania - SAGCOT*). Mpango huu ni mkakati wa kuleta mapinduzi ya kilimo ambaa utatekelezwa kwa ushirikiano kati ya Serikali na wadau mbalimbali wa kilimo, wakiwemo washirika wa maendeleo.

Utekelezaji wa Mpango huu ambao ni sehemu ya Kilimo Kwanza, utasaidia kupunguza umaskini mionganoni mwa wananchi wanaoishi vijijini kwa kuwaongezea mavuno ya mazao yao na kukuza ajira mionganoni mwa Watanzania. Katika mwaka 2011/12 Benki ya Dunia inatarajia kuchangia Dola za Kimarekani milioni 60 sawa na shilingi bilioni 92.8. Tunakamilisha taratibu za kupata fedha hizo na tutawasilisha Bungeni kwa ajili ya kuidhinisha matumizi yake.

Mheshimiwa Spika, Serikali pia itaendelea kufanya maboresho ya kilimo cha mazao, ufugaji na uvuvi. Kwa upande wa mazao, Tanzania ina mabonde mazuri yenye rutuba kwa kilimo cha mpunga katika mikoa ya Tabora, Mwanza, Shinyanga, Kigoma, Pwani, Mbeya, Kilimanjaro, Tanga na Morogoro.

Chini ya utaratibu huu, wakulima wadogo wadogo watawezesha kupata huduma za mikopo, ugani, mbegu bora na mbolea. Utafiti unaonesha kuwa kwa kutumia vizuri mabonde hayo, pembejeo na tija katika uzalishaji, inawezekana kutoa fursa za ajira mchanganyiko.

(b) Viwanda vyta kusindika mazao ya kilimo vitasaidia kuongeza thamani ya mazao na ajira. Aidha, eneo jingine la kuongeza ajira ni kuitia mwingiliano (*linkage*) baina ya viwanda vyta nguo na sekta ya kilimo. Juhudi zinazoendelea za kuimarisha upatikanaji wa nishati ya umeme kwa kutumia vyanzo mbadala vyta umeme wa maji na mafuta ambavyo ni upepo, juu na biogesi, zitasaidia kufanikisha mpango wa uzalishaji wa bidhaa viwandani. Kadhalika, Serikali itaboresha mazingira ya sekta ya viwanda (vikubwa, vidogo na vyta kati), ili kuviwezesha kufanya kazi kwa ufanisi zaidi.

(c) Kuongeza kasi ya utekelezaji wa MKURABITA, ili mpango huu uweze kuchangia ongezeko la ajira. Serikali kwa kushirikiana na AZAKI, AZISE na wadau wengine, itaendelea kuwawezesha wajasiriamali wadogo na wa kati (SMEs), ili kuongeza ajira.

*SIDO, VETA* na vyuo vyta maendeleo ya wananchi na vijana vitaboresha zaidi ili visaidie kutoa mafunzo ya ujasiriamali ambayo yataongeza ajira. Serikali imeweka utaratibu mzuri wa kuwawezesha waombaji wa mikopo kwa kutumia dhamana ya Serikali kuitia mifuko iliyochi chini ya Benki Kuu na kuitia benki zao za biashara kupata mikopo kwa ajili ya shughuli zao za uzalishaji. Utaratibu huu umenufaisha wajasiriamali wengi ikiwa ni pamoja na vyama vyta ushirika na sekta binafsi. (*Makofii*)

(d) Kuharakisha maboresho yanayoendelea katika sekta ya fedha na utekelezaji wa sera ya uwezesha ambazo zitasaidia upatikanaji wa mikopo kwa wananchi ili waweze kupata mitaji na kujiajiri. Hatua zinazochukuliwa na Serikali katika eneo hili ni pamoja na kuharakisha upatikanaji wa vitambulisho vyta Taifa, kuanzishwa kwa taasisi ya kuratibu taarifa sahihi za waombaji wa *mikopo* (*credit reference bureau*) ambayo itakuwa inahifadhi taarifa sahihi za wakopaji (*credit reference databank*); na mwisho, kuhamasisha mashirika ya umma, sekta binafsi na mifuko ya hifadhi ya jamii kuongeza

fursa za ajira katika maeneo yao kwa kuwekeza katika vitega uchumi na kutoa mafunzo ya kujajiri kwa vijana wasio na ajira.

Mheshimiwa Spika, ni matarajio yangu kwamba hatua hizi zitasaidia kuleta unafuu na hivyo kupunguza gharama za maisha kwa wananchi na kuboresha uchumi kwa ujumla. Serikali inaomba ushirikiano wa kila mmoja wetu ili hatua hizo zilete matokeo yanayotarajiwa.

Mheshimiwa Spika, Mapitio ya Utekelezaji wa Sera za Bajeti ya Mwaka 2010/2011, Mfumo wa Bajeti wa mwaka 2010/2011 ulizingatia Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025; Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini (MKUKUTA II); Malengo ya Maendeleo ya Milenia (*MDGs*); Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu ya Mwaka 2005; Mkakati wa Pamoja wa Misaada Tanzania (MPAMITA); na Mkakati wa Taifa wa Madeni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2010/2011, Serikali imeendelea kutekeleza majukumu yake kulingana na misingi ya sera ilizojiwekea. Sera hizo zililenga katika kuimarisha ukusanyaji wa mapato, kusimamia matumizi ya fedha za umma na uwajibikaji. Aidha, Serikali ilikusudia kuendelea kudhibiti Deni la Taifa pamoja na kuboresha mahusiano yetu na wahisani wanaosaidia Bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia sera za uchumi jumla pamoja na misingi na sera za Bajeti, katika kipindi cha mwaka 2010/2011, Serikali ilikadiria kukusanya mapato na kutumia kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo jumla ya shilingi trilioni 11.6. Kwa mwaka huo, Serikali ilipanga kukusanya mapato ya ndani ya shilingi trilioni 6.0; mapato kutoka Serikali za mitaa kiasi cha shilingi bilioni 172.6; misaada na mikopo ya kibajeti shilingi bilioni 821.6; misaada na mikopo ya miradi ya maendeleo na ya kisekta kiasi cha shilingi trilioni 2.5; mikopo ya ndani na nje shilingi trilioni 1.3; mikopo ya kulipia dhamana na hatifungani shilingi bilioni 797.6; na mapato kutokana na ubinafsishaji shilingi bilioni 30.0.

Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2010/2011, mafanikio yaliyojitokeza ni pamoja na yafuatayo:-

(i) Kiwango cha ukusanyaji wa mapato ya ndani hadi mwezi Machi, 2011 kiliongezeka kwa asilimia 21 ikilinganishwa na mapato yaliyokusanywa kipindi kama hicho mwaka 2009/2010. Aidha, katika kipindi hicho, ukusanyaji wa mapato uliongezeka kutoka wastani wa shilingi bilioni 390 kwa mwezi mwaka 2009/2010 hadi shilingi bilioni 473 mwaka 2010/2011;

(ii) Kugharamia Uchaguzi Mkuu uliofanyika mwezi Oktoba 2010 kama ilivyopangwa;

(iii) Kufanikisha ununuza tani 182,000 za chakula cha Hifadhi ya Taifa, kwa kutumia jumla ya shilingi bilioni 57, ili kukabiliana na tatizo la uhaba wa chakula lililojitekeza katika baadhi ya maeneo hapa nchini;

- (iv) Kugharamia mafunzo kwa wanafunzi 4,598 katika fani ya maafisa ugani wa kilimo na mifugo;
- (v) Serikali imeendelea kulipa madeni ya watumishi kulingana na uhakiki uliofanywa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali;
- (vi) Mishahara na stahili za watumishi ziliendelea kulipwa kwa wakati;
- (vii) Serikali imelipa kiasi cha shilingi bilioni 200 kama sehemu ya gharama kwa ajili ya ununuzi wa genereta zenyewe uwezo wa kufua umeme wa megawati 60 kwa mkoa wa Mwanza na megawati 100 kwa Mkoa wa Dar es Salaam. Aidha, Serikali imechukua hatua za dharura za kupunguza makali ya mgao wa umeme katika gridi ya Taifa kwa kugharamia ununuzi wa mafuta ya kuendesha mitambo ya kufua umeme ya *IPTL*, ambapo jumla ya shilingi bilioni 18.5 zimetumika;
- (viii) Kwa ushirikiano na Serikali ya China, Serikali iliendelea na ujenzi wa jengo maalum kwa ajili ya matibabu ya moyo katika hospitali ya Muhimbili pamoja na wodi za kulaza wagonjwa wa saratani katika hospitali ya *Ocean Road*;
- (ix) Kuongeza mtaji kwa shilingi bilioni 50 katika benki ya rasilimali (*TIB*) na hivyo kukuza mtaji hadi shilingi bilioni 92. Aidha, shilingi bilioni 20 ziliongezwa kwenye dirisha la kilimo na kufanya dirisha hilo kuwa na shilingi bilioni 42; na
- (x) Kufanikisha utoaji wa mikopo ya elimu ya juu kwa wanafunzi 96,328 ambapo jumla ya shilingi bilioni 185 zimetumika, ikilinganishwa na wanafunzi 72,035 na shilingi bilioni 145 zilizotumika kwa kipindi kama hicho mwaka 2009/2010.

Mheshimiwa Spika, mapato ya ndani, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2010/2011, Serikali ilitarajia kukusanya mapato ya ndani ya kiasi cha shilingi bilioni 6,003.6 sawa na asilimia 17.3 ya Pato la Taifa. Ili kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani, hatua mbalimbali zilizochukuliwa ni pamoja na:-

- (i) Kuendelea kuimarisha mifumo ya ukusanyaji wa mapato kwa kuhakikisha kuwa pale inapowezekana malipo yanafanyika kupitia kwenye mabenki;
- (ii) Kuweka mkakati wa kuboresha huduma za utalii kwa kutathmini hoteli ili ziwe katika viwango vinavyokubalika kimataifa kwa lengo la kuongeza mapato yanayotokana na ada;
- (iii) Kuhimiza utekelezaji wa Sheria ya Fedha Na. 13 ya mwaka 2008 na Waraka wa Hazina Na. 8 wa mwaka 2008/2009 inayoelekeza mashirika na taasisi kuchangia katika Mfuko Mkuu wa Serikali;
- (iv) Kuendelea kupanua wigo wa kodi kwa kusajili walipa kodi wapya na kuimarisha uchumi tulivu pamoja na kuweka mazingira bora ya biashara ili kuwezesha kukua kwa sekta binafsi;

(v) Kuendelea kusimamia kwa karibu mageuzi makubwa yanayoendelea ndani ya Mamlaka ya Mapato Tanzania, chini ya mpango wake wa Tatu wa Maboresho wa Miaka Mitano ambayo yamekuwa msingi wa kukua kwa ukusanyaji wa mapato ya ndani mwaka hadi mwaka;

(vi) Kuchukua hatua za kuboresha ukusanyaji wa mapato yasiyo ya kodi kutoka Wizara na Idara za Serikali;

(vii) Kupitia upya utaratibu wa kutoa misamaha ya kodi kwa lengo la kuongeza udhibiti; na

(viii) Kuendelea kuhakikisha kwamba watendaji wa Mamlaka za Serikali za Mitaa wanajengewa uwezo kwa kuwapatia utsalam wa kutosha ili kuongeza ufanisi katika ukadiriaji na ukusanyaji wa mapato katika Serikali za Mitaa. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2010/2011, Serikali ilifanya marekebisho ya Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Sura 148. Marekebisho mengi yaliyofanyika katika Sheria hii yalilenga kutoa kipaumbele katika kukuza uzalishaji kwenye sekta ya kilimo na mifugo na kuongeza mchango wake kwenye Pato la Taifa. Hivyo, marekebisho hayo yalijumuisha kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa mashine na vifaa vya kukusanya, kusafirishia na kusindika maziwa pamoja na vifungashio vya maziwa ili kuhamasisha uwekezaji katika sekta ndogo ya maziwa na hivyo kuboresha kipato cha wananchi.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilisamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye mashudu kwa ajili ya chakula cha mifugo ili kuhamasisha ufugaji bora na kuwawezesha wakulima wa mbegu za mafuta kupata bei yenyе tija kwa mauzo ya bidhaa hiyo; kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye zana za kilimo, na huduma za kuzalisha mifugo kwa njia ya kupandisha mifugo na kutumia mashine maalum za kuzalishia/kutotolea vifaranga pamoja na vifungashio vya juisi za matunda. Aidha, Serikali ilitoa unafuu maalum wa kodi ya ongezeko la thamani kwenye mabanda yanayotumika katika kilimo cha maua na kusamehe kodi ya usafirishaji wa maua kwa ndege kwenda nje ya nchi. Hatua hizi zimepelekeea kuongezeka kwa uzalishaji na usindikaji wa maziwa, uagizaji wa matanki ya kuhifadhi maziwa, upatikanaji wa zana za kilimo, pamoja na uzalishaji wa mifugo na mazao ya kilimo kwa baadhi ya maeneo nchini.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilitoa unafuu maalum wa kodi ya ongezeko la thamani kwenye uuzaaji wa bidhaa na huduma zitolewazo kwa wakulima waliosajiliwa au mashamba ya vyama vya ushirika kwa ajili ya kujenga miundombinu ya mashamba kama vile mifereji ya umwagiliaji, barabara za mashambani, ujenzi wa maghala au huduma nyinginezo za namna hiyo; na kutoza kodi ya ongezeko la thamani kwa kiwango cha asilimia sifuri kwenye usindikaji wa mafuta ya kula kwa wazalishaji wa mafuta ya kula wanaotumia mbegu za mafuta zinazozalishwa hapa nchini. Hatua hizi kwa pamoja zimesaidia kupunguza gherama za uzalishaji na kuboresha thamani ya bidhaa.

Mheshimiwa Spika, hatua hizi zimepelekeea kuongezeka kwa upatikanaji wa zana za kilimo, pamoja na uzalishaji wa mifugo na mazao ya kilimo kwa baadhi ya maeneo nchini. Takwimu za awali zinaonesha kuwa uzalishaji wa alizeti unatarajiwa kuongezeka kutoka tani 328,533 mwaka 2009/2010, hadi tani 666,030 mwaka 2010/2011; uzalishaji wa karanga kutoka 475,918 mwaka 2009/2010, hadi kufikia tani 600,300 mwaka 2010/2011; na ufuta kutoka tani 146,919 mwaka 2009/2010, hadi kufikia tani 326,660 mwaka 2010/2011. Hadi kufikia Aprili 2011, uagizaji wa vifaa vinavyotumika kuunganisha mabanda maalum yanayotumika kuzalishia maua (*green houses*) uliongezeka kutoka nyumba zenye uzito wa kilo 4,542,959 mwaka 2009/10, hadi kilo 7,181,228. Hata hivyo, matokeo ya hatua nyingine zilizochukuliwa katika kuboresha uzalishaji kwenye kilimo yatajitekeza katika muda wa kati na mrefu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2010/2011, Serikali pia ilifanya marekebisho ya Sheria ya Kodi ya Mapato, SURA 332 kwa kuweka wigo wa ukomo wa maeneo ya uchimbaji wa madini kwa nia ya kudhibiti gharama zinazotakiwa kutolewa katika kukokotoa faida itakayotozwa kodi ya mapato kuwa ni zile zinazohusika; kupunguza kiwango cha chini cha Kodi ya Mapato yanayotokana na ajira kutoka asilimia 15 hadi asilimia 14, ili kuwaongezea kipato na kuwapunguzia mzigo wa kodi watumishi wenyе kipato cha chini; na kuwataka wafanyabiashara wenyе namba za utambulisho wa mlipa kodi (*TIN*), kuzuia asilimia 2 kila wanapofanya malipo kwa wasiokuwa na namba hizo, kutokana na bidhaa au huduma walizopata kutoka kwao, ili kuwahamasisha wasiokuwa na namba kwenda kusajiliwa.

Mheshimiwa Spika, hatua hii, pamoja na juhudи nyinginezo ziliwezesha kuongeza idadi ya walipa kodi wapya ambapo hadi Machi, 2011 jumla ya walipakodi waliosajiliwa na *TIN* wamefikia 686,098, ikilinganishwa na lengo la kusajili walipa kodi 674,442 ifikapo Juni, 2011. Maboresho ya kodi ya mapato kwa sekta ya madini yanatarajiwa kuongeza mapato katika muda wa kati na mrefu.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2010/2011, Serikali ilifanya marekebisho katika Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, SURA 147 kwa kupunguza ushuru wa bidhaa kwenye mafuta mazito ya kuendeshea mitambo kutoka shilingi 97, hadi shilingi 80 kwa lita moja, ili kupunguza gharama za uzalishaji wa bidhaa nchini, katika kuzingatia dhamira ya Serikali ya kukuza viwanda, kuongeza ajira na mapato ya ndani. Aidha, katika kipindi hicho, Serikali ilifanya marekebisho ya Sheria ya Magari SURA 124 pamoja na Sheria ya Usalama Barabarani, SURA 168 kwa kupandisha ada ya usajili, uhamisho wa umiliki na ada ya mwaka ya leseni za magari ili kuongeza mapato.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia matakwa ya Itifaki ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, mwaka 2010/2011 Mawaziri wa Fedha wa Nchi wanachama waliridhia kufanya marekebisho mbalimbali katika Sheria ya Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya mwaka 2004 ili kuboresha sekta za viwanda, kilimo na usafirishaji kama vichocheo muhimu katika kukuza uchumi wa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai 2010 hadi Machi 2011 mapato ya ndani, yakijumuisha mapato ya Serikali za Mitaa, yalifikia shilingi bilioni 4,256.3, sawa na asilimia 69 ya lengo la bajeti ya mwaka 2010/2011 la shilingi bilioni 6,176.2. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 3,910.6 ni mapato ya kodi, shilingi bilioni 227.4 ni mapato yasiyo ya kodi na mapato ya Serikali za Mitaa yalikuwa shilingi bilioni 118.2.

Mheshimiwa Spika, mapato halisi ya ushuru wa forodha yalikuwa shilingi bilioni 343.2, sawa na asilimia 70 ya lengo la mwaka la kukusanya shilingi bilioni 493.1. Mapato kutokana na ushuru wa bidhaa kutoka nje yalifikia shilingi bilioni 455.0, sawa na asilimia 73 ya bajeti ya shilingi bilioni 622.8, wakati shilingi bilioni 258.7, zilikusanywa kutokana na ushuru wa bidhaa zilizozalishwa nchini, ikilinganishwa na bajeti ya shilingi bilioni 404.2, sawa na asilimia 64.

Aidha, mapato kutokana na Kodi ya Ongezeko la Thamani kutoka nje yalifikia shilingi bilioni 664.6, ikilinganishwa na bajeti ya shilingi bilioni 999.3, sawa na asilimia 67, wakati shilingi bilioni 611.2 zilikusanywa kutokana na Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa mauzo ya ndani, ikilinganishwa na bajeti ya shilingi bilioni 992.3 sawa na asilimia 62. Makusanyo halisi yanayotokana na Kodi ya Mapato yalikuwa shilingi bilioni 1,255.8, ikiwa ni asilimia 74 ya bajeti ya shilingi bilioni 1,702.3. Aidha, mapato halisi yatokanayo na vyanzo vingine vya kodi yalikuwa shilingi bilioni 449.7, ikiwa ni asilimia 72 ya bajeti ya shilingi bilioni 620.9.

Mheshimiwa Spika, mapato yasiyo ya kodi kwa kipindi cha Julai 2010 hadi Machi 2011, yalikuwa shilingi bilioni 227.4, ikilinganishwa na bajeti ya shilingi bilioni 365.0, sawa na asilimia 62. Aidha, mapato ya Serikali za Mitaa yalikuwa shilingi bilioni 118.2, sawa na asilimia 68 ya bajeti ya shilingi bilioni 172.6.

Mheshimiwa Spika, Mikopo ya Ndani. Katika mwaka 2010/2011, Serikali ilipanga kukopa shilingi bilioni 1,397.6, kutoka vyanzo vya ndani ili kugharamia bajeti yake. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 600.0 ni kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo na shilingi bilioni 797.6 ni kwa ajili ya kulipia hatifungani zitakazoiva. Hadi Machi 2011, kiasi cha shilingi bilioni 1,107.5 kilikopwa kwa ajili hiyo. Kiasi hiki kinajumuisha dhamana za Serikali zenye thamani ya shilingi bilioni 607.6 zilizouzwa katika soko ili kulipia zilizoiva na shilingi bilioni 499.9 zilitumika kugharamia miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada ya mwaka 1974 (kama ilivyorekebishwa mwaka 2004) na Kanuni zake, imeendelea kuwa msingi na nguzo kuu ya ukopaji mikopo, utoaji dhamana na kupokea misaada ikiwemo misamaha na unafuu wa madeni.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai 2010 hadi Machi 2011, misaada na mikopo ya kibajeti ilikuwa shilingi bilioni 845.7, sawa na asilimia 103 ya makadirio. Ongezeko hili limetokana na nchi ya Canada kuongeza mchango wake wa misaada ya kibajeti mara mbili ya makadirio ya awali.

Misaada na mikopo kwa ajili ya miradi ya maendeleo, ikijumuisha mifuko ya kisekta ilifikia shilingi bilioni 1,427.6, sawa na asilimia 58 ya makadirio. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Tathmini ya uwezo wa Nchi Kukopa na Kulipa Madeni (*Sovereign Credit Rating*). Kufuatia kuanza kutengemaa kwa uchumi wa dunia baada msukosuko wa kiuchumi duniani na nia ya Serikali ya kuboresha upatikanaji wa taarifa zilizohakikiwa kuhusu mwenendo mzuri wa Taifa kiuchumi, kisasa, na utawala bora, Serikali inaendelea kumtafuta Mshauri Mwelekezi wa Kimataifa kwa ajili ya kusimamia zoezi la kutathmini uwezo wa Nchi wa kukopa na kulipa madeni (*Sovereign Credit Rating*).

Mambo muhimu yanayozingatiwa katika tathmini hii ni pamoja na; hali ya utulivu wa kisasa; kasi ya kukua kwa uchumi; udhibiti wa usimamizi wa bajeti ya Serikali; udhibiti wa masoko ya fedha na hali ya mfumuko wa bei; na urari wa malipo ya nje ya nchi.

Hatua hii itasaidia kuwavutia wawekezaji na wakopeshaji kutohana na kuwepo kwa taarifa ya hali ya uchumi, siasa na utawala wa nchi na hivyo kurahisisha upatikanaji wa mikopo nafuu kutoka nje ya nchi kwa Serikali na kwa sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, Deni la Taifa. Mwaka 2000/2001 Deni la Taifa, lilikuwa Dola za Kimarekani bilioni 8.55 ikilinganishwa na Dola bilioni 10.01.

Mwaka 2005/2006na kupungua mwaka 2006/2007 hadi kufikia Dola bilioni 7.53. Kupungua kwa deni hilo kilitokana na misamaha mbalimbali ya madeni kutoka nchi wahisani na mashirika ya fedha ya kimataifa chini ya utaratibu wa (*HIPC na MDRI*). Aidha, Deni la Taifa liliongezeka hadi kufikia Dola bilioni 10.54 mwaka 2009/2010, kutoka Dola bilioni 9.36 mwaka 2008/2009.

Kati ya Deni la mwaka 2009/2010, Dola bilioni 5.99 ni deni la nje na Dola bilioni 4.55 ni deni la ndani, ikijumuisha Dola bilioni 1.63 za dhamana za Serikali kwa miradi ya Wizara, Idara na Taasisi za Serikali.

Mheshimiwa Spika, Utegemezi wa Bajeti. Pamoja na mafanikio niliyoyaeleza kwenye mwenendo wa mapato hapo juu, Bajeti ya Serikali imekuwa ikitegemea misaada ya wahisani, ambayo hivi sasa (2010/2011) ni asilimia 17 ya Bajeti kutoka asilimia 28 mwaka 2007/2008. Hii ni dalili kwamba utegemezi unapungua. Kwa kuzingatia umuhimu wa Taifa kujitegemea kifikra na kirasilimali katika kuleta maendeleo, Serikali imeamua kuchukua hatua madhubuti za kuongeza mapato ya ndani, ikiwa ni pamoja na kupanua wigo, kuongeza ufanisi katika ukusanyaji na kutambua walipa kodi wapya; na kudhibiti matumizi ili ifikapo mwaka 2015, kiwango cha utegemezi wa misaada ya wahisani kwenye Bajeti ya Serikali kisizidi asilimia 10. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Matumizi. Katika mwaka wa fedha 2010/11, sera za matumizi ya Serikali zililenga katika kuboresha usimamizi na udhibiti wa matumizi ya

fedha za umma ili kuongeza ufanisi pamoja na kutoa kipaumbele kwa maeneo muhimu ya kiuchumi yanayochochea kasi ya ukuaji wa uchumi na kupunguza umaskini, hususan wa kipato.

Katika kipindi cha Julai 2010 hadi Machi, 2011, jumla ya matumizi ilikuwa shilingi bilioni 7,169.3, sawa na asilimia 67 ya Makadirio ya mwaka. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 5,226.9 ni Matumizi ya Kawaida na shilingi bilioni 1,942.4 ni Matumizi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, hadi Machi 2011, malipo ya mishahara ya watumishi wa Serikali yalikuwa shilingi bilioni 1,749.1, sawa na asilimia 79 ya Makadirio ya mwaka. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 569.96 zilitolewa kwa ajili ya Wizara na Idara zinazojitegemea, shilingi bilioni 52.9 kwa ajili ya Sekretarieti za Mikoa na shilingi bilioni 1,126.2 kwa ajili ya Halmashauri. Aidha, jumla ya shilingi bilioni 443.9 zililipwa kwa ajili ya mishahara ya taasisi na Mashirika ya Umma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa kipindi cha Julai, 2010 hadi Machi, 2011 malipo ya riba kwa madeni ya ndani yalifikia shilingi bilioni 173.6, sawa na 74% ya makadirio ya mwaka. Aidha, kiasi cha shilingi bilioni 44.6 kilitumika kulipia riba kwa madeni ya nje, sawa na asilimia 34 ya makadiro ya mwaka. Kwa upande wa madeni mengine (*CFS Others*), jumla ya shilingi bilioni 361.3 zilitumika ikiwa ni asilimia 66 ya makadirio ya mwaka na kiasi cha shilingi bilioni 1,955.3 kilitumika kugharamia matumizi mengineyo. Kwa ujumla, matumizi yalifanyika kulingana na upatikanaji wa mapato.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai 2010 hadi Machi 2011, matumizi kwa ajili ya miradi ya maendeleo yalifikia jumla ya shilingi bilioni 1,942.4, ambapo shilingi bilioni 514.8 ni fedha za ndani na shilingi bilioni 1,427.6 ni fedha za nje, ikinganishwa na lengo la mwaka mzima la kutumia shilingi bilioni 1,366.1 na bilioni 2,452.9, kwa mtiririko huo.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua umuhimu wa vitambulisho vya Taifa, Serikali imekamilisha taratibu za kumpata mzabuni na tayari mkataba umekwishesainiwa. Mradi huu utagharimu jumla ya shilingi bilioni 355 mpaka utakapokamilika. Kwa mwaka 2011/12, jumla ya shilingi bilioni 70 zitatumika kama ilivyopangwa. Awamu ya kwanza ya uzalishaji wa vitambulisho hivyo itakamilika mwishoni mwa mwaka 2011. Mradi huu ukikamilika utawezesha wananchi kuwa na utambulisho na hivyo kusaidia, pamoja na mambo mengine, kuongeza wigo wa ulipaji kodi, kurahisisha upatikanaji wa huduma mbalimbali, ikiwa ni pamoja na huduma za kifedha, na kuwatambua wahamiaji haramu.

Mheshimiwa Spika, Masuala yanayoihusu Serikali za Mitaa. Katika mwaka 2010/2011, Serikali Kuu imeendelea kuzipa uwezo Serikali za mitaa wa kusimamia rasilimali watu na fedha ili ziweze kutoa huduma kwa wananchi kwa ufanisi. Aidha, Serikali imeendelea kuzipatia fedha, watumishi na vitendea kazi na ushauri wa kitaalamu kulingana na maeneo yaliyoainishwa kwenye Bajeti.

Hadi kufikia Machi, 2011, Serikali za Mitaa zilikuwa zimepokea jumla ya shilingi bilioni 1,358.6, sawa na asilimia 90 ya lengo la shilingi bilioni 1,504.7 zilizotarajiwaa kupelekwa kwa kipindi hicho. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mapato ya ndani, Serikali za mitaa, zimeendelea kukusanya mapato kutoka katika vyanzo mbalimbali kwa mujibu wa sheria ya fedha ya Serikali za Mitaa Sura namba 290. Katika mwaka wa fedha 2010/2011, mapato kutoka halmashauri yalikadiriwa kuwa shilingi bilioni 172.6. Hadi kufikia mwezi Machi, 2011, mapato halisi yaliyokusanywa kwenye Halmashauri yalifikia jumla ya shilingi bilioni 118.2, ambayo, ni sawa na asilimia 68 ya bajeti. Aidha, Serikali imetekeleza majukumu mengi ikiwa ni pamoja na:-

- (i) Kulipa kiasi cha shilingi bilioni 10.5 kwa ajili ya madeni ya watumishi wa Serikali za Mitaa wasio Walimu, kulingana na uhakiki uliofanywa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali;
- (ii) Ujenzi wa hospitali 3 za mikoa ya Manyara, Singida na Mbeya, pamoja na ukarabati wa hospitali 10 za Mikoa na 17 za Wilaya;
- (iii) Ujenzi wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Dodoma, nyumba 3 za wakuu wa mikoa, ofisi 22 za Halmashauri na nyumba 210 katika Halmashauri mbalimbali;
- (iv) Ukarabati wa ofisi 17 za Wakuu wa Mikoa, ofisi 26 pamoja na nyumba 23 za Wakuu wa Wilaya; na
- (v) Kuboreshwa na kusambazwa kwa Mfumo wa IFMIS (*Integrated Financial Management Information System*) kwenye ngazi ya Halmashauri ili kuimarisha uwajibikaji, ufuatiliaji na tathmini ya matumizi ya fedha za umma.

Mheshimiwa Spika, Usimamizi wa Fedha za Umma. Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka 2009/10, inaonesha kutetereka kwa udhibiti na usimamizi wa fedha za umma katika Wizara, Idara na Sekretarieti za Mikoa, ikilinganishwa na taarifa ya mwaka 2008/09. Taarifa inaonesha kupungua kwa Hati safi za ukaguzi zilizotolewa kwa Wizara na Idara za Serikali, kutoka asilimia 87 hadi asilimia 77, wakati hati zenyenye shaka zimeongezeka kutoka asilimia 10 hadi asilimia 20. Aidha, kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa, hati safi za ukaguzi zimebungua kutoka asilimia 58 mwaka 2008/2009, hadi 48.5 mwaka 2009/2010, wakati hati zenyenye mashaka zimeongezeka kutoka asilimia 41 hadi asilimia 48.5.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya sababu za kupungua kwa hati safi za ukaguzi ni kutofuatwa kikamilifu kwa Viwango vya Kimataifa vya utoaji wa taarifa za kihasibu katika Sekta ya Umma (IPSAS), Sheria ya Ununuzi ya Umma ya mwaka 2004 na kanuni zake za mwaka 2005, kukosekana kwa usimamizi na ufuatiliaji wa karibu katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo, kutozingatiwa kwa mfumo wa udhibiti wa ndani, ukosefu wa mafunzo endelevu kwa watumiaji wa mfumo wa *IFMIS* kwenye Serikali za Mitaa na kutotekelezwa kwa mapendekezo ya ukaguzi kwa miaka iliyopita.

Katika kuimarisha usimamizi na udhibiti wa fedha za umma, Sheria ya Fedha za Umma Sura namba 348 imepitiwa na kurekebishwa ili kuwapatia Mlipaji Mkuu wa Serikali na Mhasibu Mkuu wa Serikali mamlaka ya kusimamia na kufuatilia usimamizi wa fedha za umma katika ngazi ya Serikali za Mitaa. Kupitia marekebisho haya, Serikali imeunda nafasi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali Msaidizi atakayeshughulikia usimamizi wa fedha katika Serikali za Mitaa, na hivyo kuwezesha utekelezaji wa dhima ambayo imekusudiwa na mabadiliko haya.

Mheshimiwa Spika, Usimamizi wa Mashirika ya Umma. Katika miaka ya hivi karibuni, zimejitokeza changamoto nyingi katika kusimamia wakala, taasisi na mashirika ya umma. Baadhi ya mashirika na taasisi za umma zinazotakiwa kuijendesha kibiashara zimeshindwa kuijendesha kwa ufanisi na kuwa mzigo mkubwa kwa kutegemea ruzuku kutoka Serikali Kuu, kinyume na lengo la kuanzisha mashirika na taasisi hizo.

Mheshimiwa Spika, kutokana na changamoto hizo, Serikali imefanya mabadiliko katika muundo wa Wizara ya Fedha kwa kuifanya Ofisi ya Msajili wa Hazina kuwa wakala anayejitegemea, kwa lengo la kuzisimamia kwa karibu wakala, taasisi na mashirika ya umma na hivyo kuongeza ufanisi, tija, mapato na kupunguza utegemezi wa ruzuku kutoka Serikali Kuu. Serikali inapitia sheria zilizoanzisha mashirika na taasisi mbalimbali na sheria nyinginezo zinazohusiana na Ofisi ya Msajili wa Hazina, ili kuondoa muingiliano wa kiutendaji.

Mheshimiwa Spika, Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini (MKUKUTA II). Serikali ilikamilisha maandalizi ya MKUKUTA Awamu ya Pili (MKUKUTA II) na kuanza kutekeleza mnamo Julai 2010. Kama nilivyojulisha Bunge lako Tukufu katika kikao cha Bajeti mwaka 2010/2011, MKUKUTA II ni nyenzo kuu ya kuliwezesha Taifa kufikia Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025 na Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi.

Serikali inaendelea kutenga fedha kwa ajili ya kugharimia MKUKUTA II hasa kwa vipaumbele vinavyogusa wananchi walio wengi na kuboresha huduma za jamii. Ugharamiaji wa Mkakati huu unategemea bajeti ya Serikali, michango ya jamii na sekta binafsi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, MKUKUTA II umejikita katika maeneo muhimu yafuatayo:-

- (i) Miundombinu hususan, barabara za vijijini, reli, bandari, viwanja vya ndege, nishati ya umeme na miundombinu ya mawasiliano na habari pamoja na usafirishaji wa nishati ya mafuta na gesi;
- (ii) Sekta ya Kilimo ikiwa ni pamoja na maendeleo ya Mifugo na Uvuvu;
- (iii) Sekta ya Viwanda, lengo likiwa kuendeleza viwanda vitakavyotumia rasilimali za ndani; na

(iv) Dhana ya ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi, kwa maana ya kupanua na kuimarisha ushiriki na mchango wa sekta binafsi katika maeneo ya miundombinu, uzalishaji wa mazao ya chakula, biashara pamoja na utoaji wa huduma za jamii kama vile afya, usafirishaji, elimu na mafunzo na huduma za kifedha.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Pamoja ya Fedha. Tume ya Pamoja ya Fedha ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, iliundwa kwa mujibu wa Ibara ya 134 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Sheria ya Tume ya Pamoja ya Fedha SURA 140. Tume imetoa taarifa kadhaa na mapendekezo ikiwemo taarifa iliyotolewa mwaka 2006, kuhusu vigezo vya kugawana mapato na kuchangia gharama za Muungano.

Taarifa hiyo imefanyiwa mapitio mwaka 2010, ili kuiboresha na imewasilishwa kwa Wizara ya Fedha ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar mwezi April 2011. Kila upande unaendelea kufanya uchambuzi wa mapendekezo ya Tume na utawasilisha maoni yake katika kikao cha pamoja, chini ya uenyekiti wa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mapema mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Spika, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi. Katika mwaka 2010/2011, Serikali iliendelea kutekeleza Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi, kwa kutoa mikopo yenye masharti nafuu kupitia mifuko na *program* mbalimbali; kuhamasisha uanzishwaji wa vyama vya ushirika (*SACCOS*) na *VICOBA* kama njia bora ya kupata mikopo yenye masharti nafuu, kuongeza kipato, ajira na kupunguza umaskini. Matokeo ya uhamasishaji huo ni kuongezeka kwa vyama hivyo mara tatu kutoka 1,875 mwaka 2005 hadi 5,344 mwaka 2010, na kuongezeka kwa idadi ya wanachama wa vyama hivyo kutoka 1,360,850 hadi 2,100,000. Akiba na amana za wanachama zimeongezeka zaidi ya mara tano, kutoka shilingi bilioni 31.4 mwaka 2005, hadi shilingi bilioni 174.6 mwaka 2010. Aidha, Serikali imekamilisha Mwongozo wa Ufutiliaji na Tathmini ya Mkakati wa Utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi. Vile vile, maandalizi ya Mwongozo wa Kitaifa wa Kutoa Mafunzo ya Ujasiriamali yanaendelea.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2011/2012, Serikali itaendelea kutekeleza Sera ya Taifa ya Uwezeshaji wa Wananchi Kiuchumi, kwa kuieneza ili wananchi wengi waielewe na kushiriki kikamilifu katika utekelezaji wake; kutoa mafunzo kwa wajasiriamali; kuhamasisha uwekaji akiba, uwekezaji na kuhamasisha uanzishwaji wa vyama vya ushirika; na kufanya tafiti zenye lengo la kuendeleza stadi za ujasiriamali na kuanzisha na kuboresha shughuli za kiuchumi. Serikali itaendelea pia kuhamasisha ushiriki wa wananchi katika shughuli za maendeleo kupitia utaratibu unaosimamiwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii, yaani *TASAF*.

Mheshimiwa Spika, Mwelekeo wa Bajeti ya Mwaka 2010/2011 hadi Juni, 2011. Kulingana na mwenendo wa makusanyo ya mapato kwa kipindi cha miezi tisa ya mwaka 2010/2011, inategemewa kwamba hadi kufikia Juni, 2011 Serikali itaweza kukusanya jumla ya shilingi bilioni 5,553.7, sawa na asilimia 93 ya lengo la shilingi bilioni 6,003.6.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mikopo na misaada ya kibajeti, hadi kufikia Juni 2011, kiasi cha shilingi bilioni 927.9 zinakadiriwa kupatikana, ikilinganishwa na shilingi bilioni 821.6 zilizokadiriwa hapo awali sawa na ongezeko la asilimia 13. Mwelekeo unaonesha kwamba, hadi kufikia Juni 2011 sehemu kubwa ya fedha zilizokadiriwa kupatikana kutokana na misaada na mikopo kwa ajili ya miradi ya maendeleo zitapatikana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa matumizi, Serikali imeendelea kutoa fedha kulingana na upatikanaji wa mapato na kwa kuzingatia vipaumbele viliwyopangwa. Mwelekeo ni kwamba matumizi yatakuwa chini ya lengo la bajeti ya mwaka 2010/2011 kutokana na upungufu wa mapato. Aidha, kabla ya mwisho wa mwaka 2010/2011, Serikali italipa madeni yaliyohakikiwa ya vyombo vya dola ikiwa ni pamoja na posho za nyumba kwa Wahadhiri wa vyuo vikuu vya umma na pango la nyumba kwa Waheshimiwa Majaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Msingi na Shabaha za Bajeti kwa mwaka 2011/2012. Bajeti ya Mwaka 2011/2012 inazingatia maeneo muhimu ya utekelezaji ili kufikia malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, Awamu ya Pili ya Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini (MKUKUTA II); Malengo ya Maendeleo ya Milenia 2015; Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010-2015; Mkakati wa Pamoja wa Misaada Tanzania (MPAMITA) na Mkakati wa Taifa wa Madeni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, maeneo muhimu yatakayozingatiwa katika utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2011/2012 ni kama ifuatavyo:

- (i) Kukabiliana na changamoto za kupunguza makali ya maisha kwa wananchi kama nilivyoeleza hapo awali;
- (ii) Kuendelea kuboresha mfumo wa makusanyo ya mapato ya ndani, kuboresha mazingira ili kuvutia wawekezaji wa ndani na nje na uendelezaji wa sekta binafsi ili kupanua wigo na kuongeza vyanzo vipyta vya mapato;
- (iii) Kuendelea na utekelezaji wa mradi wa Vitambulisho vya Taifa; uanzishwaji wa anuani za makazi na utekelezaji wa MKURABITA;
- (iv) Kuhakikisha kwamba maduhuli ya Serikali yanakusanywa ipasavyo na kuwasilishwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali;
- (v) Kutenga rasilimali katika maeneo ya kuongeza kasi ya ukuaji uchumi kama vile miundombinu ya umeme, maji, barabara, bandari, kilimo, umwagiliaji, pamoja na TEHAMA;
- (vi) Kuimarisha utawala bora na uwajibikaji;

- (vii) Kuendelea kutekeleza mipango na mikakati maalum ya kuharakisha ukuaji wa uchumi, kama vile kuvutia wawekezaji kwenye miradi ya uzalishaji kwa ajili ya kuuza nje (*EPZ*) na wa uanzishaji wa maeneo maalum ya uwekezaji (*SEZs*);
- (viii) Kukamilisha uandaaji wa awamu ya nne ya programu ya maboresho ya usimamizi wa fedha za umma (*PFMRP IV*);
- (ix) Kuimarisha uandaaji na utekelezaji wa sera za fedha ziendane na zile za mapato na matumizi ili kupunguza mfumuko wa bei na ongezeko la riba pamoja na kuongeza mikopo kwa sekta binafsi na kuhakikisha uhimilivu katika deni la Taifa;
- (x) Kuimarisha urari wa malipo kwa kusindika bidhaa kabla ya kusafirishwa nje, hasa mazao ya kilimo, madini na bidhaa nyingine;
- (xi) Kutafuta mikopo ya masharti nafuu na ya kibashara kutoka benki mbalimbali ili kuongeza uwezo wa Serikali kugharamia miradi mikubwa ya maendeleo;
- (xii) Kuharakisha utekelezaji wa Sheria ya Ubia kati ya Sekta ya Umma na ya Binafsi ili kupanua fursa za utekelezaji wa miradi ya maendeleo;
- (xiii) Kuendelea kutenga fedha kwa ajili ya Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2012; na
- (xiv) Kulinda na kudumisha mafanikio yaliyopatikana katika Sekta za huduma za jamii (Elimu, Maji na Afya).

Mheshimiwa Spika, Sera za Mapato. Katika mwaka 2011/2012, Sera za mapato zinalenga kukusanya mapato ya ndani, yasiyopungua shilingi bilioni 6,775.9, sawa na asilimia 17.2 ya Pato la Taifa, ikilinganishwa na matarajio ya kukusanya shilingi bilioni 5,553.7 au asilimia 16.0 ya Pato la Taifa kwa mwaka 2010/2011.

Kati ya kiwango hicho, mapato ya kodi ni shilingi bilioni 6,228.8, mapato yasiyo ya kodi ni shilingi bilioni 547.1 na mapato kutokana na vyanzo vya Halmashauri ni shilingi bilioni 350.5.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani kwa kuchukua hatua mbalimbali za kiutowala kwa kuhusisha maeneo ya mapato ya kodi na yasiyo ya kodi, pamoja na kupanua wigo wa mapato katika maeneo mengine. Maeneo ya kisera yatakayozingatiwa ili kuongeza mapato ni pamoja na: -

- (i) Kuimarisha utaalamu na mbinu za kuhakiki kodi kutoka kwenye kumbukumbu za biashara (*audit capacity*); kuimarisha mfumo wa utawala wa kodi kwa kutumia vitalu (*Block Management System*); kuingiza sekta isiyo rasmi kwenye mfumo wa kodi; kutekeleza utawala wa kodi kwa kutumia mfumo wa viashiria hatarishi (*Enterprise wide Risk Management*); na kudhibiti mbinu zote za ukwepaji Kodi;

- (ii) Kuhuisha Sheria mbalimbali zinazoruhusu misamaha ya kodi kwa nia ya kudhibiti misamaha hiyo. Kwa sasa misamaha hiyo ni asilimia 2.5 ya Pato la Taifa na lengo ni kufikia angalau asilimia 1 ya Pato la Taifa katika muda wa kati; (*Makofi*)
- (iii) Kuendelea kuimarisha mifumo ya ukusanyaji wa mapato kwa kuhakikisha kuwa malipo yanafanyika kupitia benki; na kuanza kutumia mfumo wa kulipa kodi kwa kutumia mfumo wa M-PESA kwa malipo ya Kodi yasiyozidi shilingi 500,000 ili kuondoa kero ya walipa kodi kukaa kwenye mistari;
- (iv) Kuimarisha TEHAMA katika utawala wa kodi – hasa katika utozaji kodi kwenye sekta za Mawasiliano na Fedha, ukaguzi wa kina (*Forensic Audit*), na utunzaji na uchambuzi wa takwimu;
- (v) Kuendelea kuimarisha matumizi na udhibiti wa Mashine za Elektroniki za kutoa stakabadhi za kodi (*Electronic Fiscal Devices-EFDs*) na kutoa elimu kwa walipakodi na wafanya biashara kuhusu matumizi ya mashine hizi;
- (vi) Kusimamia Mpango wa tatu wa Miaka Mitano wa Maboresho ya utendaji wa Mamlaka ya Mapato Tanzania kwa lengo la kuongeza ufanisi zaidi katika kukusanya mapato;
- (vii) Kuboresha Mifumo ya Ukusanyaji na Usimamiaji kwa Mapato yasiyo ya Kodi kwa kupitia upya mfumo wa utoaji stakabadhi na leseni, pamoja na kuboresha viwango vya kubakiza maduhuli (*retention*) kwa Wizara, Idara na Taasisi za Serikali;
- (viii) Kupitia upya mfumo wa ukusanyaji wa kodi ya majengo (*Property tax*) katika majiji, manipaa, miji, wilaya na miji midogo na kuboresha mfumo wa ukusanyaji wake, kwa kutumia taarifa mpya za thamani za majengo hayo na kusimamia ulipaji wa kodi hiyo, ikiwa ni pamoja na kupitia upya vyanzo vya mapato na mfumo wa ukusanyaji katika Serikali za Mitaa;
- (ix) kuendelea kuimarisha uchumi tulivu na kuweka mazingira bora ya biashara ili kuwezesha sekta binafsi kukua na hatimaye kuweza kuchangia katika mapato;
- (x) Kuimarisha miundombinu ya bandari, reli na barabara ili kuchochea biashara na hatimaye kuongeza mapato; na
- (xi) kuimarisha usimamizi na udhibiti wa bidhaa zipitazo katika bandari zetu kwenda nchi za jirani, hasa bidhaa za mafuta, ili kuzuia uvujaji wa mapato ya serikali.

Mheshimiwa Spika, Misaada ya Mikopo. Katika Bajeti ya mwaka 2011/2012, Serikali inatarajia kupokea jumla ya misaada na mikopo yenyne masharti nafuu kiasi cha shilingi bilioni 3,923.6, ikilinganishwa na kiasi cha shilingi bilioni 3,274.6 kwa mwaka 2010/2011. Hili ni ongezeko la shilingi bilioni 648.99, sawa na asilimia 20, ukilinganisha na kiwango cha mwaka 2010/2011. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 869.4 ni misaada na mikopo ya kibajeti na shilingi bilioni 3,054.1 ni misaada na mikopo kwa ajili ya miradi ya maendeleo ikijumuisha mifuko ya kisekta.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwatambua na kuwashukuru washirika wetu wa maendeleo ambao wameendelea kutoa misaada na mikopo kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu licha ya nchi zao kuathirika na msukosuko wa uchumi Duniani. Wahisani hao ni: Uingereza, Denmark, Uholanzi, Ubelgiji, Canada, China, Finland, Ufaransa, Ujeruman, Ireland, Italia, Japani, Korea ya Kusini, Norway, Sweden, Uswisi, Marekani, India, Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika, *BADEA*, Umoja wa Ulaya, *Global Fund*, Shirika la Fedha la Kimataifa (*IMF*), Kuwait Fund, *Nordic Fund*, *Opec Fund*, *Saudi Fund* na Mashirika ya Umoja wa Mataifa. Wote tunawashukuru sana kwa michango yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mikopo ya Kibiashara. Kiwango cha mikopo yenye masharti ya kibiashara kinazingatia tathmini ya uhimilivu wa deni la Taifa, ambapo kiasi cha Dola za Kimarekani milioni 1,500 zinakadirwa kukopwa kwa muda wa miaka mitatu, 2010/2011 – 2012/2013. Hivyo, Dola za Kimarekani milioni 822, sawa na shilingi bilioni 1,271.6. zinatarajiwa kutumika mwaka 2011/2012. Kati ya kiasi hiki, Dola milioni 297 sawa na shilingi bilioni 459 ni albaki ya mikopo iliyotarajiwa mwaka 2010/2011 na Dola milioni 525, sawa na shilingi bilioni 812 zinatarajiwa kupatikana mwaka 2011/2012. Fedha hizi zitatumika kwa miradi ya maendeleo ikijumuisha miradi ya miundombinu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mikopo ya Ndani. Katika mwaka 2011/2012, Serikali inakusudia kukopa kiasi cha shilingi bilioni 1,204.3 katika soko la fedha la ndani. Kati ya kiasi hiki, shilingi bilioni 393.4 kwa ajili ya kuziba nakisi ya mapato ya Serikali na kiasi cha shilingi bilioni 810.9 ni kwa ajili ya kulipia dhamana zinazoiva.

Mheshimiwa Spika, sera za matumizi ya Serikali zinalenga katika kuboresha usimamizi na udhibiti wa matumizi ya fedha za umma, yakijumuisha udhibiti wa ulipaji wa mishahara, matumizi katika miradi ya maendeleo, ruzuku ya pembejeo, ununuzi wa umma na kuendelea kudhibiti ulimbikizaji wa madeni. Msisitizo utawekwa kwenye kutekeleza maeneo yaliyoainishwa kwenye misingi na shabaha za bajeti ya mwaka 2011/2012, ili kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi na kupunguza umasikini.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia maeneo ya kipaumbele niliyoyaainisha katika aya ya 9, mchanganuo wa bajeti kwa baadhi ya sekta kwa mwaka 2011/2012 ni kama ifuatavyo:-

- (i) Miundombinu ya barabara, reli, bandari na Mkongo wa Taifa zimetengewa shilingi bilioni 2,781.4 ikilinganishwa na shilingi bilioni 1,505.1 mwaka 2010/2011 sawa na ongezeko la asilimia 85;
- (ii) Nishati na madini imetengewa shilingi bilioni 539.3 ikilinganishwa na shilingi bilioni 327.2 mwaka 2010/2011, sawa na ongezeko la asilimia 65;

- (iii) Maji imetengewa shilingi bilioni 621.6 ikilinganishwa na shilingi bilioni 397.6 mwaka 2010/2011, sawa na ongezeko la asilimia 56; (*Makofi*)
- (iv) Kilimo na umwagiliaji kimetengewa shilingi bilioni 926.2 ikilinganishwa na shilingi bilioni 903.8 mwaka 2010/2011, sawa na ongezeko la asilimia 2.5;
- (v) Elimu imetengewa shilingi bilioni 2,283.0 ikilinganishwa na shilingi bilioni 2,045.4 mwaka 2010/2011, sawa na ongezeko la asilimia 12; na
- (vi) Afya imetengewa shilingi bilioni 1,209.1 ikilinganishwa na shilingi bilioni 1,205.9 mwaka 2010/2011, sawa na ongezeko la asilimia 0.3.

Mheshimiwa Spika, Kudhibiti Matumizi. Serikali itahakikisha kwamba taratibu za kifedha na ununuzi wa umma zinafuatwa kikamilifu pamoja na kuondokana na matumizi yasiyokuwa ya lazima:-

- (a) Katika mwaka wa fedha wa 2011/2012, Serikali itaendelea kuchukua hatua mbalimbali za udhibiti wa matumizi, ikiwa ni pamoja na kuimarisha ukaguzi wa mishahara, (*Payroll Audit*) ambapo Maafisa Masuuli watafanya ukaguzi wa malipo ya mishahara ya asasi/taasisi zao kila mwezi. Chini ya utaratibu huu wakuu wa Idara watawajibika pia kufanya ukaguzi wa mishahara ili kuhakikisha kuwa watumishi wanaolipwa mishahara ni wale walio chini yao. Wakuu wa Idara na Maafisa Wahasibu watawajibika kwa malipo ya mishahara hewa. Aidha, Serikali itaendesha ukaguzi wa mara kwa mara kwa malipo ya mishahara kupitia Idara ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Serikali na pia kupitia Sehemu ya Ufuatilaji wa Matumizi ya Serikali na Utendaji Kazi katika Idara ya Bajeti ya Serikali. (*Makofi*)

Katika mwaka 2011/2012, Serikali imepanga kufanya sensa ya watumishi wote wa Serikali na Taasisi kwa kuandaa siku maalum ya malipo ya mshahara dirishani “*National Pay Day*” siku hii itakuwa ya mshitukizo hawataarifiwa. Aidha, Serikali itasimamia utekelezaji wa Waraka Na. 2 wa Hazina wa mwaka 2010 kuhusu uwajibikaji na udhibiti katika usimamizi wa malipo ya mishahara pamoja na ukamilishaji wa maboresho ya mfumo wa kuandaa mishahara (*Lawson, version 9*), ambao utaimarisha udhibiti wa malipo ya mshahara.

- (b) Eneo lingine ambalo litazingatiwa ni ukaguzi wa miradi ya maendeleo. Kazi hii itafanywa na Kitengo cha Ukaguzi wa Kiufundi (*Technical Audit Unit*) ambacho kitakuwa chini ya Idara mpya ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Serikali. Ukaguzi huu utajikita katika kuhakikisha kuwa matumizi ya fedha katika miradi husika, yanaendana na thamani halisi ya fedha iliyotumika (*Value for Money*).
- (c) Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali aliyoitoa mwezi Machi 2011 imeonesha kuwa kuna udhaifu mkubwa wa usimamizi wa fedha za umma katika Serikali za Mitaa. Katika jitihada za kukabiliana na hali hii, Serikali inaendelea

kupunguza idadi ya Akaunti za Benki katika Halmashauri hadi zifikie sita. Hivyo, kuanzia tarehe 1 Julai, 2011 Serikali za Mitaa zitakuwa na akaunti zifuatazo:-

Akaunti ya Mapato, Akaunti ya Amana, Akaunti ya Mishahara, Akaunti ya Matumizi ya Kawaida, Akaunti ya Matumizi ya Maendeleo na Akaunti ya Mfuko wa Barabara. Hatua hii itasaidia kudhibiti matumizi ya fedha, kuongeza uwazi na uwajibikaji na kuboresha utoaji wa taarifa za mapato na matumizi. Aidha, Serikali imeendelea kuimarisha mfumo wa uwajibikaji na ufuutiliaji katika Serikali za Mitaa ili kupata thamani stahiki ya fedha za umma.

Vilevile, Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Serikali, pamoja na mambo mengine, atakuwa na majukumu ya kusimamia masuala ya ukaguzi wa ndani katika Serikali za Mitaa.

(d) Kila mwaka Serikali inatumia sehemu kubwa ya bajeti yake katika ununuzi wa bidhaa na huduma mbalimbali. Hivyo, katika mwaka wa fedha 2011/2012, Serikali imedhamiria kuweka mfumo wa ununuzi wa umma unaowezesha Serikali na Taasisi zake kupata bidhaa na huduma zenyenye ubora unaotakiwa kwa bei nzuri. Aidha, Serikali itaendelea na juhudhi zake za kudhibiti matumizi yake kwa kusitisha ununuzi wa magari ya aina zote isipokuwa kwa sababu maalum na kwa kibali cha ofisi ya Waziri Mkuu.

Vile vile, Serikali itasitisha ununuzi wa samani za ofisi hususan zile zinazoagizwa nje ya nchi; kupunguza malipo ya posho mbalimbali yasiyokuwa na tija; kupunguza matumizi ya mafuta kwa magari ya Serikali; kupunguza safari za ndani na nje ya nchi ikiwa ni pamoja na ukubwa wa misafara; na pia kuendelea kupunguza uendeshaji wa semina na warsha isipokuwa pale inapobidi na hata hivyo kwa kibali cha Ofisi ya Waziri Mkuu; pamoja na kupunguza gharama za maonesho na sherehe mbali mbali. (*Makofit*)

(e) Tangu kutungwa kwa Sheria ya Ununuzi wa Umma SURA 410 yamejitokeza mapungufu mbalimbali katika utekelezaji wa Sheria hii. Mapungufu hayo ni pamoja na yale yaliyobainishwa katika ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali ya mwaka 2009/2010, ambapo baadhi ya Idara na taasisi za Umma zimeonesha udhaifu katika utekelezaji wa Sheria hii. Aidha, ili kushughulikia mapungufu haya, Serikali iliwasilisha Muswada wa Sheria wenye mapendekezo ya marekebisho ya Sheria ya Ununuzi wa Umma 2010 katika Mkutano wa Bunge uliofanyika mwezi Aprili mwaka huu. Muswada huu ulijadiliwa na Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi pamoja na wadau mbalimbali, ambapo ilitolewa michango ya kina yenye lengo la kuboresha Muswada. Serikali kwa kuthamini michango hii, iliona ni vyema kuchapisha upya Muswada huu na baada ya kukamilika kwa zoezi hili, Serikali inatarajia kuuwasilisha Bungeni kwa ajili ya kujadiliwa kwa ruhusa ya Spika. (*Makofit*)

(f) Kuendelea kuimarisha mtandao wa kompyuta wa mfumo wa usimamizi wa fedha (*IFMIS*) katika ngazi zote za Serikali kwa lengo la kudhibiti matumizi na kuzuia malimbikizo ya madeni; kutoa mafunzo kwa Wahasibu juu ya uandaaji wa hesabu katika

viwango vya Kimataifa vya uhasibu katika sekta ya umma (*IPSAS*) ili viweze kuzingatiwa kikamilifu; kutumia utaratibu wa kufanya malipo kwa kutumia *TISS* na kuanza kutumia utaratibu huu wa malipo katika Ofisi za Hazina ndogo na Sekretarieti za Mikoa.

(g) Serikali itaendelea kudhibiti utoaji wa dhamana za Serikali kwa Wizara, Idara na Taasisi za Serikali. Aidha, Wizara, Idara na Taasisi za Serikali zinatakiwa kuomba fedha za miradi mbalimbali kwa utaratibu wa kawaida wa kibajeti na sio kwa utaratibu wa kuomba dhamana. Hatua hii itasaidia kupunguza maombi ya dhamana ili kuepuka ongezeko la deni la Taifa lisilohimilika. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi. Katika mwaka wa fedha 2010/2011, Bunge lilipitisha Sheria ya Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi ya mwaka 2010 (*Public Private Partnership Act Na.19 of 2010*). Kupitia Sheria hii, Sekta Binafsi kwa kushirikiana na sekta ya umma itaweza kujenga na kuendesha miradi muhimu na kutoa huduma za kijamii na kiuchumi kama kilimo, miundombinu, viwanda, madini, elimu, afya, mazingira, TEHAMA, biashara, michezo na burudani; hivyo kutoa nafasi kwa Serikali kuelekeza nguvu katika vipaumbele vingine. Aidha, Sheria hii inakusudia kuwawezesha wananchi kupata huduma za uhakika, endelevu, na kwa gharama nafuu, hivyo kuinua uchumi wa nchi yetu kwa kasi kubwa.

Mheshimiwa Spika, miradi ya ubia itakuwa na faida nyingi kwa taifa letu kama ifuatavyo:-

- (i) Kuongeza ushindani katika soko la ajira na hivyo kuchochea ufanisi;
- (ii) Kupanuka kwa biashara na kuongeza wigo wa kodi ya mapato;
- (iii) Kutumia raslimali-fedha za sekta Binafsi ambazo kwa kawaida ni nyingi na zinahitajika sana katika kuongeza mzunguko wa fedha katika uchumi wa nchi;
- (iv) Kuipunguzia au kuiondolea mzigo Serikali wa kubeba Mashirika yasiyo na ufanisi na kuelekeza nguvu katika vipaumbele vingine; na
- (v) Wananchi kupata uhakika wa huduma na kwa gharama nafuu.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Ubia kati ya sekta ya Umma na sekta Binafsi, imeanzisha vitengo viwili. Kitengo kimoja kiko Kituo cha Uwekezaji Tanzania ambacho kitatusika na kutangaza na kutoa vivutio kwa wawekezaji, Kitengo iko kiko Ofisi ya Waziri Mkuu. Kitengo cha pili kiko Wizara ya Fedha ambacho kitatusika na kuifanyia tathmini miradi ya ubia na kuhakikisha kuwa miradi inayoanzishwa hapa nchini inaijiendesa kibiashara, na kwa misingi ya thamani ya fedha, na haisababishi mzigo kwa Serikali. Serikali inakusudia kuvipatia vitengo hivi watalaam zaidi na wenye ujuzi wa fani ya Ubia kimataifa.

Mheshimiwa Spika, Majadiliano kati ya Wizara na Kamati za Kisekta za Bunge. Katika mchakato wa kupitisha bajeti katika baadhi ya Kamati za Kisekta za Bunge, kulikuwa na maoni kwamba bajeti za baadhi ya sekta hizo zilizopangwa kwa mwaka 2011/2012, ni ndogo na kutoa ushauri kwamba ziongezwe. Serikali imetafakari hayo yote na imeazimia kufanya marekebisho kwa baadhi ya mafungu ya bajeti kwa kuzingatia upatikanaji wa mapato mapya. Marekebisho hayo yatawasilishwa bungeni kwa ajili ya kuidhinishwa.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuboresha maslahi ya watumishi kulingana na uwezo wa mapato yake kwa lengo la kuwawezesha kumudu gharama za maisha. Maeneo ambayo yatatiliwa mkazo ni pamoja na malipo ya mshahara na likizo kwa wakati, kuhakikisha watumishi wanalipwa mafao yao mara baada ya kustaafu, pamoja na pensheni zao za kila mwezi. Sambamba na hayo, Serikali itatoa mafunzo kwa maafisa wa Hazina Ndogo na wa Mahakama zote zinazoshughulikia mirathi, na kuweka mikakati ya pamoja kuwaondolea kero wasimamizi na warithi wa mali ya marehemu.

Mheshimiwa Spika, Usimamizi wa Mashirika ya Umma. Katika mwaka wa fedha wa 2011/2012, Ofisi ya Msajili wa Hazina, pamoja na mambo mengine, imelenga kufanya yafuatayo katika usimamizi wa Wakala, Taasisi na Mashirika ya Umma.

- (i) Kuwezesha Wakala, Taasisi na Mashirika ya Umma kuingia mikataba ya utendaji na Wizara mama;
- (ii) Kutekeleza ukaguzi wa kimenejimenti kwa Wakala, Taasisi na Mashirika ya Umma;
- (iii) Kuuandaa mfumo wa uperembaji na uhakiki wa Menejimenti na Bodi za Wakala, Taasisi na Mashirika ya Umma;
- (iv) Kuongeza makusanyo ya mapato yasiyo ya kodi kwa kuzingatia Sheria ya Fedha Na. 13 ya mwaka 2008 pamoja na Waraka wa Hazina Na. 8 wa 2008/2009;
- (v) Kuunda Mfuko wa Uwekezaji kwa ajili ya mitaji ya Wakala, Taasisi na Mashirika ya Umma;
- (vi) Kutathmini mfumo wa uwiano wa mishahara ya Wakala, Taasisi na Mashirika ya Umma;
- (vii) Kuratibu uperembaji na uhakiki wa mashirika yaliyobinafsishwa; na
- (viii) Kuendelelea kushauri Serikali juu ya uwekezaji katika Wakala, Taasisi na Mashirika ya Umma.

Mheshimiwa Spika, Masuala yanayohusu Serikali za Mitaa. Serikali itaendelea kuboresha utendaji na uwajibikaji wa Mamlaka za Serikali za Mitaa kupitia Programu ya

Maboresho ya Serikali za Mitaa (*LGRP II*) ili kuwawezesha Wakurugenzi kusimamia majukumu yao kikamilifu.

Serikali pia itawajengea uwezo Waheshimiwa Madiwani ili wasimamie utendaji wa Halmashauri zao na kuhakikisha nidhamu ya kazi inaimarishwa kulingana na sheria, taratibu na kanuni za Utumishi wa Umma. Aidha, Kamati za kupambana na rushwa pamoja na Kamati za Maadili za Halmashauri zitaimarishwa ili kusimamia nidhamu ya watumishi wa kada zote na kuhakikisha utendaji wao unazingatia maslahi ya Taifa. Vile vile, Serikali itaimarisha mfumo wa tathimini ya utendaji kazi - *OPRAS* kwa Watendaji wa Halmashauri na kufanya mapitio ya vigezo vya kupima utekelezaji wa majukumu ya Halmashauri (*Performance Assessment Criteria*) ili kuongeza tija na ufanisi wa watendaji wa Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, Serikali za Mitaa zitaendelea kukusanya mapato kutoka katika vyanzo vyake, ambapo jumla ya shilingi bilioni 350.5 zinakadirwa kupatikana kutoka vyanzo hivyo. Kiwango hicho cha mapato ni sawa na asilimia 5.2 ya mapato ya ndani yanayokusanywa na Serikali Kuu.

Kiwango hicho kinaonesha juhudu zitakazochukuliwa na Serikali kuboresha ukusanyaji ikilinganishwa na asilimia 2.9 ya mapato ya ndani yanayotarajiwa mwaka 2010/2011. Serikali itaendeleza juhudu za ukusanyaji mapato katika ngazi ya Halmashauri, ili kuhakikisha kwamba mapato hayo yanawiana na fursa zilizopo.

Baadhi ya hatua zitakazochukuliwa, ni pamoja na: kuendelea kuboresha mifumo ya ukusanyaji na usimamizi wa mapato kutoka vyanzo vya Halmashauri; kupitia upya vyanzo vya Halmashauri vilivyofutwa; kupitia mfumo wa kodi ya majengo katika Majiji, Manispaa, Miji, Wilaya na miji midogo; na kuainisha mianya ya upotevu wa mapato na vyanzo mbadala vya kuongeza mapato ya Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa matumizi, Serikali itaendelea kuboresha uratibu na usimamizi wa matumizi ya Halmashauri.

Baadhi ya hatua zitakazotekelawa ni pamoja na kuziwezesha na kuziimarisha Idara za Mipango, Uhasibu na Ugaguzi wa Ndani ili kuongeza uwajibikaji, usimamizi na udhibiti wa fedha katika Halmashauri; kuboresha na kupanua miundombinu ya barabara, maji na umeme; kuendelea kutekeleza sera ya ugatuaji wa madaraka kwa wananchi kwa kujenga uwezo wa Halmashauri katika kusimamia utekelezaji wa majukumu yao; na kuendelea kutekeleza program mbalimbali za maboresho.

Mheshimiwa Spika, Maboresho ya Mfumo wa Kodi, Ada, Tozo na Hatua nyingine za Mapato. Serikali itaendelea kuchukua hatua mbalimbali za kisera na kiutawala ili kuongeza mapato ya kodi na yasiyo ya kodi, na kupanua wigo wa mapato katika maeneo mengine. Aidha, Serikali itaendelea kufanya mapitio ya sheria mbalimbali zinazotoa misamaha ya kodi kwa lengo la kudhibiti na kupunguza misamaha hiyo; kusimamia Mpango wa Tatu wa Miaka Mitano wa Maboresho ya utendaji wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA); Kuendelea kuingiza Sekta isiyo rasmi kwenye

mfumo wa kodi; kupitia upya mfumo wa ukusanyaji wa kodi ya majengo katika Majiji, Manispaa, Miji, Wilaya na miji midogo; na kufanya mapitio ya vyanzo vyia mapato na mfumo wa ukusanyaji katika Serikali za Mitaa ili kuongeza mapato.

Mheshimiwa Spika, marekebisho ya mfumo wa Kodi yanahusu Sheria zifuatazo:-

- (a) Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Sura 148;
- (b) Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura 332;
- (c) Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura 147;
- (d) Sheria ya Elimu na Mafunzo ya Ufundu Stadi, Sura 82;
- (e) Sheria ya Ushuru wa Stempu, Sura 189;
- (f) Sheria ya Ushuru wa Mafuta ya Petroli, Sura 220;
- (g) Sheria ya Leseni za Biashara, Sura 208;
- (h) Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, Sura 290;
- (i) Sheria ya Usalama Barabarani, Sura 168.
- (j) Marekebisho madogo madogo katika baadhi ya sheria za kodi;
- (k) Marekebisho ya Ada na Tozo Mbalimbali za Wizara, Mikoa na Idara zinazojitegemea; na
- (l) Sheria ya Forodha ya Jumuuya ya Afrika Mashariki, ya mwaka 2004.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Slusra 148. Ili kuhamasisha uwekezaji na kuboresha uzalishaji katika Sekta za Kilimo, Mifugo, Viwanda, Biashara na Utalii na kuziwezesha kuchangia zaidi kwenye pato la Taifa, napendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Sura ya 148 kama ifuatavyo: -

- (i) Kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye Vipuri vyia Zana za kilimo zifuatazo:- fyeko (*threshers*), mashine za kukausha na kukoboa mpunga (*rice dryers and mills*), mashine za kupandia mbegu (*planters*), na matrekta yote.
- (ii) Kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye chakula cha kuku (*NASCOR Pellet Feed*). Hatua hii ina lengo la kuhamasisha uwekezaji katika ufugaji wa kuku hapa nchini;
- (iii) Kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye nyuzi (*Nylon Fishing Twine*) zinazotumika kutengeneza nyavu za kuvulia samaki. Hatua hii inalenga katika kupunguza gharama za uzalishaji na kuendeleza sekta ya uvuvi hapa nchini;

(iv) Kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye vipuri vyaa mashine za kunyunyiza na kutifua udongo (*sprayers and harrows*) na mashine za kupanda nafaka (*grain conveyors*); na

(v) Kuanzisha utaratibu wa marejesho ya Kodi kwenye mauzo ya rejareja kwa bidhaa za ndani zinazouzwa kwa abiria ambaa sio raia wa Tanzania wanaosafiri nje ya nchi. Utaratibu huu utaanza kutekelezwa kwa kuanzia na Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Mwalimu Julius Nyerere na Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro kwa mauzo ya thamani ya shilingi 400,000 na zaidi. Utekelezaji wa utaratibu huu mpya utaanza rasmi tarehe 1 Januari, 2012.

Mheshimiwa Spika, napendekeza pia kufanya marekebisho katika Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, SURA 148 kwa nia ya kuongeza mapato na kuhamasisha Mashirika na Taasisi mbalimbali ziweze kuchangia katika juhudii za Serikali za kuboresha huduma katika sekta ya elimu.

(vi) Kuondoa msamaha wa Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye kuuza na kupangisha majengo ya kuishi ya nyumba za Shirika la Nyumba la Taifa (*NHC*);

(vii) Kuondoa unafuu wa Kodi ya Ongezeko la Thamani uliokuwa unatolewa kwa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (*Non Governmental Organizations*). Hatua hii haitazihusu Taasisi za Kidini (*Religious Organizations*); na

(viii) Kutoa unafuu wa Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa Mashirika yasiyo ya Kiserikali (*Non Governmental Organizations*) kwa vifaa vyaa matumizi binafsi ya kawaida (*household consumables*) kama vile vyakula, mavazi, na vifaa kama sabuni ambavyo vinatolewa msaada kwenye vituo mahsusii vyaa kulelea watoto yatima na shule.

Hatua hizi katika Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa pamoja zitaongeza mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi milioni 71,518.9.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Kodi ya Mapato Sura ya 332. Napendekeza kufanya marekebisho ya sheria ya Kodi ya Mapato, Sura 332 kama ifuatavyo: -

(i) Kusamehe kodi ya mapato kwenye posho wanazolipwa wafanyakazi wa Serikali na wanaofanya kazi kwenye Taasisi zinazopata ruzuku kutoka kwenye bajeti ya Serikali.

(ii) Kufuta Kodi ya Zuio kwa usafirishaji wa samaki nje ya nchi kwa kutumia ndege za nje. Hatua hii inalenga katika kuhamasisha mauzo ya samaki nje ya nchi.

Hatua hizi za Kodi ya Mapato zitapunguza mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi milioni 20,287.5.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Ushuru wa Bidhaa Sura 147. Napendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, SURA 147 kama ifuatavyo:-

(i) Kupunguza ushuru wa bidhaa kwenye mafuta mazito ya kuendeshea mitambo kutoka shilingi 80 hadi shilingi 40 kwa lita ili kupunguza gharama za uzalishaji wa bidhaa hapa nchini; (*Makofi*)

(ii) Kutoza ushuru wa bidhaa wa asilimia 50 badala ya asilimia 120 kwenye mifuko ya plastiki za *microns* 30 na zaidi yaani *Polymers of ethylene* na nyinginezo za (*HS. Code 3923.2900*).

(iii) Kurekebisha kwa 10% viwango vya Ushuru wa bidhaa mbalimbali isipokuwa zile za mafuta ya Petroli kama ifuatavyo: -

(a) Vinywaji baridi kutoka shilingi 63 kwa lita hadi shilingi 69 kwa lita;

(b) Bia inayotengenezwa na nafaka ya hapa nchini na ambayo haijaoteshwa, kutoka shilingi 226 kwa lita hadi shilingi 249 kwa lita;

(c) Bia nyingine zote, kutoka shilingi 382 kwa lita hadi shilingi 420 kwa lita;

(d) Mvinyo uliotengenezwa kwa zabibu inayozalishwa nje ya nchi kwa kiwango kinachozidi asilimia 25, kutoka shilingi 1,223 kwa lita hadi shilingi 1,345 kwa lita;

(e) Mvinyo uliotengenezwa kwa Zabibu inayozalishwa hapa nchini kwa kiwango kinachozidi asilimia 75 utatozwa shilingi 420 kwa lita; na

(f) Vinywaji vikali, kutoka shilingi 1,812 kwa lita hadi shilingi 1,993 kwa lita.

(iv) Kurekebisha viwango vya Ushuru wa bidhaa kwenye sigara kama ifuatavyo:-

(a) Sigara zisizo na kichungi na zinazotengenezwa kutokana na Tumbaku inayozalishwa hapa nchini kwa kiwango cha angalau asilimia 75, kutoka shilingi 6,209 hadi shilingi 6,830 kwa Sigara elfu moja;

(b) Sigara zenye kichungi na zinazotengenezwa kutokana na Tumbaku inayozalishwa hapa nchini kwa kiwango cha angalau asilimia 75, kutoka shilingi 14,649 hadi shilingi 16,114;

(c) Sigara nyingine zenye sifa tofauti na (a) na (b) kutoka shilingi 26,604 hadi shilingi 29,264 kwa Sigara elfu moja(d) Tumbaku ambayo iko tayari kutengeneza sigara (*cut filler*) kutoka shilingi 13,436 hadi shilingi 14,780 kwa kilo; na

(e) Ushuru wa *Cigar* unabaki asilimia 30.

Hatua hizi katika Ushuru wa Bidhaa kwa pamoja zinatarajiwa kuongeza mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi milioni 99,521.5.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi, Sura 82. Napendekeza kufanya marekebisho kwenye sheria ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi, Sura ya 82 kama ifuatavyo:-

(i) Kufanya marekebisho katika mgawanyo wa mapato yatokanayo na tozo ya kuendeleza ufundisti (Skills Development Levy) ya asilimia 6 ili asilimia 4 zipelekwe kwenye Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu, na asilimia mbili zipelekwe Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (*Vocational Education and Training Authority - "VETA"*). Lengo la hatua hii ni kuongeza fedha za mikopo kwa wanafunzi wa Elimu ya Juu. (*Makofi*)

Hatua hii katika Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi haitarajiwu kupunguza wala kuongeza mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Ushuru wa Stempu, Sura ya 189. Napendekeza kufanya marekebisho ya Ushuru wa Stempu, SURA 189 kama ifuatavyo: -

(i) Kusamehe ushuru wa stempu wakati umiliki wa mali (Asset) unapohamishiwa katika chombo maalum (Kampuni) cha kutekeleza na kusimamia uzalishaji wa kipato (*Special Purpose Vehicle "SPV"*) kwa madhumuni ya kutoa dhamana zinazotegemea hiyo mali ambayo umiliki wake umehamishwa. Hatua hii inalenga katika kuhamasisha miradi ya uwekezaji inayohitaji fedha nyingi, mfano; miradi ya barabara, madaraja, nishati na maji. Aidha, ni njia mbadala ya mabenki ya upatikanaji wa fedha za kugharamia miradi.

Hatua hii ya ushuru wa stempu haitapunguza mapato ya Serikali bali inalenga katika kuhamasisha utunzaji wa akiba na kuchochea uwekezaji (*Savings Mobilization and Investment Promotion*).

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Ushuru wa Mafuta ya Pwetroli, Sura 220. Napendekeza kufanya Marekebisho katika Sheria ya Ushuru wa Mafuta ya Petroli, SURA 220 kama ifuatavyo:-

(i) Kusamehe Ushuru wa Mafuta ya Petroli unaotozwa kwenye mafuta yanayotumika kwenye kuendesha meli, na vifaa vingine vinavyotumika katika utafiti wa mafuta na gesi na msamaha huu utatolewa kuititia Tangazo la Serikali. Aidha, maombi ya msamaha yatahakikiwa na kuitishwa na Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (*TPDC*) kabla ya kuwasilishwa Wizara ya Fedha. Hatua hii inalenga katika kutoa unafuu wa gharama kwa Kampuni zinazofanya utafiti wa mafuta na gesi.

(ii) Ili kutatua tatizo la ucheleweshaji wa marejesho ya kodi (*tax refunds*) kwenye mafuta yanayonunuliwa na Kampuni za madini, Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) itaanzisha utaratibu wa kuweka kiasi cha fedha kwenye Akaunti maalum (*escrow account*) ambacho kinawiana na kiwango cha mahitaji ya mafuta kwa mwezi. Aidha Kampuni itaruhusiwa kununua mafuta kwenye matanki ya Kampuni za waagizaji wa mafuta bila ya kulipia kodi kwa kiwango cha fedha ilichoweka kwenye akaunti.

Endapo mahitaji ya mafuta kwa mwezi yatakuwa makubwa zaidi ya kiwango ilichoweka kwenye akaunti, Kampuni hiyo itawajibika kuongeza fedha za ziada zenye kukidhi mahitaji yake. Hatua hii inatarajiwa kutatua tatizo la ucheleweshaji wa marejesho ya kodi iliyolipwa kwenye mafuta. Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) itaandaa utaratibu wa utekelezaji utakaohusisha kampuni za madini na kampuni za mafuta hapa nchini. Hatua hizi kwa pamoja zitapunguza mapato ya Serikali kwa shilingi milioni 2,007.6.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Leseli ya Biuashara, Sura 208. Napendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Leseni ya Biashara, Sura 208 ili kutoza ada ya leseni ya biashara kwa viwango na maeneo yafuatayo: -

(a) Mamlaka za Miji (Majiji, Manispaa na Miji) zitoze shilingi 50,000 kwa mwaka kwa kila aina ya biashara inayostahili kupewa leseni ya biashara (isipokuwa ya vileo) inayoendeshwa katika maeneo ya mamlaka hizo.

(b) Halmashauri za Wilaya zitoze na kukusanya Ada ya leseni ya biashara ya shilingi 30,000 kwa mwaka kwa biashara zinazoendeshwa katika maeneo ya miji midogo na vituo vya biashara.

(c) Halmashauri za vijiji zitoze na kukusanya shilingi 10,000 kwa mwaka kwa kila biashara inayoendeshwa katika maeneo yake.

Lengo la hatua hii ni kuimarisha usimamizi wa Kanuni za biashara hapa nchini na kuwianisha ukua ji wa biashara na mapato yanayokusanywa. Pia itaongeza mapato kwa Serikali za Mitaa na kuongeza uwezo katika kuhimili mahitaji yao. Aidha, utekelezaji wa hatua hii unazingatia Sera ya Serikali ya ugatuaji madaraka kwa wananchi (*Decentralization by Devolution “D by D”*). (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, Sura 290. Napendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa Sura ya 290 ili kuiziwezesha Serikali za Mitaa kutoza ada ya leseni ya biashara kwa viwango na maeneo yaliyoainishwa kwenye sheria ya leseni ya biashara.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Usalama Barabarani, Sura 168. Napendekeza kufanya marekebisho ya Sheria ya Usalama Barabarani, SURA, 168 ili kuongeza ukomo wa kiwango cha faini inayotozwa kwa kufanya makosa wakati wa uendeshaji gari barabarani (*Traffic Notification Fee*) kutoka shilingi 20,000 hadi shilingi 50,000. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Marekebisho madogo madogo katika baadhi ya Sheria za Kodi. Napendekeza kufanya marekebisho mengine madogo madogo yasiyo ya kisera katika Sheria mbalimbali za kodi ili ziwe sanjari na azma ya kurahisisha utekelezaji wake.

Mheshimiwa Spika, Marekebisho ya Ada na Tozo Mbalimbali za Wizara, Mikoa na Idara zinazojitegemea. Napendekeza kufanya marekebisho ya viwango vya ada na tozo mbali mbali zinazotozwa na Wizara, Mikoa na Idara zinazojitegemea ili kuvihiusha kulingana na hali halisi ya ukuaji wa uchumi.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, ya mwaka 2004. Kikao cha maandalizi ya Bajeti cha Mawaziri wa Fedha wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (*Pre-Budget Consultations of EAC Ministers for Finance*) kilichofanyika tarehe 7 Mei, 2011 Jijini Kampala, Uganda; kilipendekeza marekebisho ya viwango vya Ushuru wa pamoja wa Forodha (*EAC Common External Tariff “CET”*) na Sheria ya Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (*EAC Customs Management Act, 2004*).

**SPIKA:** Naomba *Order* kama hamjui kuendesha ndiyo hivyo sasa. Tutulie ili kusudi tumsikilize amalize upesi. (*Kicheko*)

**WAZIRI WA FEDHA:** Marekebisho hayo yanalenga katika kukuza Sekta za Viwanda, Usafirishaji, Mifugo, Biashara na Utalii. Aidha yanalenga pia katika kuboresha afya ya jamii na kuimarissha ulinzi na usalama wa raia na mali zao.

Mheshimiwa Spika, maeneo yanayopendekezwa kufanyiwa marekebisho kwenye viwango vya Ushuru wa Pamoja wa Forodha (*EAC Common External Tariff*) ni yafuatayo:-

(i) Tanzania iruhusiwe kutoza ushuru wa forodha wa asilimia 10 badala ya asilimia 35 kwenye ngano inayotambuliwa katika *HS Code 1001.90.20* na *HS Code 1001.90.90* kwa muda wa mwaka mmoja. Lengo la hatua hii ni kupunguza gharama za uingizaji nchini wa bidhaa hiyo na kuwezesha walaji kupata vyakula kwa bei nafuu. (*Makofi*)

(ii) Kutoa msamaha wa ushuru wa forodha (*duty remission*) kwenye malighafi ya kutengeneza sabuni (*Palm Steering, RBD*) inayotambuliwa katika *HS Code 1511.90.40* kwa kipindi cha mwaka mmoja. Hatua hii inalenga kutoa unaifuu wa kodi kwenye viwanda vidogo na vya kati vya kutengeneza sabuni hapa nchini. (*Makofi*)

(iii) Kutenganisha malighafi zinazotambulika katika *HS Code 2710.19.59* ili kutoa msamaha wa ushuru wa forodha (*duty remission*) kwenye malighafi za kutengeneza manukato na sabuni (*white oil*). Hatua hii inalenga katika kupunguza gharama za uzalishaji viwandani.

(iv) Kutoa msamaha wa ushuru wa forodha (*duty remission*) kwenye malighafi za kutengeneza maganda ya viberiti (*duplex boards*) yanayotambuliwa katika *HS Code 4810.92.00*. Hatua hii inalenga katika kupunguza gharama za uzalishaji na kulinda Viwanda nya Viberiti kutozana na ushindani wa viberiti vinavyoagizwa nje.

(v) Kutoza ushuru wa forodha wa 10% badala ya 0% kwenye waya za chuma ambazo zimenakisiwa na zink (*Galvanized Plated/Coated Wire*), zinazotambuliwa katika *HS Code 7217.20.00* kwa kuwa waya ambazo hazikunakisiwa (*Non Plated/Coated Wire*) hutozwa ushuru wa forodha wa asilimia 10. Lengo la hatua hii ni kuwianisha ushuru wa malighafi inayotumika kuzalisha bidhaa hii ili iendane na kanuni/taratibu za kutoza ushuru zinazozingatia viwango nya usindikaji.

(vi) Kupunguza ushuru wa forodha kwenye mifuko ya plastiki ya kuhifadhi malighafi za matunda (*aseptic bags*) kutoka asilimia 25 hadi asilimia 10 inayotambuliwa katika *HS Code 3923.29.00* kwa kipindi cha mwaka mmoja ili kupunguza gharama za uzalishaji na kuhamasisha usindikaji wa mazao ya matunda hapa nchini.

(vii) Kutoa msamaha wa ushuru wa forodha (*duty remission*) kwa kipindi cha mwaka mmoja kwenye shaba ghafi (*copper Cathodes*) inayotambuliwa katika *HS Code 7403.11.00*. Hivi sasa bidhaa hii inatozwa ushuru wa asilimia 10 ambapo shaba iliyotengenezwa kwa ukamilifu (*copper alloys/refined copper*) hutozwa ushuru wa asilimia 0, ambapo ni kinyume na matakwa ya sheria ya ushuru wa forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya mwaka 2004. Lengo la hatua hii ni kuwianisha ushuru wa malighafi inayotumika kuzalisha bidhaa hii ili iendane na kanuni/taratibu za kutoza ushuru zinazozingatia viwango nya usindikaji.

(viii) Kutoa msamaha wa ushuru wa forodha (*duty remission*) kwa waunganishaji wa majokofu (*refrigerators and freezers*) ili walipe ushuru wa forodha wa asilimia 10 badala ya asilimia 25 kwenye vifaa nya kuunganisha majokofu hayo (*component parts and inputs for assemblers of refrigerators and freezers*). Hatua hii inalenga katika kuhamasisha uzalishaji wa bidhaa hizo na kuongeza ajira hasa kwa vijana.

(ix) Kutenganisha malighafi zinazotambulika katika *HS Code 2309.90.00* ili kutoa msamaha wa ushuru wa forodha kwenye malighafi za kutengeneza vyakula nya mifugo (*premixes*). Lengo ni kutoa unafuu katika bei za chakula cha mifugo na kuhamasisha ufugaji.

(x) Kuendelea kutoza ushuru wa forodha wa asilimia 10 badala ya asilimia 25 kwenye mabasi yenye uwezo wa kubeba abiria zaidi ya 25 yanayotambuliwa katika *HS Code 8702.10.99 na HS Code 8702.90.99*.

(xi) Kuendelea kutoza ushuru wa forodha wa asilimia 10 badala ya asilimia 25 kwenye magari ya mizigo yenye uwezo kati ya tani 5 na tani 20 yanayotambuliwa katika *HS Code 8704.22.90* kwa muda wa mwaka mmoja.

(xii) Kuendelea kutoa msamaha wa ushuru wa forodha kwenye magari ya mizigo yenye uwezo zaidi ya tani 20 yanayotambuliwa katika *HS Code 8704.23.90* kwa muda wa mwaka mmoja.

(xiii) Kutoza ushuru wa forodha wa 10% badala ya 25% kwenye mabasi yatakayoagizwa kwa ajili ya mradi wa mabasi wa jiji la Dar es Salaam yanayotambuliwa katika *HS Code 8702.10.99* na *HS Code 8702.90.99* kwa muda wa mwaka mmoja.

(xiv) Kutenganisha bidhaa zinazotambulika katika *HS Code 8703.90.10* ili kutoa msamaha wa ushuru wa forodha kwenye pikipiki maalumu za kubeba wagonjwa (*motorcycle ambulances*). Hatua hii inalenga kuimarisha utoaji wa huduma ya kusafirisha wagonjwa hasa katika maeneo ya vijijini.

(xv) Kutenganisha virutubisho vya chakula vinavyotambulika katika *HS Code 2106.90.90* ili kutoza ushuru wa forodha wa asilimia 10 badala ya asilimia 25 kwenye virutubisho vya vyakula vya binadamu (*food supplements*) ili kuendana na Sera ya Serikali ya kuboresha afya za wananchi.

(xvi) Kutenganisha bidhaa zinazotambulika katika *HS Code 9616.10.00* ili kutoza ushuru wa forodha wa asilimia 10 badala ya asilimia 25 kwenye malighafi za kutengeneza vifaa vya kunyunyizia (*scent sprays and other similar toilet sprays and mounts and heads*).

(xvii) Kuendelea kutoa msamaha wa ushuru wa forodha kwenye matrekta ya kukokota mizigo yanayotambuliwa katika *HS Code 8701.20.90* kwa muda wa mwaka mmoja. Hatua hii inalenga katika kuboresha usafirishaji mizigo na kuongeza ufanisi katika Sekta ya usafirishaji.

(xviii) Kuendelea kutoa msamaha wa ushuru wa forodha kwenye migahawa ya Majeshi ya Ulinzi kwa kipindi cha mwaka mmoja.

Mheshimiwa Spika, Mawaziri wa Fedha walikubaliana kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (*EAC Customs Management Act, 2004*) kama ifuatavyo:-

(i) Kufanya marekebisho katika kifungu cha pili (2) cha Jedwali la Tano la Sheria ya Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ili kuliwezesha Jeshi la Polisi kunufaika na msamaha wa ushuru wa forodha kama linavyonufaika Jeshi la Ulinzi. Hatua hii inalenga katika kuimarisha usalama wa raia na mali zao.

(ii) Kufanya marekebisho katika Jedwali la Tano (5) la Sheria ya Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa nia ya kutekeleza yafuatayo:-

(a) Kutoa msamaha wa ushuru wa forodha kwenye mitego ya mbung'o. Hatua hii inalenga katika kuchochea ukuaji wa kilimo na kuboresha mazingira ya kuvutia utalii hapa nchini.

- (b) Kutoa msamaha wa ushuru wa forodha kwenye vifaa vya kudhibiti usalama (*security equipments: - hand held metal detectors, walk through metal detectors, CCTV cameras, bomb detectors and undercarriage mirrors*). Hatua hii inalenga katika kuboresha usalama wa raia na mali zao.
- (c) Kutoa msamaha wa ushuru wa forodha kwenye magari yanayoendeshwa kwa kutumia beteri (*battery operated vehicles/Golf carts*). Hatua hii itaimarisha huduma za kitalii na huduma za afya kwani magari haya yanaweza kutumika kubeba wagonjwa ndani ya hospitali na kubeba wageni na mizigo katika maeneo ya hoteli.
- (d) Kutoa msamaha wa Ushuru wa forodha kwenye magari yanayotumika kubeba abiria katika viwanja vya ndege (*Apron buses*) ili kuboresha huduma kwa wasafiri na kuweka mazingira yenye kuvutia wageni na hasa watalii.
- (e) Kutoa msamaha wa ushuru wa forodha kwenye malighafi za kutengeneza vifaa vinavyotumia mionzi ya jua (*inputs for manufacture of solar panels*) kwa lengo la kuhamasisha uzalishaji wa vifaa hivyo hapa nchini.
- (f) Kupunguza kiwango cha ada ya ukaguzi (*Destination Inspection Fee*) kinachotozwa kwenye bidhaa za biashara zinazotoka nje kutoka asilimia 1.2 ya thamani ya huduma ya kuzifikisha hadi bandarini (*FOB*) na kuwa asilimia 0.6. Hatua hii inalenga katika kupunguza muda wa kuondoa mizigo bandarini na kupunguza gharama za uingizaji bidhaa na hivyo kupunguza bei za bidhaa kutoka nje.

Mheshimiwa Spika, hatua hizi kwa pamoja zinatarajiwa kupunguza mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi milioni 4,669.7.

Mheshimiwa Spika, Tarehe ya Kuanza Kutekeleza Hatua Mpya za Kodi. Hatua hizi za kodi zinazopendekezwa zianze kutekelezwa tarehe 1 Julai, 2011, isipokuwa pale ilipoelezwa vinginevyo.

Mheshimiwa Spika, Mfumo wa Bajeti kwa Mwaka 2011/2012. Kwa kuzingatia sera za uchumi pamoja na misingi na Sera za Bajeti, Sura ya Bajeti inaonesha kwamba jumla ya shilingi bilioni 13,525.9 zinahitajika kutumika katika kipindi cha 2011/2012.

Jumla ya mapato yanayotarajiwa ni shilingi bilioni 13,525.9. Kati ya mapato hayo, Serikali inalenga kukusanya mapato ya kodi na yasiyo ya kodi ya jumla ya shilingi bilioni 6,775.9, sawa na asilimia 17.2 ya Pato la Taifa. Aidha, mapato kutoka vyanzo vya Halmashauri ni shilingi bilioni 350.5. Kadhalika, Serikali inategemea kukopa kiasi cha shilingi bilioni 2,475.9 kutoka vyanzo vya ndani na nje. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 810.9 ni kwa ajili ya kulipia hatifungani na dhamana za Serikali zinazoiva, shilingi bilioni 393.4 ni mikopo kutokana na mauzo ya hatifungani za Serikali na shilingi bilioni 1,271.6 zitatokana na mikopo yenye masharti ya kibiashara.

Mheshimiwa Spika, washirika wa Maendeleo wanatarajiwa kuendelea kuchangia bajeti kupitia misaada na mikopo ya jumla ya shilingi bilioni 3,923.6. Kati ya fedha hizo,

shilingi bilioni 869.4 ni misaada na mikopo ya kibajeti na shilingi bilioni 3,054.1 ni misaada na mikopo kwa ajili ya miradi ya maendeleo, ikijumuisha mifuko ya kisekta.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa matumizi, katika mwaka 2011/12 Serikali imepanga kutumia jumla ya shilingi bilioni 13,525.9 kwa matumizi ya kawaida na maendeleo. Kati ya fedha hizo, kiasi cha shilingi bilioni 8,600.3 kimetengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida, ikijumuisha shilingi bilioni 3,270.3 kwa ajili ya mishahara ya watumishi wa Serikali, taasisi na wakala za Serikali na shilingi bilioni 1,910.4 kwa ajili ya Mfuko Mkuu wa Serikali. Aidha, jumla ya shilingi bilioni 4,925.6 zimetengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo, ambapo shilingi bilioni 1,871.5 ni fedha za ndani na shilingi bilioni 3,054.1 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, kutokana na maelezo ya mfumo wa Bajeti yaliyotolewa hapo juu, Sura ya Bajeti kwa mwaka 2011/2012 itakuwa kama ifuatavyo:-

Mapato ya Ndani yanatarajiwa kuwa shilingi milioni 6,775,952. Mapato hayo ni sawa swa na Mapato ya Kodi yanayokusanywa na TRA Ambato tatakuwa shilingi milioni 6,228,836. Mapato yasiyo ya Kodi shilingi milioni 547,116. Mapato ya Halmashauri yanategemewa kuwa milioni 350,496. Mikopo na misaada ya nje inatarajiwa kuwa shilingi milioni 3,923,551. Mikopo ya ndani inatarajiwa kuwa milioni 1,204,262. Mikopo ya masharti ya kibashara inatarajiwa kuwa shilingi milioni 1,271,634. Jumla ya Mapato yote ni shilingi milioni 13,525,895.

Mheshimiwa Spika, Matumizi ya Kawaida yanatarajiwa kuwa shilingi milioni 8,600,287. Matumizi hayo yatakuwa kama ifuatavuyo:-Mfuko Mkuu wa Serikali shilingi Milioni 1,910,376, Mishahara milioni 3,270,292, Matumizi Mengineyo milioni 3,419,619, Wizara itakuwa milioni 2,727,472, Mikoa shilingi milioni 49,981, Halmashauri za Wilaya shilingi milioni 642,166.

Mheshimiwa Spika, Matumizi ya Maendeleo yanatarajiwa kuwa milioni 4,924,608. Fedha za Ndani shilingi 1,871,471, Fedha za Nje shilingi 3,054,137. Jumla ya Matumizi yote ni sawa sawa na Mapato yote yatakayokusanywa ya shilingi milioni 13,525,895.

Mheshimiwa Spika, Hitimisho. Bajeti ya mwaka 2011/2012 ni mwendelezo wa juhudi za Serikali za kuwaletea maendeleo wananchi. Bajeti hii imezingatia:-

- (i) Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025;
- (ii) Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini Awamu ya Pili (MKUKUTA II);
- (iii) Malengo ya Maendeleo ya Milenia 2015;
- (iv) Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010-2015;

- (v) Mkakati wa Pamoja wa Misaada Tanzania;
- (vi) Mkakati wa Taifa wa Madeni; na
- (vii) Sera za Kijumla za Uchumi kwa mwaka 2011/2012. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ili kufikia malengo hayo mapema zaidi, kila mwananchi anapaswa kujituma na kushiriki kikamilifu, kwa kutumia fursa zilizopo za kuzalisha mali na kuiongezea kipato. Ni matumaini yangu kuwa utekelezaji sahihi wa Bajeti hii utaiwezesha Serikali kuwaletea wananchi maendeleo tunayokusudia.

Bajeti ya mwaka 2011/2012 imeandaliwa katika kipindi ambacho nchi yetu inakabiliwa na changamoto ya kiuchumi ikiwemo upungufu wa umeme na ongezeko la bei za mafuta katika soko la dunia. Hali hii imetishia ustawi wa uchumi na uwezo wa kukusanya mapato ya ndani.

Serikali imejipanga kukabiliana na changamoto hizi, ikiwa ni pamoja na kuharakisha miradi ya uzalishaji umeme na uanzishwaji wa hifadhi kubwa ya mafuta yanayoagizwa. Wakati Serikali ikichukua hatua hizi, wananchi wanaombwa kuanza kutumia kwa uangalifu vyanzo hivyo vya nishati, ili kupunguza gharama. Hivyo, ni matumaini ya Serikali kwamba Bajeti ya mwaka 2011/2012 itatekelezwa kama ilivyopangwa.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Awamu ya Nne, imedhamiria kwa dhati kuendeleza misingi imara ya kujenga uwezo katika kukusanya mapato ya ndani. Hili litawezekana kwa kuwekeza katika vichocheo vya ukuaji uchumi ili kuongeza wigo wa mapato ya ndani kwa lengo la kutuungeza uwezo wa kujitegemea.

Kama nilivyoleza hapo awali, maeneo yafuatayo ya kimkakati yatazingatiwa katika mgao wa rasilimali katika muda wa kati: nishati ya umeme; reli, bandari; TEHAMA; maji; kilimo na kulinda mafanikio yaliyopatikana katika sekta ya elimu na afya. Hivyo basi, hatuna budi kila mmoja wetu na kwa pamoja kuongeza ubunifu katika uzalishaji wenye tija utakaoongeza Pato la Taifa na hatimaye kuondokana na umaskini.

Mheshimiwa Spika, bajeti hii imezingatia ushauri wa Waheshimiwa Wabunge wa Kamati ya Fedha na Uchumi na Kamati nyingine za Kisekta. Pia, imezingatia mawazo na mapendekezo ya wadau mbalimbali, wakiwemo wafanyabiashara, wenye viwanda, sekta ya kilimo, utalii na wengine wengi. Nawashukuru wote hao kwa mawazo na ushauri wao mzuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kuwashukuru wapiga kura wangu wote wa Jimbo la Kilosa kwa kunichagua tena kuwa Mbunge wao kwa kipindi kingine cha miaka mitano. Napenda kuwaahidi kwamba tutashirikiana pamoja kuliletea maendeleo Jimbo letu la Kilosa. Kwangu Kilosa ni kwa sababu ya kutekeleza majukumu ya Taifa. Ninaamini kwamba sitawaangusha.

Mwisho nachukua pia nafasi hii kumshukuru kipekee mke wangu mpendwa kwa kuwa msaada mkubwa kwangu pamoja na kuwa na kazi nyingi za Kitaifa. Napenda pia kuwashukuru wanangu watano na wajukuu zangu sita kwa uvumilivu wao. Nawaahidi kwamba baada ya bajeti hii Dodoma, wataniona nyumbani. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza awali Serikali inatambua makali ya maisha yanayowakabili wananchi. Kuna tatizo la upungufu wa umeme, kuongezeka kwa bei za mafuta ya petroli na gharama za usafiri, tatizo la ajira na haja ya kuboresha hifadhi yetu ya chakula. Serikali sikuvi ya Chama cha Mapinduzi imejipanga kikamilifu kukabiliana na changamoto hizo.

**WABUNGE FULANI:** Rudia!

**WAZIRI WA FEDHA:** Nisome tena? Mnasema nyie?

**WABUNGE FULANI:** Eeeh!

**WAZIRI WA FEDHA:** Serekali sikuvi kwa wananchi wa Tanzania ya Chama cha Mapinduzi (CCM) imejipanga kikamilifu na changamoto hizo. Ni matumaini ya Serikali kwamba hatua za kukabiliana na changamoto hizo nilizozieleza zitasaidia kuondoa kero hizo na hivyo kuboresha maisha ya wananchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, bajeti hii ni bajeti ya ujumla ya Serikali, kwa wale ambao hawatakuwa wamesikia mambo mengine yanayohusu maslahi ya wafanyakazi na mengine, hayo yataachiwa sekta husika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, naafiki!

(*Hoja Ilitolewa Iamuliwe*)

**SPIKA:** Ahsante. Ahsanteni sana. Hoja imeungwa mkono. Kwa hiyo, nachukua nafasi hii kwa niaba yenu kumpongeza sana Waziri wa Fedha kwa kusoma hotuba ndefu kuanzia asubuhi (Hali ya Uchumi) na sasa hivi Bajeti ya Serikali.

Waheshimiwa Wabunge, kama ilivyo ada, kuchangia hotuba hii tutaanza tarehe 15 Juni, 2011 kwa sababu tarehe 13 Juni, 2011 na tarehe 14 Juni, 2011 tutakwenda kwenye suala zima la kuchangia Mpango ambao utawasilishwa tarehe 13 Juni, 2011.

Lakini, kabla sijaendelea kusema haya yote, naomba niwatambue wageni waliopo. Nitatumia muda mfupi kwa kutaja kwa makundi kwa sababu muda hautoshi maana wote hawa niliowaalika miminikisema nimirambulishhe mtu mmoja mmoja hapa, itachukua saa nytingine moja. Mko tayari? Najua hapana, mmechoka sana. (*Makofi*)

Kwa hiyo, naomba wageni wetu mtuelewe. Tungependa kuwatambua mmoja mmoja, lakini hatuna muda wa kutosha. Nitakao watambua kwa kumtaja mmoja mmoja ni watatu tu:-

Kwanza kabisa, huyu ni mke mpPENDWA kabisa wa Mheshimiwa Mkulo na watoto wake. Alipo asimame pamoja na wajukuu kama wapo. Ninafanya hivyo kwa sababu ni kweli, angefanya *boycott* huyo, Hotuba hii isingetoka. (*Makofī/Kicheko*)

Mwingine ambaye nitamtambua ni Mheshimiwa Mama Tunu Pinda, Mke wa Waziri Mkuu. Yuko hapo. Mwingine nitakayemtambua ni Katibu Mkuu Kiongozi Mheshimiwa Phillemo Luhanjo. Baada ya hapo, kama nilivyosema, wageni wangu mtanisamehe sana maana ndiyo hali ilivyo.

Tunao mbele yetu hapa Makatibu Wakuu wa Wizara zote, halafu tunao Wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki, Wakuu wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama, Wakuu wa Mahakama, Viongozi wa Dini, Wakuu wa Vyombo vya Fedha, Waheshimiwa Mabalozi, naomba wasimame walipo, *can you please stand up all the Ambassadors and the High Commissioners present.* (*Makofī*)

Tunao wawakilishi wa Mashirika ya Umoja wa Mataifa (*United Nations Organizations*), naomba pia nao wasimame. Halafu tunao wawakilishi wa Umoja wa Ulaya (*European Union Delegation if they are there, they can stand up wherever you are!*) Karibuni sana. Tunaye Msajili wa Vyama vya Siasa nchini, kwa sababu ni siasa, asimame Mheshimiwa Tendwa. Kwa sababu moja ya muhimu pia, naomba Mheshimiwa Kamishna wa Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma naye asimame, Mheshimiwa Jaji Salome.

Tunaye Mkurugenzi wa TAKUKURU Dkt. Hosea, tunao Wajumbe wa Baraza la Vyama niliowatambulisha asubuhi, tuna Wakuu wa Mikoa, tuna Wakuu wa Wilaya za Karibu hapa wapo. Tuna viongozi wa Vyama vya Wafanyakazi. Tuna viongozi wa sekta binafsi, pia wapo. Halafu tuna viongozi wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, halafu tuna viongozi wa vymbo vya habari. Halafu, najua kuna wanafunzi na wageni wengine wote waalikwa. Nawashukuruni sana kwa kuja, maana hii ni shughuli kama nyie mngegoma kuja, basi tungekuwa tumesoma sisi wenyewe, ingepoteza ladha kidogo.

Lakini nawashukuruni sana kwa kuja kwenu hapa Bungeni. Tunaomba ushirikiano wenu kwa wakati wote. Kama nilivyosema, Bunge langu limegawanyika katika sekta mbalimbali. Kwa hiyo unaweza kukuta umeguswa na jambo fulani katika sekta yako. Kamati za Bunge zipo na tunagawa kile kitabu chetu na unaweza kuwafuata hao na wenyewe wakalifuatilia jambo lenu vizuri zaidi, likaingizwa katika utaratibu zilizopo. (*Makofī*)

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kueleza hayo, yapo, malalamiko. Waheshimiwa Wabunge wengine hawakupata vitabu hivi. Nimehakikishiwa na Mheshimiwa Wizara ya Fedha kwamba vitakuja kabla ya kesho. Sasa wale ambao hawana watafuata utaratibu wetu wa kupata vitabu.

Halafu nina tangazo lingine kwamba kesho tarehe 9 Juni, 2011 kuanzia saa tatu asubuhi tunakusudia kuwa na semina kidogo kuhusu ule mpango. Itakuwa ukumbi wa Msekwa kuanzia saa tatu. Itanza saa tatu na mpaka saa saba tutakuwa tumemaliza. Waheshimiwa Wabunge, tuko kazini. Naomba m jitahidi muweze kuwahi kusudi tuweze kupata kile tunachotaka kupata. Mpaka saa saba tutakuwa tumemaliza.

Halafu nimeombwa na Katibu wa Kamati ya Wabunge wote wa Chama cha Mapinduzi (CCM) kwamba kesho tarehe 9 Jun i, 2011 saa 11.00 jioni, Kamati ya Uongozi ya Chama cha Mapinduzi. Uongozi wa CCM siyo Uongozi wa Bunge, watakuwa na kikao chao katika Ukumbi wa Spika, Jengo la Utawala.

Halafu, ningependa kuwakumbusha kwamba Waheshimiwa Wabunge hasa wa Kamati ya Fedha na Uchumi, pia Kambi ya Upinzani wajaribu kuona kama wanapitia ule Mpango. Utasomwa tarehe 13 Juni, 2011. Lakini mkiweza kupitia na mkatoa maoni yenu, itakuwa vizuri sana kwa sababu siku ya Jumatatu, tarehe 13 Juni, 2011 baada ya kusomwa, Kamati inayohusika itabidi itoe maoni yake. Kambi ya Upinzani pia itatoa maoni kabla ya kuendelea kujadiliwa na Wabunge wengine. (*Makofi*)

Kwa hiyo, naomba wahusika wajiandae kusudi tuweze kuendesha shughuli zetu vizuri.

Waheshimiwa Wabunge na wageni waalikwa wote, baada ya kusema hayo naomba niwashukuru kwa jioni hii. Hatuna mengine. Naahirisha kikao cha Bunge mpaka siku ya Jumatatu, tarehe 13 Juni, 2011 saa tatu asubuhi. (*Makofi*)

*(Saa 11.25 jioni Bunge lilahirishwa mpaka siku ya Jumatatu,  
Tarehe 13 Juni, 2011, Saa tatu asubuhi)*